# UHAKIKI WA MAUDHUI NA MTINDO KATIKA *TIKITIMAJI*

NA

MARGARET MUTHONI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

NOVEMBA 2014

University of NAIROBI Library
0377642 4

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo chochote kingine kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

**Margaret Muthoni** Tarehe

______________________ 20/11/2014

(Mtahiniwa)

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Dkt. Evans M. Mbuthia** Tarehe

______________________ 19-11-2014

**Dkt. Amiri Swaleh** Tarehe

______________________ 21/11/2014

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu, marehemu babangu mpendwa Andrew M'mutia aliyeniwekea msingi thabiti katika masomo yangu na ambao umekuwa ngazi ninayoitumia kukwea hadi kufikia kiwango hiki na marehemu mama yangu mzazi, Sabera Ciomwenda kwa kunilea hadi aliponiacha bado nikiwa mtoto mdogo.Mungu aendelee kuwaweka mahali pema peponi.

## SHUKRANI

Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hekima ya kuendeleza masomo yangu katika utu uzima wangu.Shukrani za dhati pia ni kwa wasimamizi wangu,Dkt. Evans M. Mbuthia na Dkt. Amiri Swaleh walionielekeza vyema na kunisaidia kujipanga ili nikamilishe kazi hii kwa wakati uliotakikana.Nawashukuru wahadhiri wote walionifundisha tangu nilipojiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi mnamo mwaka 2012.Wahadhiri hawa ni Dkt. Evans Mbuthia na Dkt. Amiri Swaleh ambao pia waliteuliwa kuwa wasimamizi wangu, Dkt. Iribemwangi, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Kineene Wa Mutiso na Prof. John Habwe. Namshukuru Prof. Kineene Wa Mutiso kwa kuchukua hatua ya kutukutanisha na wanafasihi wengine akiwemo Prof. Kithaka Wa Mberia na Omar Babu kwani maelezo yao kuhusu fasihi yalinifaa sana wakati wa kuandika kazi hii.

Namshukuru mama yangu mlezi, Rebecca Mwokabira aliyehakikisha ya kwamba nilipata malezi na mafunzo mema nilipokuwa mtoto hadi nilipohitimu shahada yangu ya kwanza.Shukrani za dhati pia ni kwa mume wangu mpendwa, Joseph Mwithalii kwa kuvumilia kuachwa pweke nilipokuwa nikihudhuria masomo mbali na nyumbani huku akiwatunza watoto wetu.Nawashukuru watoto wangu, Makena, Kagwiria, Kaura, Mutethia na Ntinyari kwa kuvumilia kuachwa nyumbani bila mwongozo wangu kila walipokuwa likizoni nami chuoni nikisoma.

Mungu awabariki nyote.

# IKISIRI

Tumefanya Uhakiki wa maudhui na mtindo katika *Tikitimaji*.Tumeangazia maudhui mbalimbali na lugha ya kitamathali iliyotumika kuendeleza dhamira na maudhui hayo. Utafiti wetu ulijikita katika *Tikitimaji* ila ilipotubidi kutoa mifano tuliangazia kazi nyingine kwa ufupi sana.Uchanganuzi wetu uliongozwa na nadharia mbili: Uhalisia uliotuongoza katika uchanganuzi wa maudhui na Umitindo uliotuongoza katika uchanganuzi wa mtindo.

Katika utafiti wetu tuling'amua ya kwamba, jamii ya *Tikitimaji* ilikumbwa na changamoto nyingi ambazo wanajamii wanakabiliana nazo ili maisha yao yaweze kutengenea.Baadhi ya changamoto hizi ni uharibifu na uchafuzi wa mazingira, utelekezaji wa watoto, udhalimu na unyanyasaji, miundo msingi mibovu na mfumo mbaya wa uchukuzi, umaskini na athari zake, mchango wa vijana katika ujenzi wa jamii mpya na jinsi wanavyoshirikiana na wazee katika suala hili.

Maudhui haya yameendelezwa kwa kutumia lugha yenye mvuto na mnato unaowavutia wasomaji na kuipa riwaya hii ujumi mwafaka.

Utafiti wetu umegundua kwamba, masuala yanayowakabili wanatikitimaji ni ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ambapo walala heri wanawanyanyasa walala hoi, jambo linalozua migogoro baina ya makundi haya mawili.Kundi la walala heri linapigania kuendeleza unyanyasaji nalo la walala hoi likikazana kujikomboa.

# YALIYOMO

Ungamo ........................................................ ii

Tabaruku ........................................................ iii

Shukrani ........................................................ iv

Ikisiri ........................................................ v

Yaliyomo ........................................................ vi

**SURA YA KWANZA ........................................................ 1**

1.0 Utangulizi ........................................................ 1

1.1 Tatizo la Utafiti ........................................................ 3

1.2 Madhumuni ya Utafiti ........................................................ 4

1.3 Maswali ya Utafiti ........................................................ 5

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........................................................ 5

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti Wetu ........................................................ 7

1.6 Msingi wa Nadharia ........................................................ 7

1.6.1 Nadharia ya Uhalisia ........................................................ 7

1.6.2 Nadharia ya Umitindo ........................................................ 11

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ........................................................ 14

1.8 Mbinu za Utafiti ........................................................ 19

1.9 Hitimisho ........................................................ 19

**SURA YA PILI** .......... **21**

**UCHANGANUZI WA MAUDHUI KATIKA *TIKITIMAJI*** .......... **21**

2.0 Utangulizi .......... 21

2.1 Uharibifu na Uchafuzi wa Mazingira na Athari Zake. .......... 22

2.2 Utelekezaji wa Watoto .......... 25

2.3 Udhalimu na Unyanyasaji .......... 28

2.4 Ukosefu wa Kazi na Athari Zake .......... 31

2.5 Nafasi na Umuhimu wa Vijana Katika Jamii .......... 34

2.6 Hali Mbaya ya Mfumo wa Uchukuzi na Miundo Msingi .......... 36

2.7 Nafasi na Hadhi ya Mwanamke Katika Jamii .......... 38

2.8 Ushirikiano wa Vijana na Wazee Katika Ujenzi wa Jamii Mpya .......... 41

2.9 Kutowajibika, Uzembe na Ujuhali wa Viongozi .......... 46

2.10 Umaskini na Athari Zake .......... 51

**SURA YA TATU** .......... **55**

**UCHANGANUZI WA LUGHA YA KITAMATHALI KATIKA *TIKITIMAJI*** .......... **55**

3.0 Utangulizi .......... 55

3.1 Matumizi ya Tashbihi .......... 56

3.2 Methali .......... 66

3.3 Misemo .......... 75

3.4 Tashihisi .......... 80

3.5 Nidaa .......... 84

3.6 Kuchanganya Ndimi ........................................................................................89

3.7 Sitiari........................................................................................................93

3.8 Takriri ......................................................................................................95

3.9 Hitimisho..................................................................................................98

**SURA YA NNE ..........................................................................................100**

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..........................................................100**

4.0 Utangulizi................................................................................................100

4.1 Hitimisho.................................................................................................100

4.2 Mapendekezo ..........................................................................................104

**MAREJELEO ..............................................................................................105**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Mada yetu ni Uhakiki wa maudhui na mtindo katika *Tikitimaji.Tikitimaji* ni riwaya iliyoandikwa na Kyalo Wadi Wamitila mnamo mwaka 2013.Kwa mujibu wa Wamitila (2002:5),riwaya ni kazi iliyoandikwa kwa mtindo wa kinathari ambayo ina urefu wa kiasi fulani na uchangamano wa kimtindo na kidhamira na inashughulikia maswala kadha katika mtazamo mpana wa wakati na matumizi mapana ya mandhari.Riwaya pia ina sifa ya kuwa na kina cha uhusika kinachohusisha undani wa kisaikolojia na ubainishaji wa misukumo ya kitendaji (Wamitila 2008:114).*Tikitimaji* ni kazi inayosheheni baadhi ya sifa tulizozitaja, jambo lililotufanya kuiainisha katika utanzu wa riwaya.

Kazi hii imeshughulikia masuala kadha katika mtazamo mpana wa wakati na mandhari kwani mwandishi ameyaangazia mambo kama vile uharibifu wa mazingira, utelekezaji wa watoto, utabaka, unyanyasaji, suala la miundo msingi, mfumo wa uchukuzi na mengine mengi.Kazi hii ina mwanda mpana wa kiwakati na kimandhari kwa kuwa mwandishi amewasawiri wahusika wake kwa njia inayotuelekeza kujua kwamba wamekuwa wakikua kimwili na kimawazo pia.Tunaelezwa kupitia mbinu rejeshi kuwa wahusika wakuu (Zinji, Maya, Sapna na Kombo) wamekulia katika makao ya watoto ya Gwadalupe na sasa wao ni watu wazima waliohitimu masomo yao.Kupitia mbinu rejeshi pia tunaelezwa kuwa Mama Rehema anaendelea kuzeeka huku akihudumu katika makao ya watoto.Kauli hii inamaanisha kwamba mama huyu amehudumu katika makao haya ya watoto kwa muda mrefu.

*Tikitimaji* ni kazi yenye mandhari mapana kwa sababu mwandishi ameangazia maeneo mbalimbali ya nchi ya Tikitimaji.Baadhi ya mandhari haya ni Mto Unasi, jiji la

Tikitimaji, Ganjoni, Langulo, Mlima Tirimacho na mengineyo.Mwandishi ameangazia shughuli zilizokuwa zikiendelezwa katika maeneo aliyoyateua kuwa mandhari yake na ambazo zinaendeleza maswala aliyokusudia kuyamulika katika kazi yake, suala kuu likiwa ni uharibifu na uchafuzi wa mazingira ambalo limeangaziwa katika mandhari mapana ya mji wa Tikitimaji na maeneo yanayouzunguka.Katika juhudi za kuendeleza shughuli mbalimbali katika maeneo mbalimbali, mwandishi anawateua wahusika kadha anaowatumia kuwasilisha ujumbe wake.

Wahusika wakuu walioteuliwa na mwandishi ili kuendeleza dhamira na maudhui yake ni vijana wanne wanaosafiri kwenda Tikitimaji ili kujisaka na kutaka kuielewa hali ya nchi yao. Vijana hawa ni: Zinji (mwanahabari), Sapna (mwanamazingira), Kombo (askari) na Maya (msomi wa masuala ya kifasihi na mfanyakazi katika maktaba mojawapo ya kitaifa).Mwandishi anawateua wahusika wadogo na wasaidizi pia ili wamsaidie kutimiza malengo yake.Wahusika hawa ni Mzee Jududi, Mzee Dhamiri, Shamsi, mamake Shamsi, Mwalimu Insafu, Mzee Jarisa, Bwana Nia, Jitikiti ambaye anajulikana kwa majina mengi ya lakabu na wengine wengi.

Maudhui ni jumla ya masuala yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi.Masuala haya hutokana na jinsi mwandishi anavyoikuza mada ambayo ni msingi wa utunzi wa kazi yake.Wazo hili kuu hujulikana kama dhamira na ndilo huitawala kazi ya kifasihi kutoka mwanzo hadi mwisho.Wazo hili hukuzwa kwa njia zilizo wazi, mojawapo ikiwa matumizi ya anwani ya kitabu kinachohusika.

*Tikitimaji* ni anwani ya kazi tunayoichunguza na ndiyo inayoitawala kazi nzima kwa kuwa matukio yote yanatendeka Tikitimaji ambayo ni nchi ya kubuni inayokumbwa na

matatizo kadha.Zinji, Sapna, Maya na Kombo wanazuru sehemu nyingi za mji wa Tikitimaji na wanagundua kuwa, ingawa viongozi wanachangia kuwepo kwa matatizo nchini Tikitimaji, pia wananchi wenyewe wana mchango wao.

Kama wanavyosema Njogu na Chimerah (1999:384), mtindo ni mseto wa fani na maudhui.Hii inamaanisha kwamba mtunzi wa kazi ya sanaa ana namna yake ya kuijenga kazi yake ili kuzioanisha fani na maudhui anayoyateua.Wahakiki hawa wanazidi kutoa maelezo kuwa mtindo ni ujuzi wa kujieleza na kuwa vipengele vyake ni kama vile: Tashbihi, tashihisi, tasfida n.k.Kwa kuzingatia maelezo haya tunaona kwamba mtindo ni dhana inayotumiwa kurejelea mbinu tofauti tofauti za kifasihi na ambazo zinadhamiriwa kuwa na athari fulani za kiujumi kwa wasomaji, zinavyotumiwa katika matini za kifasihi ili kuwasilisha ujumbe wa msanii.Mtindo hutumiwa kupeleka mbele maudhui na dhamira pamoja na kusanifu kazi nzima ili ufasaha wa msanii uweze kujitokeza.Tamathali za usemi ni sehemu ya mtindo katika kazi ya kifasihi na ndilo suala tuliloshughulikia katika kazi yetu.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Katika karne hii, matatizo mengi yanaendelea kuukumba ulimwengu na mengine kuwa tishio kubwa na balaa inayoweza kusababisha maangamzi ya mwanadamu. Binadamu ameyaingilia mazingira kwa njia hasi akidhani kwamba anajinufaisha bila kufahamu kwamba anajiangamiza mwenyewe.Watu binafsi na pia makundi ya kulinda na kuhifadhi mazingira yamejitokeza na kupaaza sauti kupitia vyombo vya habari na makongamano mbalimbali ili kuwafundisha watu umuhimu wa kuyahifadhi na kuyasafisha mazingira.

Kwa kuwa hali ya uharibifu wa mazingira imezidi kukithiri, wasanii nao wamechukua hatua ya kuyaangazia masuala yanayohusiana na uharibifu huu wa mazingira ili kutoa mchango wao katika kuwahamasisha walimwengu kuhusu hatari zinazoweza kutokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira.Kwa kuwa uharibifu na uchafuzi wa mazingira ni suala ibuka ulimwenguni na kuwa dhamira ya mwandishi ni kuangazia athari mbaya za uchafuzi na uharibifu wa mazingira, tumeamua kuihakiki *Tikitimaji* ili kuelewa jinsi mwandishi anavyoliangazia suala lenyewe na funzo ambalo msomaji anaweza kulipata kutokana na usomaji wa kazi hii.

Katika hali halisi ya maisha, tumeshuhudia maandamano yanayoandaliwa na wanaharakati wa kulinda mazingira nchini mwetu na upinzani wanaokumbana nao hasa kutoka kwa viongozi lakini wanaharakati hawa hawakati tamaa ila wamezidi kuwa na ari ya kuendeleza juhudi zao.Matukio kama haya katika jamii ndiyo huwachochea wanafasihi kuandika ili kuyaangazia kisanaa ili hadhira yao ipate kuyaelewa kwa undani na yapate kuwaathiri ili watekeleze majukumu yao ipasavyo popote walipo.

Katika kuyaangazia masuala ambayo mwandishi wa *Tikitimaji* ameyamulika pamoja na mtindo alioutumia kuyamulikia tumeamua kutumia nadharia za Uhalisia na Umitindo katika uchanganuzi wetu wa *Tikitimaji*.Pengo tunalotaka kuliziba kwa utafiti huu ni kumulika maswala yanayohusu mazingira katika fasihi kama yanavyojitokeza katika *Tikitimaji* na mtindo uliotumika kufikia lengo hili.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Tunadhamiria kuchambua na kuchanganua *Tikitimaji* kimaudhui na kimtindo ili:

(i) Kubainisha na kufafanua kwa kina maudhui na mtindo wa kazi hii.

(ii) Kuchunguza na kubainisha jinsi maudhui ya *Tikitimaji* yanavyoakisi hali halisi ya maisha ya binadamu.

(iii) Kubainisha kufanikiwa au kutofanikiwa kwa mwandishi katika uwasilishaji wa kazi yake.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Maswali yafuatayo ndiyo yatakayotuongoza katika utafiti wetu:

(i) Msanii ameteua mbinu zipi za kimtindo na zinaafikianaje na maudhui anayoyaangazia katika kazi yake?

(ii) Je, mwandishi wa *Tikitimaji* ameangazia maswala ambayo yanaakisi hali halisi ya maisha ya binadamu?

(iii) Je, mwandishi wa *Tikitimaji* amefanikiwa katika uwasilishaji wa kazi yake?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Tumechagua mada hii kwa sababu mtindo na maudhui ya *Tikitimaji* yanadhihirisha hali halisi ya maisha katika jamii zetu.Katika kazi nyingi za kifasihi waandishi wameshughulikia masuala yanayopatikana katika mazingira halisi anamojipata binadamu. Masuala yaliyoangaziwa na mwandishi ni pamoja na uongozi mbaya, utabaka, ukosefu wa kazi, utelekezaji wa watoto na uyatima, nafasi ya vijana na wanawake katika jamii na uharibifu na uchafuzi wa mazingira miongoni mwa mengine mengi.

Licha ya maandishi haya yote yaliyoandikwa ili kuwazindua wanajamii na pia kuwakashifu viongozi madhalimu, bado matatizo haya yanazidi kuwaathiri vibaya

wanajamii na hasa wanyonge wanaodhalilishwa na viongozi hawa madhalimu. Ujuhali wa viongozi pia umesababisha uharibifu na uchafuzi wa mazingira unaotishia kuwafagia wanadamu ulimwenguni kwa kuwa chemichemi na vianzo vya maji vinaendelea kuharibiwa na mito kuendelea kukauka.

Kama asemavyo Caleb (2013:4), akimnukuu Hough (1962),

> Hakuna kazi yoyote ya uhakiki wa fasihi iliyokamilika. Uhakiki haushughulikiwi wakati mmoja na kuisha kabisa kwani hutegemea historia na mazingira ya kijamii katika kila kipindi kipya cha historia.

Fasihi ya wakati uliopita yafaa ichunguzwe upya kwa kuwa mabadiliko hutokea katika maisha ya binadamu na kwa sababu hii, waandishi nao huandika kazi zao wakizingatia matukio ya wakati na mazingira yanayowazunguka.Mwandishi wa *Tikitimaji* ameangazia uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kuwa suala hili limekithiri wakati huu kuliko ilivyokuwa zamani katika jamii zetu na ulimwengu kwa jumla.

Kauli hii imetupatia ari ya kufanya utafiti kuhusu maudhui na mtindo katika *Tikitimaji* ili kumulika jamii, na mwonoulimwengu wake kuhusu mambo yanayoizunguka hasa katika karne hii ya Ishirini na Moja, ambapo *Tikitimaji* imeandikwa na kuchapishwa.Jambo lingine lililotupelekea kuchagua mada hii ni kuwa fasihi ya Kiswahili inaendelea kupewa umuhimu mkubwa katika shule za sekondari, vyuo vya walimu na hata vyuo vikuu nchini humu, Afrika ya Mashariki na ulimwenguni kote. Hali hii ndiyo iliyotufanya tutake kuchangia katika uchanganuzi wa vipengele vya maudhui na mtindo katika *Tikitimaji*, ili kuendeleza uhakiki na uelewekaji wa fasihi ya Kiswahili kote ulimwenguni. Tuliposoma *Tikitimaji* tuligundua kuwa, lengo kuu la msanii ni kuangazia jinsi mazingira

yalivyoharibiwa na kuchafuliwa.Kwa kuwa suala hili limekithiri sio tu nchini Kenya bali kote ulimwenguni, ni tatizo linalopaswa kutiliwa maanani na wanajamii wote duniani.

Tunaamini kuwa matokeo ya utafiti wenyewe yatasahilisha uelewa wa ujumbe wa msanii wa kazi tunayoihakiki kwa wasomaji.Hata wale wanaosoma kazi hii kwa kutaka kuburudika tu, wakisoma uhakiki huu, hawataburudika tu, bali wataelimika na kuelewa mambo mengi ambayo hawangeyaelewa barabara kabla ya kuisoma.

## 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti Wetu

Katika utafiti huu, tumejishughulisha na uhakiki wa *Tikitimaji* kimaudhui na kimtindo.Hata hivyo, ilipobidi tulitaja kazi nyingine zilizoandikwa na waandishi wengine kwa minajili ya kutoa mifano inayohusiana na kazi yetu.Tumejikita katika uchanganuzi wa maudhui na kipengele cha kimtindo ambacho ni tamathali za lugha au lugha ya kitamathali. Ingawa haja yetu si kuangazia wahusika, ilibidi tuwataje baadhi yao hapa na pale ili kufafanua mambo kwa ukamilifu.

## 1.6 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili:Uhalisia na Umitindo.Nadharia ya uhalisia imetuongoza katika uhakiki wa maudhui nayo ya umitindo imetuongoza katika uchanganuzi wa mtindo ambapo tumeshughulikia lugha ilivyotumika katika *Tikitimaji*.

### 1.6.1 Nadharia ya Uhalisia

Kimsingi, tunaweza kusema kuwa nadharia hii liliwekewa msingi na Hegel (1979) katika kitabu chake kinachojulikana kama *Introduction To Aesthetics*.Mtaalamu huyu

alipendekeza matumizi ya neno uhalisia kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu na maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na hali aliyomo.

Kulingana na Msokile (1993:106), Uhalisia ulianza mwaka 1820 B.M. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa inafaradhiwa iseme ukweli, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira.Inapendekeza ujenzi wa wahusika unaolingana na hali halisi, yaani mhusika awe na sura ile ile ya maisha ya kawaida kwani sanaa inafaa ieleze ukweli na iweze kueleweka.Kwa hivyo, dhana ya uhalisia hutumiwa kuelezea aina ya mtazamo wa kifasihi unaochukulia kazi za kifasihi kama zinazoakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi.Kazi za kihalisia zinatarajiwa kuakisi hali halisi za maisha katika jamii husika.

Kama asemavyo Wamitila (2002:116), Wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi, huyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao, na husawiri na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida wakati wa kuandika kazi zao.

Kama wasemavyo Wafula na Njogu (2007:63), Uhalisia unahusishwa pia na kipindi maalum cha kihistoria katika jamii za Ulaya.Kipindi hiki kilianza mwanzo mwanzo wa karne ya kumi na tisa nchini Ufaransa na kilihusishwa na waandishi kama vile Balzac, Stendhal na Flaubert.Waandishi hawa walisisitiza maelezo ya 'kikweli' katika kazi zao na waliamini kuwa dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo.

Msingi mkuu wa Uhalisia ni usimulizi wa kimuhakati.Huu ni usimulizi ambao unasimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii (Wamitila 2002:115).Mwandishi kwa

hivyo, anapaswa kuyaakisi maisha ya jamii katika ngazi ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa.Uhalisia husisitza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa.Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishaji wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii.

Waandishi wanaoandika katika msingi huu wanatarajiwa kwa hivyo, kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisi wa jamii ya mwandishi anayehusika.Mwandishi anayeandika kwenye misingi ya tapo hili analazimika kuuteua mtazamo wa kisimulizi ambao unamwezesha kuyawasilisha maisha kwa 'usahihi'.Mwandishi anatilia mkazo wahusika katika hali za kawaida za maisha, matukio na mandhari ya kawaida au yanayoweza kuonekana katika jamii.Huu ndio msingi hasa wa kauli ya Lenin kuwa fasihi ni kioo cha jamii.Haja kubwa ya kuigiza ilikuwa kuonyesha picha ya mazingira ambamo jamii inapatikana mathalan, kioo kinavyotumika kuonyesha picha za mwanadamu.

Mhakiki wa kihalisia alimtathmini mwandishi kwa namna ambavyo huyo mwandishi alijibidiisha kuonyesha ukweli.Kulingana na wahakiki wa kihalisia, mwandishi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku (Wafula na Njogu 2007).

Kigezo muhimu katika uwasilishaji huu wa maisha katika kazi ya kihalisia ni dhana ya ushabihikweli.Hii inamaanisha kwamba, msisitizo wake mkubwa upo kwenye juhudi za kuukaribia ukweli uliopo katika jamii inayohusika.Kwa kuuzingatia mtazamo huu kazi nyingi zinakwepa matukio au mandhari yasiyokuwa ya kawaida.

Waandishi wa kihalisia huchukulia kuwa picha au hali zinazopatikana kwenye kazi zao pamoja na yaliyomo huwiana na ukweli wa jamii zinazohusika.Sifa hii pia inadhihirika

katika *Tikitimaji* kwa kuwa masuala yanayoangaziwa yanadhihirika wazi katika jamii ya mwandishi na ulimwenguni kwa jumla.

Kulingana na Wamitila (2003:272), mtaalamu mwingine anayehusishwa na uhalisia ni mfuasi wa Marx kutoka Hungary anayejulikana kama Georg Lukacs.Mhakiki huyu anauona uhalisia kama lengo kuu la msanii au mwandishi.Mhakiki huyu ana maoni kuwa mwandishi anasukumwa au anapaswa kusukumwa na nia ya kuusawiri uhalisi katika ukamilifu wake katika wakati fulani maalum (wakati anaandika).

Katika kazi za kihalisia waandishi huonyesha misimamo yao juu ya lile wanalolizungumzia, ambapo, pamoja na msanii kujizatiti kuchora hali halisi ya maisha kama yalivyo, hutetea watu fulani na kuwashambulia wengine kutegemea msimamo wake.

Kulingana na maelezo haya, inadhihirika kwamba, uhalisia unapinga aina yoyote ya majaribio, ambapo matukio ya kinjozi au yanayokiuka uhalisia hujitokeza katika kazi za kifasihi.Hivyo, uhalisi wa maisha katika jamii huwa ndio msingi mkubwa wa uandishi wa kihalisia ambapo tukio, mhusika au mandhari huelezwa kama vya kihalisia ikiwa vinafanana na sura fulani ya maisha ya kila siku.

Nadharia hii imetufaa katika utafiti huu ikizingatiwa kuwa, masuala ambayo mwandishi anayaangazia katika kazi hii yanaendelea kumkumba binadamu kote ulimwenguni hata katika karne hii ya Ishirini na Moja. Nadharia hii, imetufaa katika uhakiki wa maudhui ambayo ni masuala anayoyaangazia msanii katika kazi nzima.Yanayotendeka katika *Tikitimaji*, ni mambo tunayokumbana nayo katika hali halisi za maisha yetu ya kila siku.

### 1.6.2 Nadharia ya Umitindo

Nadharia ya umitindo imetuongoza katika uchambuzi na uchanganuzi wa mtindo katika *Tikitimaji.*Tumeamua kuongozwa na nadharia hii kwa sababu kipengele cha mtindo tunachokiangazia ni tamathali za usemi au lugha ya kitamathali ilivyotumiwa katika *Tikitimaji.*

Umitindo ulianzishwa mnamo mwaka wa 1904 nchini Urusi na ulilenga kuainisha sifa za kisanaa zinazopatikana katika fasihi kama taaluma. Mwasisi wa nadharia hii alikuwa Viktor Shklovsky ambaye aliandika makala '*Ufufuo wa Neno*'alimozungumzia umuhimu wa lugha katika kueleza maana ya fasihi.

Maelezo haya yanatiliwa nguvu na Mbatiah (2001:86), anaposema kuwa nadharia hii iliibuka mjini Moscow katika miongo miwili ya kwanza ya Karne ya 20 na iliyokuwa na mwelekeo kwamba, fasihi ni matumizi ya kipekee ya lugha ambayo ni tofauti na lugha ya kawaida na kuwa fasihi humwezesha msomaji kukiona kitu, jamii au tajriba fulani kwa mwanga mpya.Mawazo haya ya Mbatiah yanashabihiana na yale ya Shklovsky kuwa umuhimu wa sanaa ni kukifanya kitu kionekane kama kisicho cha kawaida na kwa namna hii kusawiriwa kwa njia mpya.

Waasisi wa umitindo waliegemea sana upande wa ushairi kwa kuwa, kuanzia miaka ya 1915-21, utanzu wa ushairi ulitumiwa sana kwa sababu, kinyume na riwaya, mashairi yalikuwa na wepesi wa kuwasilishwa mbele ya hadhira, njiani, mikahawani au hata katika mikutano ya wafanyakazi.Walieleza vipengele vya kiarudhi vya ushairi kama vile sauti, vina, mizani, na wizani.Aidha, walitoa maelezo ya kijumla kuhusu namna mashairi yalifaa kutungwa kwa ufundi na uhuru wa kutumia lugha.

Kwa mantiki hii, kama asemavyo Wamitila (2003:189), wanaumitindo walifafanua kuwa kilichokuwepo ni ushairi wala sio washairi au msanii anayehusika, yaani, kilichokuwa muhimu ni kazi maalum za kifasihi wala sio athari zake kwa wasomaji. Lengo lao lilikuwa kutazama fasihi kama sanaa ya maneno wala sio kubainisha mitazamo ya kijamii. Hata hivyo, inatupasa kukumbuka kuwa, kutumia lugha anavyopenda msanii haipo tu katika ushairi bali pia katika kazi nyingine za kifasihi ikiwemo riwaya.Wanaumitindo walijihusisha na tanzu za kinathari au kiusimulizi baadaye na wakaelezea jinsi vipengele vya fani vilivyoainishwa.

Kanuni kuu ya umitindo ilikuwa kuichunguza fasihi kwa mtazamo wa kisayansi.Shabaha ya kijumla ya wanaumitindo katika kuichunguza fasihi kisayansi ilihusu uchunguzi wa lugha na uamili wake katika kuipa maana kazi fulani ya kifasihi.Haja yao ilikuwa kubuni sayansi huru ya lugha ambayo ingezitalii kazi za kifasihi kwa misingi ya kiisimu.Ili kuitalii lugha kisayansi, iliwabidi wanaumitindo kutafuta sifa za kijumla au za kawaida za fasihi.Hivyo Jakobson, mnamo mwaka wa 1921, akaonelea kuwa ufasihi uwe msingi wa sayansi ya fasihi badala ya kuitazama kwa ujumla wake au kwa kuzingatia kazi za kifasihi za watu binafsi.

Katika uchunguzi wao wa fasihi, Wana-umitindo walitilia maanani miundo ambayo inabainisha fasihi na amali za binadamu.Walisisitiza kuwa fasihi inapaswa izingatie mielekeo ya fasihi.Aidha walisisitiza haja ya kuupa nafasi kuu ukweli wa fasihi.

Ili kutimiza malengo haya, mitindo mbalimbali ilikuzwa.Juhudi zao zilihusisha ufafanuzi wa seti za tabia zinazohusiana na lugha ya kishairi ambayo ni ya ushairi au nathari inayotambulika kutokana na ufundi wa kisanaa.Kikundi kilichoongozwa na Viktor

Shklovsky kilitilia maanani njia rasmi na iliyolenga kuzingatia ustadi wa kiufundi na mbinu.Kazi za kifasihi, kulingana na mtindo huu zinashabihiana na mashine.Yaani huwa ni matokeo yanayosababishwa na utenda kazi wa binadamu, kama ambavyo ufundi maalumu unabadili malighafi hadi kuwa utaratibu changamano uwezao kutenda kazi maalumu.

Kama asemavyo Wamitila (2002), mtazamo huu huiondoa kazi iliyobuniwa ya fasihi kutoka kwa uhusiano wake na mwandishi, msomaji na usuli wa kihistoria.Wakati msomaji anapokumbana na miundo ya uchimuzi katika matini anayoisoma, hatambui tu miundo hii, bali hutafakari motifu kuu ya matumizi ya mbinu hizo katika matini husika.Katika kujaribu kupata motifu hii, msomaji huweza kupata maana halisi ya ujumbe ambao umewasilishwa na msanii katika kazi ya kinathari au ushairi.

Katika uhakiki wa *Tikitimaji,* tutabainisha matumizi ya lugha ya kitamathali na jinsi inavyooana na maudhui ili kutimiza malengo ya mwandishi.Tutafanya hivi kwa sababu, mojawapo ya sifa bainifu za kazi ya sanaa ni kuwa na ukamilifu wa kiasi kwamba, haiwezi kugawika katika vijisehemu hasa wakati wa kuiandika.Hii ina maana kuwa mwandishi wa riwaya au tamthilia hawezi kuandika huku akitenganisha maudhui na mtindo unaotumika ila huandika kazi inayofungamanishwa pamoja.Fasihi kama vilivyo viungo vya kibayolojia inao muundo uliokamilika, yaani sehemu zake zimefungamanishwa kwa kufuata mfumo fulani, kama vile viungo vya binadamu vinavyoshirikiana katika utekelezaji wa majukumu muhimu.

Jakobson alipoandika kuhusu dhana ya ufasihi, alitilia mkazo wazo kuwa, nia ya usomaji wa kifasihi sio kujihusisha na fasihi kwa jumla bali ni kujihusisha na ufasihi.Istilahi hii

'ufasihi' inarejelea sifa za kifasihi zinazoifanya matini fulani kuchukuliwa kama fasihi, yaani matumizi ya kipekee ya lugha katika fasihi (Mbatiah, 2001:86). Kwa Wanaumitindo, matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha huipa fasihi upekee wake na kuitofautisha na aina nyingine za mawasiliano. Kwa hivyo sifa za kifani zilipata athari kubwa katika kuipa maana kazi fulani ya kifasihi kutokana na dhana ya ufasihi.

Ufasihi unaohusishwa na lugha inavyotumika katika kazi ya sanaa ndio uliotuelekeza kutumia nadharia hii ya Umitindo katika uchanganuzi wa *Tikitimaji* kwa sababu lengo letu lilikuwa kuchunguza jinsi mwandishi alivyotumia lugha ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Tumeangazia tamathali za usemi alizozitumia mwandishi wa *Tikitimaji* na jinsi alivyokiuka hali ya kawaida ya kutumia lugha ili kuleta dhana ya ufasihi katika matumizi haya ya lugha.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili

Katika sehemu hii tumerejelea kazi zilizoandikwa kuhusu somo letu.Njogu (1997:1) anaeleza kuwa kila taifa duniani lina fasihi yake (iwe ni fasihi simulizi au andishi).Naye Wamitila (2008:2), anatoa maelezo kuwa fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa namna maalumu, inayoathiri na kupitisha ujumbe fulani unaomhusu binadamu au wenye maana fulani, inayohusishwa na matini au utungo unaotambuliwa kama wa kifasihi.Maelezo ya Njogu na ya Wamitila kuhusu dhana ya fasihi yanalingana kwa kuwa Njogu anaieleza dhana ya fasihi kama chombo cha jamii kinachotumia lugha kibunifu ili kusheheni imani na matukio katika jamii husika.Suala la lugha limesisitizwa na wahakiki hawa kuwa ni muhimu lakini sharti tukumbuke kuwa si lugha tu bali lugha ya kisanaa.

Sataalamu wa kazi za kifasihi wanakubaliana kuwa kazi yoyote ile ya kifasihi huwa na sifa maalumu za urembo ambazo huitofautisha kazi hiyo na nyingine ambazo si za kifasihi. Huu ndio msingi wa kuwa na dhana ya umbuji, ambayo ni dhana inayotokana na utanzu wa kifalsafa unaomulika urembo na hupania kuyakinisha sifa za urembo/umbuji katika kazi ya kifasihi.

Maelezo haya ya Wamitila na Njogu kuhusu dhana ya fasihi na lugha ya kiubunifu itumikayo katika sanaa hii, yametufaa katika utafiti wetu kwa sababu lugha ya kifasihi tuliyoichunguza katika *Tikitimaji* ni chombo kinachotumika katika jamii ili kuwasilisha ujumbe kwa njia inayopunguza makali ya ujumbe husika hasa kwa walengwa wanaokashifiwa hivi kwamba, hata ujumbe huo ukiwa mkali hupokelewa na walengwa hao na kuwafunza maadili fulani. Katika *Tikitimaji*, mwandishi ametumia lugha kwa njia hii na ameweza kuwasilisha ujumbe wake kwa walengwa wote na huenda amewaathiri kwa njia inayotakikana ili kila mmoja atekeleze wajibu wake katika jamii yake.

Yaliyoandikwa kuhusu dhima ya fasihi katika jamii, yametufaa kwa kuwa kazi tunayoihakiki sharti iwe na manufaa fulani katika jamii. Kama tujuavyo, msanii haandiki kutokana na ombwe tupu. Sharti awe na jambo analotaka kuliwasilisha kwa hadhira yake ama kwa njia ya maandishi au masimulizi. Kimsingi, tunaweza kujiuliza maswali yafuatayo ili yaweze kutuelekeza kwenye dhima ya fasihi: Je, msomaji aliyesoma kazi za kifasihi huona tofauti gani na yule ambaye anasoma matini nyingine? Ni nini hasa kinachotuvutia au kutufanya tusome kazi za kifasihi?

Fasihi ina dhima ya kuwapevusha wanajamii na kuwafanya waiangalie jamii yao kwa jicho pevu. Hii itakuwa fasihi ambayo ni ya uzinduzi inayoamsha fikira na hisia za

wasomaji.Baadhi ya wahakiki huamini kuwa fasihi inapaswa kutumiwa kwa njia chanya kumhamasisha na kumtia ari msomaji na mwanajamii akosoe, akemee, adadisi na kukataa mfumo unaomdhalilisha kama kiumbe. Fasihi inayoyamulika matatizo yanayowakumba wanajamii inapaswa kuwazindua na kuwatia hamasa wanajamii hao wajitahidi kubadilisha hali inayowapata (Wamitila 2008).Jukumu hili linatekelezwa katika *Tikitimaji.*

Caleb (2013), ameshughulikia matatizo yanayowakumba wanawake katika tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee* akiongozwa na nadharia ya Sosholojia.Katika kazi yake anaeleza nafasi ya mwanamke katika jamii anaposema kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe dhaifu.Ingawa tunakubaliana na Caleb, tunaona kwamba, katika karne hii ya Ishirini na Moja, juhudi nyingi zimefanywa na zinazidi kufanywa kuona kwamba, hali hii ya kumchukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu imebadilishwa ili kumpa nafasi sawa na binadamu mwenzake wa kiume.Kazi hii ya Caleb inatufaa kwa kuwa, inaangazia nafasi ya mwanamke katika jamii ya miaka ya themanini ambapo tamthilia mbili anazozishughulikia ziliandikwa.Ingawa hadi sasa, mwanamke hajakombolewa au kujikomboa kikamilifu, juhudi nyingi zimefanywa na zinazidi kufanywa ili kumkomboa.Katika *Tikitimaji*, wahusika wanawake wamepewa nafasi yenye heshima na baadhi yao wanatekeleza majukumu muhimu sana katika jamii zao.

Kulingana na Caleb (2013:8), akimnukuu Sutherland (1957), "jinsi ambavyo mwandishi alivyoandika hutegemea kipindi alichoandika, tabaka ambamo alizaliwa, elimu aliyopata pamoja na dini yake." Kauli hii ya Sutherland inatufaa kwa kuwa, kazi ya mwandishi aghalabu, huangazia masuala yanayoikumba jamii ya mtunzi katika kipindi husika.Jambo hili linadhihirika katika *Tikitimaji* kwani masuala anayoyaangazia mwandishi,

yanajitokeza katika karne hii zaidi ya vile ilivyokuwa katika karne zilizopita.Mazingira yamezidi kuchafuliwa kote ulimwenguni na uharibifu wake una madhara mengi kwa binadamu na kwa viumbe wengine.

Kamunde (1983) amejadili 'unyonge' wa kiuchumi uliopo katika tabaka la chini na 'unyonge' wa tabia katika tabaka la juu kama ujitokezavyo katika *Utengano* (1980), *Asali chungu* (1978), na *Dunia Mti Mkavu* (1980).Madhumuni ya Kamunde yalikuwa kuwajadili wahusika mbalimbali kwa kadri wanavyobainisha 'unyonge' wao.Kauli ya Kamunde (uk.124) ni kwamba, Said Ahmed Mohammed ameeleza kinagaubaga kuhusu mifumo itumiwayo kuwadhalilisha wanyonge; mifumo hiyo ikiwa ni siasa, uchumi na masuala ya kijamii.

Kazi ya Kamunde imetufaa kwa kuwa kazi tuliyoichanganua ina wahusika ambao baadhi yao wanadhihirisha unyonge wa aina fulani.Tumeuweka 'unyonge' huu katika muktadha wa kiuchumi, kisiasa na kijamii ili kubainisha kwa nini kuna uhasama baina ya viongozi ambao pia ni matajiri na wananchi wa kawaida ambao ni wachochole.Ingawa kazi hizi ziliandikwa katika karne ya Ishirini, masuala yaliyoangaziwa na wasanii wa wakati huo bado yanaangaziwa na waandishi wa karne hii ya Ishirini na Moja akiwemo Wamitila katika *Tikitimaji* kwa kuwa mambo haya yanazidi kushuhudiwa katika jamii ya sasa ya binadamu.

Mhakiki mwingine ambaye ametufaa sana katika utafiti wetu ni Senkoro (1982).Yeye anapiga hatua ya kuelezea lugha kama kipengele muhimu zaidi katika fasihi kwani ndicho kinachotofautisha fasihi na sanaa nyinginezo. Lugha basi, ndiyo njia ambayo mwanafasihi hutumia kuyaeleza mambo yanayohusu jamii yake kwa ubunifu wa hali ya

juu na kiusanii.Ukweli wa kauli ya Senkoro unadhihirika katika *Tikitimaji* kwa sababu Wamitila ametumia lugha kwa njia za kiubunifu ili kuwasilisha ujumbe wake kama tutakavyoona katika Sura ya Tatu.

Kwa mujibu wa Mbatiah, (2001:77), tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno, ili kuleta maana mpya au msisitizo. Naye Senkoro (1982:13), anaeleza kuwa tamathali za usemi ni maneno, nahau, au sentensi ambazo hutumiwa na wanafasihi ili kutia nguvu maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama usemaji. Anasema kuwa tamathali hizi hutumiwa wakati mwingine kuwa njia ya kuipamba kazi ya kifasihi na kuongeza utamu wa lugha.

Wataalamu wote hawa wanakubaliana kwamba, tamathali za usemi ni usemi wa kufananisha kitu kimoja na kingine ili kuzua maana fiche. Hata hivyo, ufafanuzi wa Mbatiah ndio unaotufaa katika uhakiki wetu kwani msanii akitumia tamathali za usemi kwa njia mwafaka, ujumbe mzito na mkali unaweza kupokelewa na hadhira bila kuzua uhasama.Vilevile, matumizi bora ya tamathali za usemi hudhihirisha tajriba ya msanii katika mawasiliano.Msanii anaweza kutumia tamathali za usemi kuboresha mitazamo ya watu kuhusu masuala fulani yanayoihusu jamii ili kuchochea hisia na mihemko katika utekelezaji wa mambo fulani.

Tamathali za usemi zilizotumika katika *Tikitimaji* ni nyingi na tutazijadili moja baada ya nyingine katika sura ya tatu huku tukidhihirisha majukumu yake katika kutia kazi ya mwandishi mnato na mvuto na pia kuonyesha jinsi zinavyotumika kuboresha mitazamo ya wasomaji kuhusu masuala yanayohusu jamii zao.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kusoma *Tikitimaji* kwa makini ili kutambua maudhui na mbinu za kimtindo zilizotumika kufanikisha dhamira ya mwandishi.Tulitumia kamusi za kifasihi ili kutuwezesha kufafanua maana ya dhana za kifasihi ambazo tulitumia katika kazi hii.Tulichunguza kazi nyingine ambazo zilichangia kutupatia mwanga zaidi kuhusiana na mambo yanayojitokeza katika *Tikitimaji.*Hii ina maana kuwa tulikuwa tukirejelea kazi nyingine za kifasihi zilizozungumzia maswala yanayohusiana na yale yanayoangaziwa katika *Tikitimaji.*

## 1.9 Hitimisho

Katika sehemu hii tumeshughulikia vipengele mbalimbali na ambavyo ni vya kimsingi katika utafiti wowote ule.Dhana na masuala tuliyogusia katika sehemu hii ndiyo yanayojitokeza katika sura tatu zinazofuata.Tumetanguliza kazi yetu kwa kutoa maelezo mafupi kuhusu *Tikitimaji* na hasa dhamira ya mwandishi na wahusika aliowateua ili kutimiza malengo yake.Aidha tumefafanua dhana za maudhui na mtindo ambazo ndizo nguzo kuu za kazi yetu.

Tumeangazia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti kwa njia ya kitaalamu kwa kuwa maelezo mwafaka kuhusu dhana hizi ni muhimu sana katika utafiti wowote.Hii inamaanisha kwamba, maelezo kuhusu dhana hizi yasipojitokeza wazi, basi huenda mtafiti asiweze kumudu na kupata mwelekeo unaofaa katika kuendeleza kazi yake.

Aidha tumedhihirisha upeo na mipaka ya kazi yetu.Hii ni sehemu muhimu ya utafiti kwa kuwa inaonyesha shughuli za mtafiti na humsaidia kupanga kazi yake na kuokoa muda wa kutafiti.

Mwisho tumefafanua msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti tulizotumia.Kuhusu msingi wa nadharia, tumefafanua nadharia za Uhalisia na Umitindo kwa kuwa ndizo zilizotufaa katika uchanganuzi wa kazi yetu.Tumeeleza waasisi wa nadharia hizi na mihimili yake.Hatimaye, tumeonyesha mbinu zetu za utafiti.

# SURA YA PILI

# UCHANGANUZI WA MAUDHUI KATIKA *TIKITIMAJI*

## 2.0 Utangulizi

Neno 'maudhui' hutumiwa katika uhakiki wa fasihi kuelezea jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi.Neno hili hutumiwa kwa upana kuhusisha dhamira, ujumbe, msimamo na falsafa.Dhamira ni lengo kuu la mwandishi wa kazi ya kifasihi au wazo ambalo linaitawala kazi hiyo kuanzia mwanzo hadi mwisho.Msanii huyasarifu na kuyasanifu maudhui kutokana na jamii maalum.Yaleayatungayo huibuka katika jamii anamoishi na kwamba hupata msukumo au kariha ya kuandika kutokana na mambo yanayomkera au yanayomgusa katika jamii husika (Wamitila 2003:113).

Katika kazi hii, mwandishi ameangazia masuala ambayo yanaziathiri jamii nyingi na hasa zile zinazopatikana katika Ulimwengu wa Tatu. Mwandishi ameangazia jinsi wanadamu wanavyoharibu na kuchafua mazingira bila kutilia maanani athari za uharibifu na uchafuzi huu katika maisha yao. Maudhui kama haya yameshughulikiwa na wasanii wengine kama Timothy Arege katika *Mstahiki Meya* ambapo mji wa Cheneo unachafuliwa kwa kurundika takataka barabarani.Takataka hizi zinatapakaza harufu mbaya hadi makazi ya Meya.

Wamitila anapiga hatua ya kuonyesha jinsi watu wanaharibu mazingira pamoja na kuyachafua. Hali hii imekuwa ikiendelea na bado inaendelea huku viongozi wakichangia hali yenyewe kwa kutochukua hatua za kuhakikisha kwamba mazingira yanalindwa.Viongozi wawa hawa wanaopaswa kuwa katika msitari wa mbele kuona kwamba mazingira yanalindwa ndio wanaoagiza miti ikatwe kwa madai kuwa mingine

na inayokua haraka ingepandwa lakini haipandwi.Sababu ya kutopanda miti wanayotoa ni kuwa miche haimei kwa kuwa mvua haitoshi na kuwa wao hawapaswi kulaumiwa kwa ukosefu wa mvua kwani wao si Mungu.Huu ni ujuhali wa hali ya juu unaodhihirishwa na viongozi hata katika hali halisi ya maisha ya mwanadamu.

### 2.1 Uharibifu na Uchafuzi wa Mazingira na Athari Zake.

Kama tulivyoeleza katika utangulizi wa sura hii, mwandishi wa *Tikitimaji* ameangazia suala la uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa kina, kwani suala hili ndilo linaloitawala kazi yake.Mzee Jududi anaeleza yafuatayo kuhusu hali ilivyokuwa nchini Tikitimaji.

> Zamani Tikitimaji ilikuwa na miti mingi na eneo zima lilikuwa mboni ya jicho la kila mwenyeji wa eneo hilo. Mandhari yenyewe yalikuwa na mvuto wa kipekee.Miti ya kila aina iliota ikashikamana na kuvunana na kuifanya misitu ya Tikitimaji kuwa ya kutisha.Haiko hivi tena kwa kuwa watu wenyewe walifyeka miti na sasa kilichobaki Tikitimaji ni joto kali lisilokuwa la kawaida. Ilisemekana kwamba miti ilihitajika mjini ambako kulikuwa na ujenzi (uk.44).

Hii inamaanisha kwamba viongozi wenyewe ndio wanaochangia ukataji wa miti huku wakidai kuwa miti mingine, tena inayokua haraka ingepandwa lakini haipandwi.Uharibifu wa mazingira katika Tikitimaji umeendelezwa bila juhudi zozote za kulinda mazingira hadi mito inakaribia kukauka.Mto Unasi husemekana kuwa ulikuwa na maji mengi zamani lakini siku hizi ni maji kidogo sana yaliyosalia.

Sapna ambaye ni mwanachama wa shirika mojawapo la kulinda mazingira na kuhamasisha Wanatikitimaji kuhusu ulinzi na usafi wa mazingira anafanya udadisi na kugundua kuwa wanatikitimaji wenyewe ndio wanaochangia katika uharibifu huu wa

mazingira. Tunaelezwa kuwa, watu wamekata miti hata katika sehemu za mijini na hata ndege ambao walikuwa wanaimba kwa sauti zao nzuri wamehama kwa kuwa hamna miti ambayo wanaweza kujenga viota vyao. Madhara ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira ni mengi. Mito inaendelea kukauka na mvua kuendelea kukosekana ambapo umma huumia kwa kukosa chakula na malisho kwa mifugo wao. Viongozi wanaopaswa kulinda misitu na mazingira kwa jumla hawawajibiki. Mwandishi anaeleza kuwa kiongozi anapoulizwa kuhusu hali ilivyo anajibu kuwa asigeuzwe bene wa kulaumiwa kwa kila kitu na kuwa hana habari kuhusu wakata miti.Mazingira yameharibiwa kiasi cha kuwafanya nyuki wahame kutoka mizinga iliyotundikwa mitini ili kutegea asali.Hatimaye, waliotegemea asali ya nyuki kwa mapato yao hawana matumaini tena. Mwishowe wanapasua mizinga yao na kuitumia kama kuni za kuwashia moto.

Mwandishi wa kazi hii anazungumzia jinsi viongozi wanavyofyeka miti ili kujenga majumba ya kufanyia biashara.Mzee Jududi anapomwuliza Maya kama watokako vituko hivi vilikuwepo, Maya anajibu kwa kusema kuwa vilikuwepo, tena sana.Anasema:

> Huko miti inafyekwa ili kujengwe majumba makubwa.Kwingine hata mito inazibwa.Mingine inamwagwa uchafu maji yake yasitamanike kamwe (uk. 46).

Wanamazingira wanaandamana ili kupinga uharibifu wa aina hii ya mazingira lakini wanaambulia patupu.Kama tunavyoelezwa na mhusika Maya, maandamano makubwa ya amani yalifanywa mjini kupinga wajenzi waliodhamiria kujenga nyumba za kuuza kwenye vyanzo vya maji. Juhudi zilifanywa pia na vyombo vya habari ili kuweza kupinga mradi huu. Makala mengi yalichapishwa magazetini ili yachangie katika

kuupinga mradi huu lakini baada ya mradi wenyewe kusitishwa kwa muda, watu wanayasahau mambo haya lakini badaaye wanashtukia kuwa jengo kubwa ajabu lilikuwa limesimikwa mahali pale pale walipopinga lisijengwe.

Migogoro kati ya viongozi na mashirika yanayojitokeza ili kulinda mazingira imekuwa ikishuhudiwa katika jamii ambapo viongozi wa mashirika haya hudhulumiwa ili wayanyamazie maovu haya.Hali hii ndiyo inayowafanya baadhi ya wahakiki kuamini kuwa fasihi ni kioo cha jamii.Wasanii huandika kuhusu matukio yanayodhihirika katika jamii walimozaliwa hali inayowafanya wasomaji wao kuyaona katika kazi zao za sanaa.Mwandishi wa riwaya tunayoichanganua ni mzaliwa wa Kenya na matukio mengi katika riwaya yenyewe yameshuhudiwa nchini humu na ulimwenguni kwa jumla.

Waafrika humlaumu mkoloni kwa takribani kila jambo mbaya,hata kwa matatizo wanayoyasababisha wao wenyewe.Mwandishi anatumia jazanda ya jinamizi kumaanisha mkoloni.Maya anawauliza wenzake kama wanadhani kuwa jinamizi ndilo linalosababisha uharibifu na uchafuzi wa mazingira na swali lake linajibiwa na Sapna ifuatavyo:

> Hata! Haya ya maji kukauka mtoni tunayasababisha wenyewe! Vitendo vyetu vinanyonga koo mazingira yenyewe! Na ukiendelea hivi kiwiliwili cha mazingira kitasakamwa hadi kitoke ngama. Kumbukeni kisa cha kule jijini tulikotoka.Zamani kulikuwa na miti iliyolifanya jiji lipendeze.Enzi hizo hata hewa ya jijini ilivutia kwa harufu…Harufu ya kijani.Mvua ilinyesha kila wakati… kisha tukafanya nini? Miti tukaipukuta yote ili tuanze kuyapamda majengo.Mto uliokuwa na maji safi ambayo uliweza kuyaona ndani na hata kuwaona ndubwi wa chura

> wakichezacheza sasa una nini? Maji yamekuwa meusi kama bereu.Maji yaliyotiririka na kuimba nyimbo za kupendeza za maumbile sasa yanachuruzika kama lami yakiimba nyimbo za makiwa.Harufu ya kijani haipo; iliyojaa ni ya vumbi (uk 26).

Maneno haya yanadhihirisha athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwani mvua iliyonyesha sawa sawa zamani, sasa imetoweka na matokeo yake ni uhaba wa malisho kwa mifugo.Mvua inayonyesha ni kidogo hivyo haitoshi na matokeo ni maafa ya watu na pia mifugo. Maji ambayo yangenyweka zamani, sasa hayawezi kunyweka kwa sababu yamechafuliwa kwa uchafu utokao viwandani. Sapna, Maya, Kombo, na Zinji wanakutana na mfugaji anayewambia kuwa alikuwa anatafuta mahali pa kulisha mifugo wake.Anapoulizwa na Kombo kama alikokuwa anatoka hapakuwa na malisho, anamjibu kuwa hakukuwa na malisho yoyote.

Wananchi wanaochangia katika uharibifu na uchafuzi wa mazingira ndio hawa hawa wanaoathiriwa na uchafuzi na uharibifu huu.Kama tulivyosema hapo awali, fasihi inapaswa kuwazindua wanajamii ili kuweza kurekebisha hali kama hizi, na ambazo wanajisababishia wenyewe.

### 2.2 Utelekezaji wa Watoto

Kama tulivyosema hapo awali, msanii aghalabu huwa ni mzawa wa jamii anayoiandikia au anayoandika kuihusu.Kwa sababu hii, mawazo yake huwa yanamulika matukio yanayodhihirika katika jamii yake hiyo.Utelekezaji wa watoto ni jambo ambalo limekithiri katika jamii zetu.Mara nyingi ripoti zinazovuma kwenye vyombo vya habari, huhusisha matukio ya aina hii ambapo inasikika kuwa watoto wametupwa katika mapipa

au jaa la taka au wengine wameachwa tu mahali fulani kujifia.Watoto wanaobahatika na kuokolewa na wasamaria wema hunusirika na wengine kujipata katika makao ya watoto wakiwa mayatima bila wao kujua chanzo cha maisha ya aina hiyo.

Katika *Tikitimaji,* msanii ameangazia mambo haya kisanii, lakini inatudhihirikia wazi kwamba mambo haya ni yale yale yanayotukia katika maisha yetu halisi.Mwanzoni mwa riwaya, msimulizi anatuelezea jinsi yeye na wenzake watatu, yaani Sapna, Maya na Kombo walivyolelewa na kusomeshwa katika makao ya watoto ya Gwadalupe. Zinji, ambaye ndiye mhusika msimulizi wa hadithi, anaeleza kuwa, wao walilelewa na kusomeshwa na Mama Rehema, na ambaye ndiye mama wa pekee waliyemjua katika maisha yao. Katika hatua hii, msomaji anajiuliza, Je, wazazi wa watoto hawa walienda wapi? Mama Rehema aliwalea na kuwasomesha watoto wengi katika makao ya watoto ya Gwadalupe.Msimulizi anatueleza kuwa, waliporudi Gwadalupe, walezi wao wengine walifurahi sana kuwaona tena.Anasema:

> Walezi wetu wengine walichanukwa na furaha kutuona. Wakaterema kuona kuwa tulikuwa, kwa maneno yao tumepiga hatua kubwa.Watoto wa makao yenyewe walitushangilia kwa vifijo na nderemo nyingi ajabu (uk5).

Maneno haya ni ithibati kuwa, Mama Rehema aliwalea na kuwasomesha watoto wengi katika makao haya ya watoto. Tunaelezwa pia kuwa alikuwa tayari amefaidi kutokana na juhudi hizi kwani mtoto wake wa kwanza katika makao haya alikuwa amemnunulia kochi linalokaliwa nje ya ofisi yake.Msimulizi anaeleza makaribisho wanayopewa na Mama Rehema ifuatavyo:

> Alitukalisha kwenye kochi refu lililokuwa nje ya ofisi hiyo ndogo.Mama Rehema alilipenda kochi hilo kwa sababu alisema lilikuwa zawadi ya mtoto wake wa kwanza kwenye makao hayo (uk 5).

Maneno haya yanatuelekeza kutambua kuwa, makao haya ya watoto yalianzishwa mahali hapa kitambo na bado Mama Rehema anaendelea kuwapokea watoto waliotelekezwa katika jamii. Hali hii imekuwako katika jamii hii kwa muda mrefu na bado inaendelea kuwepo.Hamna suluhisho lililopatikana hasa la kuwashinikiza wazazi kuwajibika kuwatunza watoto wao. Jukumu la kuwatunza watoto waliotelekezwa limeachiwa wasamaria wema kama vile Mama Rehema kulishughulikia.Hakuna juhudi zinazofanywa na utawala wa Tikitimaji ili kuhakikisha kuwa watoto hawatelekezwi.

Sapna anajiita Binti wa jaa.Anasema kuwa aliokolewa na Mama Rehema alipokuwa ametelekezwa kwenye jaa la mjini. Hakumjua mama wala jamaa na mpaka leo hata hajui kama wapo au la. Juhudi zake zote za kuwapata jamaa zake zimeambulia patupu, ila anachojua, ambacho hata hajui Mama Rehema alilipataje, ni kuwa alitelekezwa huko labda kwa kuwa alichanganya damu ya jamii ya mamake na jamii nyingine, yaani alizaliwa nje ya ndoa, jambo lililosababisha kubaguliwa na kutengwa kwake.Hatimaye alitupwa katika jaa la mjini.

Maelezo haya ya Sapna yanadhihirisha baadhi ya sababu zinazowafanya watoto kutelekezwa na baadhi yazo ni kutowajibika kwa wazazi wao. Watoto wanaojipata mikononi mwa wazazi wa aina hii hawana budi kujipata wametupwa jaani bila wao kuwa na hatia.Wanaobahatika kuokolewa na wasamaria wema wanatunzwa na kusomeshwa

kama ilivyotokea kwa Sapna, Maya, Kombo na Zinji pamoja na watoto wengine waliopo katika makao ya watoto ya Gwadalupe.

### 2.3 Udhalimu na Unyanyasaji

Mwandishi wa *Tikitimaji* amedhihirisha udhalimu na unyanyasaji unaotawala katika jamii nyingi hasa katika Ulimwengu wa Tatu.Wanyonge wanadhulumiwa na kunyanyaswa na askari wanaopaswa kuwalinda.Katika safari yao ya kwenda Tikitimaji, Sapna, Kombo, Zinji na Maya wanakutana na kijana anayeitwa Shamsi. Kijana huyu anamtumbulia macho Kombo ambaye alikuwa afisa wa polisi na hatimaye akasema kuwa kombo alikuwa anafanana na poli, jina walilotumia kuwarejelea polisi. Anapotamka maneno haya, uso wake unaonekana kuwa na hofu kuu, na hatimaye anatimua mbio.Kijana huyu anatimua mbio kwa sababu katika Tikitimaji askari wanawanyanyasa wanyonge na matokeo yake ni kuwa wanyonge wanawaogopa sana na pia kujaribu kuwaepuka iwezekanavyo.Shamsi anaeleza:

> Huku hatuwaogopi polisi tu. Tunawaepuka kabisa.Wanatutesa. Hawatuheshimu. Wanawapendelea wenye mali. Ndio wanaomtumikia Master Stiker (uk. 64).

Kauli hii ya Shamsi inaashiria kuwa katika Tikitimaji, wanyonge waliteswa na polisi waliowatia woga mwingi. Katika mataifa mengi ya Afrika, askari wanatumiwa na viongozi kulinda maslahi yao na mara nyingi huwapiga wananchi wa kawaida bila sababu ili kuwaogofya. Hali hii hutokea hasa ikiwa viongozi ni wafisadi, wabadhirifu na wa kiimla na hasa ikiwa wananchi wanajaribu kurekebisha utawala wa aina hii.Wananchi

wanaojaribu kujikomboa hutishwa kwa kutumia vyombo vya dola hasa askari wanaowapiga na kuwaumiza.

Waandishi wengi wameangazia hali hii ya dhuluma na unyanyasaji ambapo askari wanatumiwa na viongozi kuwadhalilisha wanyonge wanaodhubutu kupigania haki zao.Kithaka wa Mberia ni mmoja wa wasanii hawa.Katika *Kifo Kisimani,* anaonyesha jinsi askari wanavyotumiwa kuwadhulumu wanaharakati wa ukombozi na pia kuwapiga wengine, hata wasiokuwa na hatia ili kuwatia woga.Mateso ya aina hii ndiyo yanayowafanya wananchi wa kawaida katika Tikitimaji kuwaogopa polisi kiasi cha kutoroka wanapowaona.Hata ingawa hali hii ya polisi kuwatesa wanyonge imekashfiwa katika maandishi mengi, bado inaendelezwa na maafisa wa usalama katika jamii nyingi barani Afrika.Hii ndio sababu inayowafanya waandishi kuendelea kuyaangazia hadi viongozi watakapoacha tabia hii ya kuwatumia askari kulinda maslahi yao badala ya kuulinda umma.

Kiongozi wa Tikitimaji anawadhulumu wananchi wa jimbo lake kwa kuwa anatawala kiimla. Anapiga marufuku baadhi ya visa vilivyokuwa vikihadithiwa nchini Tikitimaji na hasa katika mashule.Kabla ya Jitikiti kuchukua hatamu za uongozi nchini Tikitimaji, kisa cha Jitikiti kilikuwa kinasimuliwa na kilijulikana Tikitimaji kote lakini mara tu alipochukua hatamu za uongozi kisa hiki kilipigwa marufuku hata shuleni. Kisa cha Jitikiti kinasimuliwa na Mama Shamsi baada ya Sapna kuuliza asili ya neno 'Tikitimaji'.

Jina Tikitimaji linatokana na Jitikitimaji moja kubwa ambalo kisa kulihusu kinajulikana kote Tikitimaji.Mama Shamsi anasimulia kisa hiki kwa kueleza kuwa kulikuwa na tikitimaji kubwa katikati ya shamba la kijijini ambako kijana fulani alikuwa anawinga

ndege na wanyama wengine. Anapolikaribia jitikitimaji hilo na kuuliza, “Ni tikitimaji la aina gani hili?”, jitikiti hilo linarudia swali hilo, jambo linalomfanya kijana yule kutimua mbio na kuelekea nyumbani.Kijana anapowaeleza wanakijiji habari za tikitimaji linalozungumza wanaamua kwenda kuhakikisha. Wanapofika, mmoja wao anarusha kisu kinacholipasua na kunatokea jitu kubwa linalowameza wote walioenda shambani.

Hadithi hii ya jitikimaji dhalimu, inaashiria uongozi wa kidhalimu unaowadhalilisha wananchi wa kawaida kwa kuwanyang’anya mali yao hadi wanabakia wanyonge wasiokuwa na mbele wala nyuma.

Mwandishi anatueleza jinsi mzee Jududi na wengine walivyopokonywa Mlima Tirimacho na ukauziwa Durago.Viongozi wengi katika jamii tunamoishi ni wanyakuzi wa mali ya umma. Wanyonge wanafurushwa na mashamba yao kunyakuliwa kama anavyofanyiwa Mzee Jududi pamoja na wenzake waliokuwa wanaishi katika Mlima Tirimacho.Kama mtunzi asemavyo, hali hii ya kuunyanyasa na kuudhulumu umma bado imo katika jamii zetu na inapaswa kupigwa vita vikali na wanajamii.Mamake Shamsi anasema kuwa hadithi aliyoisimulia haipendwi na kiongozi wa Tikitimaji.Anasema, “kuna fununu kuwa hadithi hii haipendwi na Ami mdogo” (uk.76).Ami mdogo haipendi hadithi hii kwa sababu inasimulia kisa cha dhuluma na unyanyasaji unaotokana na viongozi kama yeye.

Baada ya wasikilizaji wa hadithi kuuliza kama hadithi ilikuwa imefika mwisho, msimulizi ambaye ni mamake Shamsi anawaambia kuwa, hiyo ndiyo hadithi wanayosimuliana kila siku na huenda kizazi cha kina Zinji ndicho kitakachoimalizia

hadithi yenyewe.Hii ina maana kuwa udhalimu bado unaendelezwa katika jamii na suluhisho lapaswa kutafutwa na vizazi vilivyopo wala si vile vya kesho.

Zinji anadhulumiwa na ami yake ambaye pia ndiye kiongozi wa Tikitimaji.Zinji anapokuwa mdogo, anaachiwa urithi na wazazi wake lakini ami yake anampokonya urithi huo kwa madai kuwa mtoto msichana hapaswi kurithi mali.Zinji anamwambia ami yake mdogo maneno yafuatayo:

> Ulininyang'anya urithi nilioachiwa na wazazi wangu.Ulinifanya nilelewe kwenye makao ingawa huko nimejua mapenzi ni nini. Ulininyima nafasi ya kukulia iliko jamaa yangu (uk.152).

Tunathibitishiwa kuwa, Ami Mdogo hakutaka Zinji arithi mali ya wazazi wake kwa kuwa alikuwa msichana.Ami mdogo anamwambia Zinji: "Mwanangu, niliamini kuwa mwanamke hawezi kurithi" (uk.152).

Maneno tuliyoyanukuu yanatuthibitishia kuwa, watoto wa kike pamoja na watu wazima katika *Tikitimaji* wanadhulumiwa na uongozi wa Jitikiti.Baada ya Zinji kufiwa na wazazi wake na Ami yake akaachiwa mali yake ili amrithishe anapokuwa mtu mzima, ami yake anamtendea unyama kwa kumtelekeza na hatimaye anamnyang'anya mali anayopaswa kurithi.

## 2.4 Ukosefu wa Kazi na Athari Zake

Suala la ukosefu wa ajira ni janga linalokera katika mataifa ya Afrika.Ni jambo ambalo hujadiliwa katika vyombo vya habari na kwingineko hususan na wasomi ambao hali hii ya nchi hizi inawakumba na kuwaathiri vibaya.Wasanii wengi wameliangazia suala hili

ili kuweza kuwahamasisha viongozi waliotwikwa jukumu la kuhakikisha kuwa wameboresha uchumi ili wanaofuzu katika masomo yao wapate kazi.Mwandishi wa *Tikitimaji* amepiga hatua kuonyesha matatizo yanayotakana na ukosefu wa kazi na athari zake katika jamii.Anaeleza matatizo wanayokumbana nayo wasichana wanapoondoka kutoka kwa wazazi wao, na kwenda kutafuta kazi.

Dadake Shamsi anayeitwa Sabiya anaondoka kwao siku moja kwenda kutafuta kazi na hajarudi nyumbani tangu alipoondoka.Shamsi anajaribu kumtafuta lakini inakuwa kazi ngumu kumpata. Tunaelezwa kwamba juhudi zote za kumtafuta Sabiya zimeambulia patupu (uk.139).Hata hivyo, Shamsi anasaidiwa na marafiki zake kumtafuta dadake kwa juhudi kubwa hadi siku moja wanampata akiwa katika harakati za kazi ya ukahaba aliyokuwa amejiingiza kwayo.Wasichana wengine aliokuwa nao vilevile, walikuwa wamefungiwa mahali fulani katika jengo ambamo hawakukubaliwa kutoka.Maelezo yafuatayo yanafafanua yaliyokuwa yakiwatendekea wasichana hawa:

> Mahali walipokuwa wakiishi wasichana hawa palikuwa na jumba kubwa lenye muundo uliofanana na majengo ya enzi ya wakoloni. Lilikuwa jengo lililojengwa zamani labda hata enzi ya utumwa. Huko ndiko walikokaa Sabiya na vijana kadha waliotolewa Tikitimaji. Hakuna aliyekuwa na uhuru wa kutoka pale (uk.142).

Kama Sabiya anavyoeleza, wasichana wengi hudanganywa kwamba wanaenda kupewa kazi kama vile za uyaya na hatima yao huwa ni kama wanayopatana nayo wasichana hawa.Wengine hudanganywa kuwa kazi nyingi na zenye malipo bora hupatikana hata Ughaibuni na wao hukubali kwenda huko bila kujua matatizo wanayoenda kukumbana nayo.Mpwawe Jarisa anayeitwa Waridi alisafirishwa kwenda Ughaibuni kufanya kazi ya

ulezi labda wa watoto au hata wazee wakongwe.Mara nyingi visa kuhusu mateso wanayopitia wanawake wanaoenda Ughaibuni kutafuta kazi hutangazwa katika vyombo vya habari.Wengine hata huuawa.

Nchini Kenya kwa mfano, vyombo vya habari huarifu umma kuhusu wasichana wanaouawa huko Uarabuni na wengine kutoroka baada ya kuteseka sana.Mambo haya ndiyo yanayozungumziwa na mwandishi katika kazi yake.

Tumeamini kuwa wasichana hawa wameteseka kwa sababu Sabiya anapokutana na nduguye analia kwa kwikwi labda kwa kukumbuka alivyoteseka mikononi mwa wanaume wakatili.Kumekuwa na watoto wengine wavulana na wasichana waliofungiwa ndani katika jumba lingine na ambao waliokolewa na Kombo kisha wakapelekwa katika makao ya watoto huko Gwadalupe.

Ukosefu wa kazi umesababisha hofu na woga kwa wale waliopata kazi kiasi kwamba hawawezi kuzungumza hadharani kuhusu maovu yanayotekelezwa na viongozi madhalimu.Wengine wanapodhubutu kuzungumza wanasema kwa sauti za chini ili wasije wakasikika.Maneno ya bawabu anayelinda lango katika shamba la maua yanatuaminisha kuwa, kuna uhaba wa kazi Tikitimaji.Sapna anapomuuliza kwa nini anawashuku wanapoingia kumwona Nia pale shambani mwa maua, anawajibu ifuatavyo:

> Msinidhanie mbaya.Ni kazi.Nisipofanya hivyo nitajimwagia unga. Na kazi hapa Tikitimaji kupata ni ngoma nakwambia (uk.104).

Kauli ya bawabu inadhihirisha kuwa Tikitimaji kulikuwa na uhaba wa kazi uliokithiri.Zinji alikuwa amepata stashahada ya uanahabari lakini bado hakuwa amepata

kazi ya kudumu ila alikuwa anaandikaandika makala na kuyatuma magazetini.Ni dhahiri kuwa, vijana wengi wanahitimu masomo ya vyuoni lakini inakuwa vigumu kupata kazi moja kwa moja.Uhaba huu wa kazi umekuwa tatizo sugu katika mataifa mengi ulimwenguni.

## 2.5 Nafasi na Umuhimu wa Vijana Katika Jamii

Vijana huwa na umuhimu wao katika jamii ingawa katika mataifa mengi ya Kiafrika, wao huitwa 'viongozi wa kesho'. Ni jambo la kusikitisha kuwaweka vijana pembeni na kuwaita viongozi wa kesho ilhali wao wana uwezo wa kuongoza na kutatua baadhi ya matatizo yanayoyakumba mataifa mengi ulimwenguni.Uwezo wa vijana unadhihirika katika *Tikitimaji* kwa kuwa wanachangia kusuluhisha baadhi ya matatizo yanayowasumbua wakaazi wa jiji la Tikitimaji.

Riwaya inapoanza tunakutana na vijana wanne ambao walilelewa katika makao ya watoto ya Gwadalupe.Vijana hawa walijipata Gwalalupe chini ya ulezi wa Mama Rehema wanayemjua kama Mama yao.Vijana hawa ni Zinji, Kombo, Sapna na Maya.Wote wanakulia mikononi mwa Mama Rehema.Mama Rehema ndiye anayewalea na kuwasomesha hadi wanapohitimu masomo yao.Zinji anakuwa mwanahabari naye Kombo anakuwa afisa wa polisi.Maya anafanya kazi maktabani na Sapna anakuwa mwanachama wa shirika la utunzaji wa mazingira.

Vijana hawa wanafunga safari kuelekea Tikitimaji.Safari hii ya Tikitimaji ni safari ya kujisaka na kujielewa kwa wanatikitimaji.Vijana hawa ni vielelezo vya jinsi jamii inapaswa kujisaka ili kuyaelewa na hatimaye kuchangia kusuluhisha matatizo yao.Katika safari yao, wanagundua matatizo mengi yanayoikumba Tikitimaji.Wanagundua kuwa

wananchi wenyewe wanachangia katika kuharibu na kuchafua mazingira. Sapna ndiye anayegundua kuwa watu wenyewe ndio wanaoharibu mazingira na kuwa hali hii inasababisha mito kukauka.

Mto Unasi umepunguza maji yake na unakaribia kukauka kabisa.Kujisaka na kugundua mambo haya ndiko kunakoweza kuwasaidia wanatikitimaji kujiondoa katika hali hii kwa kujishughulisha katika kulinda mazingira yao na kuyaweka katika hali safi.Baada ya Sapna kugundua kwamba kuna uchafuzi na uharibifu wa mazingira, anaanza harakati za kuusafisha mji wa Tikitimaji uliokuwa na uvundo mkali kutokana na taka iliyorundikana.Sapna ni mwanamazingira anayegundua kuwa umma ndio unaofanya makosa haya.Vijana hawa wanapofika Tikitimaji kuliko na rundo la takataka barabarani Sapna anauliza:

> Kumbe huku wanafanya yale yale makosa yetu? Sasa barabara nzuri kama hii itapakanaje na pande la mlima la uchafu kama hili? (uk.89).

Kama tunavyoelezwa na mhusika Zinji, Sapna alikuwa mlinzi na msafishaji wa mazingira hata huko walikotoka (Gwadalupe).Zinji anasimulia ifuatavyo:

> Nilizikumbuka juhudi za Sapna na kundi lake za kuusafisha mji wa tulikotoka.Nikakumbuka hata mara kadha ambazo tulijiunga naye kuyasafisha maeneo kadha.Mtaani tulikoishi tuliwashawishi wenzetu ambao waliacha tabia yao ya kumwaga takataka karibu na lango kuu.Hawakusema tena kuwa uzoaji takataka hizo ni kazi ya baraza la mji kama zamani.Hata jirani anayefuga mbwa ambaye alichafua kila mahali alishaanza kuuzoa uchafu wake (uk.89).

Kutokana na maelezo haya ya Zinji ambaye ni mhusika msimulizi, tunaona jukumu la vijana katika kuuboresha mji uliokuwa umechafuliwa.Baada ya vijana hawa kugundua kuwa waliochangia kuharibu na kuchafua mazingira ni wao wenyewe, hawakomei hapo bali wanashughulika kuyasafisha mazingira na pia kuwahamasisha watu wengine kuyalinda mazingira.Waliokuwa wakimwaga takataka kwenye lango kuu sasa wameiacha tabia hiyo kwa kugundua kuwa lilikuwa jukumu lao pia kudumisha usafi wa mazingira bali si jukumu la baraza la mji pekee.

**2.6 Hali Mbaya ya Mfumo wa Uchukuzi na Miundo Msingi**

Katika harakati za kujichumia mali na riziki ya kila siku, binadamu anahitaji barabara nzuri na vyombo vya kufana vya uchukuzi.Magari ya kuwasafirisha abiria kutoka sehemu moja hadi nyingine katika harakati hizi, yanafaa kuwa katika hali nzuri ili abiria wawe na hakikisho la kufika wanakoenda.Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa magari mabovu yanaondolewa barabarani na kuwa barabara zimejengwa na zilizo mbaya kukarabatiwa. Hali ilivyo Tikitimaji ni kinyume na matarajio ya wananchi.

Magari wanamosafiria abaria ni mabovu na inashangaza ni vipi magari ya aina hii yanaweza kuwa yanawahudumia wananchi.Pamoja na hali hii ya magari, abiria wanatozwa nauli ya juu zaidi kuliko ilivyo kawaida hasa wakati ambapo wasafiri huwa wengi.Matatizo ya usafiri ni mengi.Kuna nyakati ambapo hata magari ya kusafiria ni adimu sana Tikitimaji.Hii ndio maana vijana wanne wanaofunga safari ya kwenda Tikitimaji kufanya utafiti wao wa hali ya maisha, wanaamua kusafiri siku ya Jumatano ambayo ilikuwa nafuu kwao kwa kuwa siku hiyo, kama walivyofahamishwa, magari hayakuwa adimu. Vijana hawa, Sapna, Kombo, Zinji na Maya wanaabiri basi la kuelekea Tikitimaji katika kituo kikuu cha mabasi.Jambo la kwanza wanaloligundua ni kuwa, basi

lenywe walilokusudia kusafiria lilikuwa kuukuu ajabu.Kama aelezavyo msimulizi, hali ya uchukuzi na usafiri kwa jumla ilikuwa mbaya Tikitimaji.Msimulizi anaeleza:

> Tulipanda basi kuelekea Tikitimaji katika kituo kikuu cha mabasi jijini.Basi lenyewe lilikuwa kuukuu ajabu. Hata ilikuwa vigumu kuamini kuwa liliruhusiwa kufika jijini seuze kubeba abiria. Rangi ya nje ilikuwa imepauka hapa na pale na kuacha mabakamabaka. Viti vyake vilikuwa vimekwanyuka hapa na pale.Karia za ndani zilifanana na matenga wazi ya kubebea nyanya.Ilikuwa vigumu kuamini kuwa basi kama hili lilikuwa likifanya kazi (uk.16).

Maelezo haya ya msimulizi yanathibitisha kuwa hali ya usafiri ilikera lakini bado wananchi walijipata wanaabiri mabasi ya aina hii.Mabasi yaya haya yalitumika kuwasafirisha watalii kuelekea katika vivutio mbalimbali vya kitalii huko Tikitimaji.Basi walimosafiria vijana hawa pamoja na watalii lilipewa jina la lakabu *Maafu Express*.Jina hili la kimajazi linaoana barabara na hali ya basi hilo.Ni kama liliwabeba watu kuwaelekeza mautini.

Kwa ufupi, mwandishi anaangazia hali ya usafiri wa watu na uchukuzi wa bidhaa katika jamii zetu.Wananchi wanajipata katika hali ya hatari ya kuabiri magari mabovu ambayo huenda yakasababisha ajali zinazochangia katika vifo vya watu wengi.Mwandishi anasisitiza hali hii anaposema kuwa, baada ya vijana hawa kushuka kutoka basini, walingia katika matwana nyingine iliyokuwa kuukuu ili kuendelea na safari yao.

Ujumbe wa mwandishi unakusudiwa kuwafikia viongozi ambao wanapaswa kuwajibika ili kurekebisha hali ya uchukuzi inayotishia kuangamiza wananchi wanaoshughulika ili

kuinua uchumi wa nchi.Hali ya mfumo wa uchukuzi wa aina hii unadhihirika katika hali halisi ya maisha na unachangia pakubwa katika ajali za barabarani.

Wananchi pia wana mchango wao katika hali hii kwani hawasusii kuabiri magari mabovu ili kusaidia kurekebisha makosa haya.Wananchi wanapaswa kuzinduka na kuchangia katika harakati za kuboresha hali hii mbaya ya mfumo wa uchukuzi.Wanapaswa kususia kuabiri magari mabovu na kuchangamkia magari ambayo yametunzwa vizuri ili kuhakikisha kuwa maisha yao hayamo hatarini.Hata hivyo, wakati mwingine raia hawana namna nyingine ila kuabiri magari hayo mabovu kwa kuwa magari mengi ya uchukuzi wa umma yamo katika hali ya kusikitisha.

## 2.7 Nafasi na Hadhi ya Mwanamke Katika Jamii

Kwa muda mrefu wanawake wamedhaniwa kuwa viumbe duni katika jamii nyingi ulimwenguni na hasa katika Ulimwengu wa Tatu.Waandishi wengi wameandika kuthibitisha hali hii.Said Ahmed Mohamed, kwa mfano, ameonyesha hali ya kudunishwa kwa mwanamke katika jamii katika *Utengano*.Katika riwaya hii, wanawake wanatawishwa na kunyimwa uhuru wa kutoka nje bila idhini ya waume zao.Wanawake pia wanatumiwa kukidhi ashiki za wanaume na wengine kuachiwa jukumu la kuwalea watoto huku waume zao wakistarehe vilabuni na kukimbizana na makahaba.

Ingawa waandishi wengi wamejitokeza kuangazia hali hii na kujaribu kumzindua mwanamke kupigania haki zake, bado mwanamke anaendelea kudhulumiwa hata katika karne hii ya Ishirini na Moja.Wamitila anaendelea kumulika hali ya wanawake ilivyo katika jamii,kwa kushughulikia hali yao katika *Tikitimaji*.

Ingawa wanaufeministi wengi, wanaume kwa wanawake wameangazia hali ya wanawake na kujaribu kuwazindua wapiganie haki yao, bado baadhi ya wanamke wanaendelea kujipata wakitumiwa vibaya na baadhi ya wanaume.Katika *Tikitimaji,* mwandishi ameisawiri hali ambapo wasichana wanaondoka kwao kwenda kutafuta kazi na hatimaye wanajipata katika danguro wakitimiza matakwa ya wanaume.

Sabiya ni mhusika anayejipata katika hali hii.Yeye na wasichana kadha wamejipata wamefungiwa katika nyumba fulani ambapo wanazizima kiu za wanaume na hapa hawana uhuru wa kutoka.Wanashinda katika nyumba mchana kutwa na kukubaliwa kutoka wakati wa usiku pekee.Hii ndio maana inakuwa vigumu kuwapata wasichana hawa hata wanapotafutwa na jamaa zao.Sabiya na Waridi wametafutwa kwa muda mrefu kabla ya kupatikana.

Hata hivyo, juhudi nyingi za kuwaokoa wasichana kama hawa zimefanywa na mashirika mengi ya kutetea haki za mtoto wa kike na mwanamke kwa jumla. Mama Rehema ni mhusika anayewakilisha watetezi wa haki za watoto na katika makao yaliyoanzishwa na Balozi wa Meksiko Gwadalupe, watoto wanaodhulumiwa wanatunzwa na kusomeshwa. Watoto wanaotelekezwa na wazazi wao au mayatima wanaokolewa na Mama Rehema na kupelekwa katika makao ya Gwadalupe. Shamsi anapompata dadake aliyepotelea mjini na kutumiwa kama kahaba na wanaume, anampeleka Gwadalupe pamoja na watoto wengine waliojipata katika hali hii.

Kwa hivyo, mwandishi amemsawiri mwanamke kama mtu mwenye huruma na anayejihusisha na ukombozi wa watoto waliotelekezwa.Katika makao ya Gwadalupe Mama Rehema amewalea na kuwasomesha watoto wengi wa kike na wa kiume.Mama

huyu amechangia pakubwa kuwainua watoto waliotelekezwa na kuwafanya kuwa watu wa kuheshimika katika jamii na kuchangia maendeleo ya nchi ya Tikitimaji. Baadhi ya watoto aliowalea na kuwasomesha wamehitimu masomo yao na sasa wanachangia katika utatuzi wa baadhi ya matatizo yanayoikumba Tikitimaji.

Sapna (mwanamazingira), Kombo (polisi), Zinji (mwanahabari) na Maya (mkutubu) ni vijana waliolelewa na kusomeshwa na Mama Rehema na kila mmoja wao anachangia katika kugundua matatizo yanayoikumba Tikitimaji na kushughulika katika utatuzi wake.Sapna, Zinji na Maya ni vijana wanawake na wanaoshughulika ili kutafiti na kujua matatizo ya Tikitimaji.Kupitia uongozi wa Sapna, vijana hawa wanasafisha mazingira na kuwahamasisha wananchi kulinda na kuyachunga mazingira.Wanaondoa mlima wa takataka barabarani na kuuongoza umma kuandamana ili kupinga ukataji wa miti ili majengo yapandwe mahali pa miti.

Mzee Jududi anapowauliza vijana hawa kama hawalalamiki wakati miti inakatwa huko kwao anajibiwa kuwa wanalalamika sana na kuwa Sapna ambaye ni mwanamangira ameongoza maandamano mara nyingi kuupinga uharibifu na uchafuzi wa mazingira.Naye Zinji amechangia kupambana na waharibifu wa mazingira kwa kuchangia mada kuhusu uharibifu huu magazetini (uk46).Mzee Juhudi anawahimiza waendelee kupigana kwani penye mawimbi na milango i papo.

Mchango wa wanawake katika *Tikitimaji* ni mkubwa kwani kina mama na vijana wa kike wamejibidiisha kuona kwamba, baadhi ya matatizo yanayoikumba Tikitimaji yamesuluhishwa. Kina mama ni walezi bora ni wenye huruma na ni wasafishaji na wahifadhi wa mazingira.Ukarimu wa kina mama pia umedhihirika kupitia mamake

Shamsi ambaye anawakaribisha Sapna, Maya, Kombo na Zinji na kuwakirimia kwa kuwapa malazi na chakula wanapokuwa katika safari ya kuelekea Tikitimaji.Wanawake kwa hivyo, wamepewa jukumu kubwa na mwandishi kwani wao wamechangia pakubwa katika elimu na malezi ya watoto wanaotelekezwa katika jamii na pia katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Watoto waliotelekezwa ni tatizo sugu katika mataifa ya Ulimwengu wa Tatu kwa sababu katika miji mingi, watoto hawa wanashinda wakirandaranda huku tawala nyingi zikiwapuuzilia mbali. Msanii anawahimiza watu binafsi au mashirika mbalimbali kujitolea kama alivyojitolea Mama Rehema, ili kusaidia kusulubisha tatizo hili.

## 2.8 Ushirikiano wa Vijana na Wazee Katika Ujenzi wa Jamii Mpya

Katika jamii ambamo mna changamoto nyingi za kisiasa, kiuchumi na kijamii, makundi mbalimbali hujitokeza kupambana nazo.Mara nyingi jamii hukumbwa na matatizo yanayoibukia uongozini na kusambaa hadi kuwafikia wananchi wa kawaida ambao ndio huathirika zaidi kutokana na matatizo haya. Ikiwa viongozi waliotwikwa jukumu la kuwaelekeza na kuwalinda wananchi wa kawaida watapuuza majukumu yao, basi wananchi wa kawaida ndio wanaoumia. Mambo yakitokea kuwa namna hii, inabidi baadhi ya wananchi kujitolea kurekebisha mambo yanayoenda mrama.

Katika *Tikitimaji*, mwandishi anaonyesha jinsi wanatikitimaji wanavyojitolea kushirikiana ili kujikosoa wao wenyewe na pia kuwahamasisha wenzao ili hali yao ya maisha iweze kutengenea.Vijana na wazee kwa pamoja wanatia juhudi za kurejesha mazingira yaliyoharibiwa katika hali yake ya awali. Mzee Jududi ameshuhudia

Tikitimaji iliyojivunia rangi ya kijani na mito iliyokuwa na maji mengi na safi kabla ya miti kuvamiwa na kufyekwa na kabla ya uchafu kuanza kumwagwa mitoni.

Mzee Jududi pia ameshuhudia yeye na wanatikitimaji wengine wakifurushwa kutoka Mlima Tirimacho, mahali walikoishi kwa miaka na dahari huku wakiuchunga mlima na kuhakikisha kwamba, mlima ulihifadhiwa.Akisimulia kisa hiki kwa Zinji, Sapna, Maya na Kombo anasema kuwa, tangu jadi na asili jamii yao iliishi kwenye msitu wa Mlima Tirimacho.Ulikuwa msitu maarufu na uliokuwa na miti adimu sana.Mingine hata haipatikani sehemu yoyote nyingine nchini.Huko ndiko walikoishi kwa miaka mingi.Maisha yao yalitegemea urinaji na kuhemera. Msitu huo ndio uliokuwa kila kitu chao na walijua jinsi ya kuulinda msitu wenyewe.Wamefanya hivi kwa dahari na dahari kwa sababu wanaelewa kuwa mlima ndio chanzo cha maisha yao. Anaeleza kuwa, kwa miaka mingi huo ndio msitu mkubwa uliobakia katika eneo zima la kwao. Anasema: "Hata huo mto mliovuka ambao siku hizi hauna maji, chanzo chake ni Tirimacho" (uk.37).

Mzee Jududi anawafahamisha vijana hawa kuwa, Mlima Tirimacho uliokuwa chanzo cha maisha ya Wanatikitimaji uliuzwa na kiongozi wa Tikitimaji.Anasema kuwa tamaa na ubinafsi imesababisha madhara mengi kwa wanatikitimaji.Yeye na jamaa yake wote walibumburushwa kutoka Tirimacho.Hata hivyo, Jududi na wengine walimkosoa Jitikiti na hatimaye Mzee Jududi akafurushwa na Jitikiti kutoka eneo hilo.Mzee Jududi anawasimulia vijana hawa kuhusu masaibu yaliyompata yeye na wanaharakati wengine na kuwahimiza vijana nao wasiogope bali waendeleze juhudi za ukombozi wa nchi yao.

Mamake Shamsi anashirikiana na vijana katika ujenzi wa Tikitimaji mpya anapowakaribisha Zinji, Sapna, Maya na Kombo kwake wanapokuwa katika safari ya kujijua na kujua matatizo yanayoikumba nchi yao.Vijana hawa wanapofika kwa mamake Shamsi anawakaribisha kwake na kuwasimulia hadithi inayowafahamisha kuhusu udhalimu wa kiongozi wa Tikitimaji. Anawasimulia hadithi ambapo Jitikiti kubwa linageuka na kuwa jitu kubwa linalowameza wanakijiji wote nchini Tikitimaji.

Jitikiti kuwameza wanakijiji wote ni jazanda ya jinsi wanatikitimaji wanavyodhulumiwa kwa kufurushwa msituni walimoishi maisha yao yote na vile vile jinsi wanaharakati wa ukombozi wanavyofurushwa kutoka sehemu walimoishi na kutorokea kwingineko kama anavyofanyiwa mzee Jududi na mzee Dhamiri.Mama Shamsi anapomaliza usimulizi wake anawaeleza kuwa hadithi hii haikuisha, yaani dhuluma bado imo na itawabidi vijana hawa kuiendeleza hadithi yenyewe na kuifikisha mwisho.

Mzee Dhamiri ni mwanaharakati wa vita dhidi ya udhalimu.Jitikiti hataki akae karibu naye kwa sababu hii.Maya anapomuuliza mzee Dhamiri kwa nini anakaa mbali aliko, mzee Dhamiri anamjibu kwa maneno yafuatayo:

> Jitikiti hakutaka mzee Dhamiri karibu naye.Alihofu kuwa nitayafichua matendo yake au nitayaweka wazi aliyotaka kuyafunika kwa kuwasahaulisha watu jana yao.Niliamua kuja kukaa huku.kwa njia hii nitaweza kuwaonya wanaopita hapa! Lakini wengi hawanitaki ushauri.Wananipuuza na kwenda zao! Wananidharau kwa kuona sioni kama wao bila kujua naona kuliko wanavyoweza kuona na macho yao.Laiti wangejua kosa wanalolifanya! Ni kama mtu anayeshika mwangaza

kwenye sehemu ya nyuma wakati wa usiku na kuanza kutembea.Kivuli chake ndicho kinachotangulia! (uk.97).

Maneno haya ya mzee Dhamiri yanawasaidia vijana hawa kuelewa alivyokuwa kiongozi Jitikiti na vilevile kuelewa kuwa baadhi ya wanatikitimaji hawashughuliki kupigania haki zao ila wanayapuuza maneno ya hekima ya wazee kama vile ya Mzee Dhamiri.Mzee Dhamiri anawafahamisha vijana hawa kuwa, Jitikiti ni kiongozi anayependa kuiga mambo kama kasuku.Pamoja na kuiga huku, Jitikiti pia anachukia yeyote anayeikosoa tamaa yake kubwa (uk 97).Mzee Dhamiri anaeleza kuwa, Jitikiti alikuwa kiongozi aliyekuwa na umero hasa.Kwa sababu ya umero huu, wazee kama vile Jududi na Dhamiri walijaribu kumpiga vita lakini wakafurushwa na kuhamia kwingineko.Hata hivyo, Juhudi zao hazijadidimia kwa sababu hata pale walipo, wanawatia ari vijana ili kuendeleza Juhudi zao za ukombozi.

Vijana hawa wanapokutana na Nia ambaye ni mpwaye Mzee Dhamiri anawajulisha kuwa mwalimu Insafu alipoteza kazi yake baada ya somo la historia kupigwa marufuku.Somo hili huenda lilipigwa marufuku kwa sababu ya kuwakumbusha Wanatikitimaji madhila yaliyowapata wakati uliopita kutokana na viongozi wao.Mwalimu Insafu ndiye anayemweleza Nia kuwa sehemu kubwa ya Tikitimaji palijaa maji lakini siku hizi vianzo vya maji upande wa juu kama huko Tirimacho vimeharibiwa (uk.112). Jitikiti pia alitumia askari kuwadhulumu wanaharakati wa ukombozi kama vile mwalimu Insafu ambaye pia alitoroka ili kuokoa maisha yake.

Hata hivyo mapoli kama wanavyoitwa askari walikuwa wamemfuata hadi alikotorokea.Polisi wanawakuta Zinji, Sapna, Kombo, Maya, Nia na mwalimu Insafu wakizungumza kisha wanawambia: “tumewafuata tangu mbali!” (uk.116). Naye

mwalimu Insafu anawaambia: “maisha yenu mtaendelea kufuata msipofanya juhudi ya kuwaongoza wafuatao!” (uk.11).Mmoja wa askari hao anasogea mbele na kuongea akimwashiria mwalimu Insafu na kusema, “msikilize huyu! Atawapotosha kama alivyowapotosha vijana wengi!”

Polisi wa Tikitimaji wanatumiwa kulinda maslahi ya viongozi wao wala si kuwalinda wanatikimaji. Wanaojaribu kuikosoa hali mbaya wanafurushwa na wanaojaribu kuwashauri vijana kuhusu maisha ya Tikitimaji wanaitwa wapotoshaji. Uongozi wa Tikitimaji kwa hivyo ni wa kukandamiza na kuwadhalilisha wanaojaribu kuikosoa serikali.Wengi wao wanafukuzwa kwao na wengine kuachishwa kazi kama anavyofanyiwa mwalimu Insafu.Hata hivyo Wanatikitimaji hawafi moyo ila wanaendelea na Juhudi za kuhakikisha kuwa matatizo yanayowakumba yanatatuliwa.

Sapna anaomba apewe idhini ya kuanzisha vuguvugu la kuyatunza mazingira ya Tikitimaji.Yeye kama mwanamazingira anaongoza uzoaji wa taka iliyorundikana kando ya barabara.Naye Kombo, anafanya juhudi za kuwa askari mwema ili wanatikitimaji wasiendelee kuwa na hofu kila wanapowaona askari.

Kwa ufupi, wazee na vijana wa Tikitimaji wanashirikiana kurejesha Tikitimaji mahali pake pa zamani, wakati mazingira yalikuwa imara na wakati ambapo kiongozi alikuwa na uhusiano mwema na watu aliowaongoza..

Mzee Jududi, Mama Rehema, mamake Shamsi, Mwalimu Insafu na mzee Dhamiri wametoa ushauri kwa vijana wanaodhamiria kufanya utafiti Tikitimaji ili wajue matatizo na chanzo cha matatizo yenyewe, ili kuchangia katika utatuzi wake.Vijana kama vile Sapna, Zinji, Kombo, Maya, Shamsi na wengineo wameusikiliza ushauri wa wazee na

kuitikia mwito wao wa kuendeleza na kumalizia vita dhidi ya udhalimu, uharibifu na uchafunzi wa mazingira, ubadhirifu wa pesa za umma katika sherehe nyingi zikiwemo za kuzaliwa kwa kiongozi, kukiukwa kwa haki za watoto na kufurushwa kwa wanaharakati wa ukombozi.

## 2.9 Kutowajibika, Uzembe na Ujuhali wa Viongozi

Viongozi wanatarajiwa wawe mfano bora wa kuigwa na wananchi lakini mara nyingi, mambo huwa kinyume na matarajio ya raia. Umma huwa na matarajio kuwa viongozi wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali katika nchi yoyote ile, huwa na wajibu wa kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili kuboresha maisha ya raia wa nchi zinazohusika.Mambo yanapoendelezwa kinyume na matarajio ya raia wapenda maendeleo, mara nyingi baadhi ya raia hujitokeza na kutaka kurekebisha hali isiyowaridhisha.

Hali hii ndiyo inayotokea Tikitimaji wakati viongozi wanashindwa kuwajibika.Viongozi waliopewa jukumu la kushughulikia usafi wa mazingira na kuhakikisha kuwa hakuna uchafuzi na uharibifu wake, hawafanyi kazi yao.Kutowajibika kwao kunasababisha kuwako kwa milima mikubwa ya takataka kando ya barabara na nyingine inatupwa hata karibu na makaazi ya watu.Wananchi kama vile Sapna wanajitolea pamoja na vijana wengine ili kuchangia katika kuyasafisha mazingira na pia kuwahamasisha wananchi wengine ili waweze kuona faida ya kuchangia katika kusafisha mazingira.

Sapna anaomba idhini ya kuanzisha vuguvugu la kuyalinda mazingira kutoka kwa wanaohusika na masuala ya mazingira ili kutimiza lengo lake la kuona kuwa mazingira yamehifadhiwa.Sapna anapopewa idhini ya kuanzisha vuguvugu hili la kulinda mazingira, anaenda hadi ofisi kuu ya Tikitimaji na kumkuta ofisa aliyeshiba siha

iliyomvimbisha mashavu.Ofisa mwenyewe anasinziasinzia huku akifunga macho na kuyafungua nusunusu.Hali hii ya maofisa kujikalia tu maofisini bila kujua kinachoendelea nje ya ofisi hizi, ndicho chanzo cha mambo kuharibika bila wao kufahamu, nchini Tikitimaji.

Sapna anapotaja neno vuguvugu tu, yule ofisa anadhani kuwa vuguvugu hilo ni la kisiasa na anaelekea kulipinga vikali kabla ya kuelezwa kuwa ni vuguvugu la kulinda mazingira. Ujuhali wa kiongozi huyu unadhihirika wazi kwa kuwa yeye anaelewa kwamba vuguvugu huwa la kisiasa tu.Anapoelezwa kuwa nia hasa ya vuguvugu hilo ni kuhakikisha kuwa mazingira ya Tikitimaji ni safi, anasema kuwa Tikitimaji ni kielelezo cha utunzaji wa mazingira.Maneno haya yanamshangaza Sapna kwa kuwa alikuwa amejionea kwa macho yake jinsi mazingira yalivyokuwa yameharibiwa na kusababisha mito ya Tikitimaji kutishia kukauka.Afisa huyo anaongezea kuwa mazingira ya Tikitimaji ni mazuri.Maneno ya ofisa huyu yanazidi kumshangaza Sapna ambaye anawaza yafuatayo:

> Labda huyu hata hana habari ya kilio cha jamii ya maskini mzee yule.Ikiwa mambo yanayotokea hapa alipo hayajui sembuse ya mbali? (uk 124).

Yule afisa anaendelea kumweleza Sapna jinsi mimea na miti ya kila aina ilivyopandwa Tikitimaji. Lakini Sapna anamweleza kuwa mahali kwingi hakupendezi kisha akataja lile jalala lililokuwa kando ya barabara.Ofisa huyo anamjibu kuwa alikuwa na miaka mingi bila kufika huko, na ikiwa pana uchafu basi litakuwa tatizo la wazembe waishio eneo hilo.Eneo lenyewe analolizungumzia ndilo lango kuu la kuingilia Tikitimaji.Ikiwa

wageni na hasa wawekezaji wangefika Tikitimaji na kukuta rundo hili la takataka, huenda wangesusia kuwekeza huko.

Katika hali halisi ya maisha, kuna viongozi wasiowajibika katika kazi yao na huwa hawajui mambo yanapoharibika katika zile zile nyadhifa wanazozishikilia.Viongozi kama hawa wasipofuatiliwa husababisha hasara kubwa kwa nchi huku wakiendelea kulaza damu tu katika maofisi ya umma.Kutowajibika na ujuhali wa viongozi unadhihirika ambapo hata wakubwa wa ofisa huyu hawana habari kwamba hafanyi kazi yake inavyopasa.Hata Sapna anapomweleza ofisa huyu wa mazingira kuhusu hali mbaya ya mazingira, anaipuuza kauli hii ya Sapna kwa kusema kuwa mazingira yapo kwa ajili ya binadamu na si mwanadamu awepo kwa ajili ya mazingira.Kauli hii ya ofisa wa usafi inathibitisha jinsi baadhi ya maafisa walivyo na ujuhali mwingi kuhusiana na mazingira yanayowahifadhi wao pamoja na wanajamii wengine ulimwenguni.

Wakubwa wake ofisa huyu wa usafi pia hawawajibiki.Kiongozi wa jimbo la Tikitimaji ambaye amepewa majina mengi ya lakabu kwa sababu ya udhalimu wake, pia hawajibiki. Jitikiti kama anavyoitwa na wanatikitimaji anapoulizwa kuhusu watu wanaoharibu misitu anasema kuwa yeye hajui habari ya wakatao miti na kuwa watu wasimlaumu hata kwa makosa yao wenyewe.Maneno haya ya Jitikiti yanadhihirisha jinsi viongozi wanavyoyafungia macho maovu yanayoendelezwa katika majimbo yao huku mazingira yakizidi kuharibika na kutishia kuangamiza jamii nzima.Viongozi hawa hawa wanakata miti na kuahidi kupanda mingine. Wanapoulizwa kwa nini miti mingine haipandwi wanasema kuwa mvua haitoshi na hivyo wao hawapaswi kulaumiwa kwani sio wao wanohusika na mvua.Hiki ni kinaya kwa sababu ukataji miti ndiko kumechangia kupotea kwa mvua.Viongozi hawa hawaelekei kuelewa kuwa matendo yao ndiyo

yanayosababisha hali kuwa kama ilivyo kwa sababu hawawajibiki, kama viongozi wanavyopaswa kuwajibika.

Maneno ya ofisa wa usafi yanashangaza anapowauliza kina Sapna kama hawakujua ni nini kilichoyaongoza maisha ya Tikitimaji.Anasema kuwa kilicho muhimu hakikuwa mazingira bali ni kinachotokana na mazingira yenyewe.Anaeleza:

> Haijalishi hata kama mtu atayatia mazingira yenyewe kwenye kamuzi na kuyakamua kiowevu kumfaidi.Watu wamo mbioni kutafuta hela; hakuna anayeshughulika na asili au mazingira hayo ayasemayo.Haijalishi kama mtu atayaua mazingira yenyewe au la.Ukiweza hata kuufukua utumbo wa mazingira ndiyo bora kabisa.Hawajui kuwa hata siku hizi milima inabomolewa ili kuufichua utajiri mkubwa uliofichwa ndani? Hawajui mifupa ya ardhi inatobolewa utolewe utajiri kwenye uboho wake? Ikiwa wewe huna la kufanya isipokuwa kuwaza kama mlima wa takataka shauri yako! ( uk.127).

Haya ndiyo maneno ya viongozi.Sapna anapomuuliza ofisa wa usafi kama yeye na wenzake wangeruhusiwa kuzoa takataka zilizojaa kando ya barabara, afisa anamjibu ifuatavyo:

> Sawa! Ukiona unaweza, shauri yako! Ila msije kusema kuwa mnakerwa na harufu! Isitoshe, usiulize malipo yoyote kwenye ofisi hii.Hela zilizopo ni za kumalizia miradi mingine muhimu sio za kuwaza kama milima!wewe na hiyo mikono mirembo hivyo.Huoni usumbufu kuizika mikono teketeke kama hiyo kwenye majalala? (uk.128).

Maneno haya ya ofisa wa usafi yanadhihirisha hali ya kutowajibika kwa viongozi wanaohusika katika utunzaji wa mazingira.Kutowajibika na ujuhali huu ndio unaosababisha mazingira kuharibiwa na kuchafuliwa kama inavyoshuhudiwa nchini Tikitimaji.

Utunzaji wa mazingira unapuuzwa na miradi mingine inapewa kipaumbele.Watu wanaendelea kuyatia kitanzi mazingira bila kufahamu kuwa wanajitia kitanzi pia.Vianzo vya maji vikiharibiwa kama ilivyofanyika Tikitimaji, mito huathirika na mvua kuwa haba.Uhaba huu wa mvua unasababisha uhaba wa chakula kwa binadamu na pia uhaba wa malisho kwa mifugo, jambo linalochangia kudidimisha uchumi wa nchi.Hali hii haiwaathiri tu wale wanaoharibu mazingira bali wanajamii wote kwa jumla.

Sapna na wenzake wanapokubaliwa kuanzisha vuguvugu la utunzaji wa mazingira wanaloliita WAZALIMA wanaanza kufumua mlima wa takataka uliokuwa kando ya barabara.Ndugu Kikwiro, yaani yule ofisa wa usafi, anapendekeza uchafu huo ukatupwe mtoni jambo analolipinga vikali Sapna.Ni jambo la kuvunja moyo kwa raia wa nchi yoyote ile, kuona viongozi wanaopaswa kuwa katika msitari wa mbele katika uhifadhi na usafi wa mazingira, wakiwa ndio wanopendekeza uchafu kumwagwa mitoni bila kuwajali wenzao wanaotumia maji yale wala mifugo wanaokunywa maji hayo.Kutowajibika na ujuhali wa viongozi kama hawa ni kero kubwa kwa wananchi wanaojitolea kurekebisha hali ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira, kama wanavyofanya kina mzee Jududi na vuguvugu la utunzaji wa mazingira linaloongozwa na Sapna.

## 2.10 Umaskini na Athari Zake

Umaskini ni hali ya uhitaji wa mwanadamu hasa anapokosa mahitaji ya kimsingi kama vile mavazi, chakula na makazi.Kwa karne nyingi binadamu amejipata katika matabaka tofauti tofauti yakiwemo yale ya kitajiri na kimaskini hali inayoendelea kudhihirika katika mataifa mengi Ulimwenguni.Wasanii wengi wameandika kuhusu suala hili wakionyesha chanzo cha matabaka haya na kuwazindua maskini wanaodhulumiwa kupigania haki zao ili kuweza kujikomboa.Mfano wa wasanii hawa ni Timothy Arege aliyeandika tamthilia inayoitwa *Mstahiki Meya* anamoelezea jinsi viongozi wanaochaguliwa na umma wanajilimbikizia mali kupitia njia za kifasidi huku raia waliowachagua wakila makombo yaliyosazwa na viongozi hawa.Wafanyakazi wanaozalisha mali wanalipwa mishahara duni, mara nyingine wanalipwa nusu nusu na hata wakati mwingine mishahara yao inachelewa.Hali hii inaendelea kuwadidimiza katika umaskini huku viongozi wao wakiendelea kustawi.

Katika *Tikitimaji*, viongozi wana tamaa na ubinafsi, hali ambazo mzee Jududi anazozirejelea kama umero hasa.Jitikiti ambaye ni kiongozi wa jimbo la Tikitimaji anawafurusha raia walioishi katika msitu wa mlima Tirimacho na kuuza mlima wenyewe kwa Durago.Kufurushwa kwa wakaazi wa Tirimacho kunawasababishia umaskini unaompelekea mzee Jududi kuvaa ngozi ya mnyama badala ya nguo.Zinji akiyakumbuka masaibu ya Mzee Jududi na wengine anamwambia Ami Mdogo, "umewanyang'anya watu ardhi yao umwuuzie Durago!" (uk.152). Kauli hii inatuelekeza kufahamu kwamba, raia walipokonywa ardhi yao ikauziwa wawekezaji kama vile Texas Euro Drillers Ltd (uk.138).

Hii ni kampuni inayochimba mafuta na gesi Tikitimaji. Uwekezaji kama huu hauwafai kwa njia yoyote vijana wengi nchini Tikitimaji kwa kuwa wengi wao huchakurachakura katika jalala ili waweze kupata riziki ya kujiendeshea maisha.Mzee Jarisa ni mmoja wa watu wanaotafuta riziki yao katika jalala la Kumbo.Jarisa ni mzee wa miaka isiyopungua sitini na anayechakura katika jaa hili pamoja na vijana wa Tikitimaji.Mbwa na ndege pia wanatafuta riziki yao katika jaa hili.Maelezo kuhusu mzee Jarisa yanadhihirisha hali ya umaskini inavyowakumba baadhi ya wanatikitimaji.Tunaelezwa ifuatavyo:

> Jarisa alikuwa mzee wa miaka isiyopungua sitini aliyevalia nguo zilizochakaa ajabu.Mararu yake yalichakaa na kutwaa rangi nyeusi iliyomfanya atishe kwa sura (uk.132).

Maelezo haya kumhusu mzee Jarisa yanatuchorea taswira ya mijini barani Afrika na kwingineko ulimwenguni ambapo watu, wanyama na ndege hujumuika kutafuta riziki za kuyaendeshea maisha yao katika majalala ya takataka.Katika Tikitimaji, hali hii imeendelea kwa muda mrefu bila uongozi kuitafutia suluhisho.Mzee Jarisa amekulia katika jaa hili la taka na hajapata msaada ili aweze kukidhi mahitaji yake kwa njia yenye heshima kuliko hii.Vijana wanaochakura pamoja na Jarisa katika jaa lile la Kumbo wanasema kuwa Jarisa aliwatangulia pale kwa siku nyingi na analifahamu fika jaa lenyewe.Hii ina maana kuwa Jarisa amekuwa akitafuta riziki yake katika jaa hili kwa miaka mingi.Kutafuta riziki katika jaa la takataka si ishara ya umaskini tu bali ni ishara inayodokeza kuwa kuna uchafuzi wa mazingira uliokithiri.

Ingawa umaskini umeneea sana Tikitimaji, kuna watu ambao ni wakarimu na wanaoamini kuwa kutoa ni moyo usambe ni utajiri.Mzee Jududi anapoagana na Zinji, Sapna, Kombo na Maya katika safari yao ya Tikitimaji, anawashauri kuwa wakiona usiku

unaingia kabla ya kufika mwisho wa safari yao, wasione ugumu kutafuta msaada. Anawaambia: "licha ya kuwa watu ni mafukara wa ulimwengu, lakini ni wakarimu sana." (uk.56).Maneno haya ya mzee Jududi ni ithibati tosha kuwa, kweli wanatikitimaji walipambana na hali ya umaskini.

Umaskini uliowakumba wanatikitimaji ndio unaowafanya vijana kuondoka huko na kwenda kutafuta kazi na hatimaye kujipata wameingilia kazi ya ukahaba.Watoto wengi pia wamejipata katika makao ya watoto.Baadhi ya watoto wamejipata huko baada ya kufiwa na wazazi wao na hatimaye kudhulumiwa na jamaa zao ambao waliachiwa mali ili kuwatunza watoto hawa.Zinji ni mfano wa mtoto aliyefiwa na wazazi wake na kujipata mikononi mwa ami yake aliyempokonya mali aliyoachiwa na wazazi wake.Hatimaye, Zinji alijipata katika makao ya watoto ya Gwadalupe.

Vijana wengi wanaoenda kutafuta kazi ili kukidhi mahitaji yao wanajipata wamenaswa katika mitego ya ukahaba na wengine kusafirishwa ughaibuni wanakoenda kufanya kazi mbalimbali.Sabiya na Waridi ni mfano wa watoto wa kike wanaojipata katika hali hizi. Sabiya na wasichana wengine wa umri mdogo wanajipata katika ukahaba baada ya kukosa kazi walizotarajia kuzipata.Naye Waridi anasafirishwa Ughaibuni anakoenda kufanya kazi ya ulezi.

Katika hali halisi ya maisha ya binadamu, watoto hujipata katika hali kama hizi zinazodhihirika katika *Tikitimaji*.Wasichana kwa wavulana wanapatikana wamefungiwa katika majumba tofauti tofauti wanakotoa huduma zisizoeleweka.Hata hivyo, watoto hawa wanaokolewa na kupelekwa katika makao ya watoto ya Gwadalupe.Vijana wa Tikitimaji wanaojitolea kujisaka na kuelewa matatizo ya nchi yao, huku wakishauriana na

wazee, ndio wanaowaokoa watoto hawa.Zinji, Sapna, Maya na kombo ni vijana wanaoelewa fika kuwa elimu ni njia mojawapo inayoisaidia jamii kupigana na umaskini kwani wao walilelewa na kusomeshwa na Mama Rehema katika makao ya Gwadalupe, na sasa wanajitegemea wao wenyewe na pia wamekuwa tegemeo la Tikitimaji nzima.

## 2.11 Hitimisho

Ni dhahiri kuwa mwandishi wa *Tikitimaji* ameshughulikia maswala yanayomwathiri binadamu takribani kote ulimwenguni na kudhihirisha hali halisi za maisha kama yalivyo.Kwa hakika Uhalisia unadhihirika wazi katika maswala makuu ambayo mwandishi ameangazia, ukiwemo uharibifu na uchafuzi wa mazingira, utelekezaji wa watoto, miundo msingi mibovu, suala la mfumo wa uchukuzi, makundi ya upinzani na ukombozi, ukiukaji wa haki za watoto na mengineyo.

Mwandishi ameweza kuyawasilisha masuala haya kwa njia ambayo inaaminika na kukubalika na wataalamu kwani, masuala haya ni ya kihalisia tunayoyashuhudia katika maisha yetu ya kila siku.Katika kuyafafanua maswala haya, mwandishi ameyaweka katika muktadha wa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kisaikolojia ili yaweze kuonekana wazi katika hali zote za maisha ya mwanadamu.

# SURA YA TATU

# UCHANGANUZI WA LUGHA YA KITAMATHALI KATIKA *TIKITIMAJI*

## 3.0 Utangulizi

Swala la lugha lina umuhimu mkubwa katika uhakiki wa kazi yoyote ya kifasihi.Dhana ya lugha imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali akiwemo Senkoro (1982:13), anapoeleza kuwa kipengele cha lugha ndicho muhimu sana kwani ndicho kinachotofautisha fasihi na sanaa nyinginezo kama vile uchoraji, ufinyanzi, uchongaji na nyinginezo.Lugha basi ndiyo njia ambayo mwanafasihi hutumia kuyaeleza mambo yanayohusu jamii kwa njia ya kiubunifu.

Mdee (1986) anaieleza lugha kama chombo kilichoundwa na mwanadamu kwa ajili ya mawasiliano. Naye Mgullu (1999:6), anaeleza kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa kwa mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake.

Katika fafanuzi hizi zote, kuna makubaliano kuwa lugha ni mfumo wa nasibu unaotumiwa kuwasiliana.Kutokana na maelezo haya, inaaminika kuwa lugha ikitumiwa ipasavyo huimarisha mawasiliano na ikitumiwa vibaya huenda ikatatatiza mawasiliano.Kwa hivyo,msanii anayeitumia lugha ipasavyo kutegemea hadhira yake huimarisha mawasiliano kwa kuwa ataeleweka ipasavyo na ujumbe wake utapokelewa kwa njia mwafaka na inayoathiri hadhira yake kama anavyokusudia.

Lugha, kama asemavyo Wamitila (2003), ina nafasi kubwa sana katika fasihi kwa kuwa fasihi yenyewe ni sanaa ya lugha.Lugha ni nguzo kuu ya kazi za fasihi na uchunguzi

wowote wa kazi hizo hauna budi kuangalia suala la lugha kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja.Kazi ya kifasihi huyawasilisha maudhui yake, dhamira yake na maana yake kwa kuitegemea lugha.Katika sura hii, tumeangazia sifa mojawapo ya lugha ya kifasihi ambayo ni tamathali za usemi.

Dhana ya tamathali za usemi imefafanuliwa na wahakiki mbalimbali.Senkoro (1982), anaeleza kuwa, tamathali za usemi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wanafasihi kuongeza kiwango cha ujumi katika kazi fulani.

Naye Mbatiah (2001:77), amefafanua tamathali za usemi kama ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno, ili kuleta maana mpya au msisitizo.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), tamathali za usemi ni kama vile tashbihi, sitiari, tashhisi, tasfida n.k. Ufafanuzi uliotolewa na Mbatiah na Wamitila ndio unaotufaa zaidi katika uchambuzi wetu kwani tunaangazia jinsi msanii anavyogeuza lugha kimaksudi ili kusisitiza ujumbe fulani katika kazi yake.Msanii wa *Tikitimaji* ametumia tamathali za usemi nyingi, zikiwemo, tashbihi, misemo, methali, utohozi, kuchanganya ndimi n.k, ili kusisitiza lengo lake kuu, na hasa katika kutilia nguvu maudhui aliyolenga kuyaangazia.

### 3.1 Matumizi ya Tashbihi

Kama wasemavyo King'ei na Kemoli (2001:55), tashbihi pia huitwa tashbiha au mshabaha.Hii ni lugha ya ulinganishaji ambapo vitu viwili halisi vinavyolinganishwa huwa vinaonyesha mshabaha fulani wa sifa, sura au tabia. Naye Wamitila (2003:222), anaeleza kuwa tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia

waziwazi.Tashbihi hutambulishwa na matumizi ya viungio: kama, mfano wa, mithili ya, ja, kama vile, sawa na, n.k.

Ufafanuzi zaidi kuhusu tashbihi unatolewa na Mohammed (1995:125), anapoeleza kuwa msingi wa tashbihi katika fasihi ni ule wa kutafuta namna ya kuweka wazi maana, dhana, picha au hali fulani kwa mujibu wa ulinganifu wa kipicha.

Mwandishi wa *Tikitimaji* ametumia tashbihi kwa mapana na marefu katika kulinganisha hali au vitu mbalimbali anapoendelea kufafanua maudhui na dhamira katika kazi yake. Zinji alikuwa na hamu kuu ya kutaka kujua habari za siri kumhusu ambazo zilikuwa hukoTikitimaji.Naye Mama Rehema ambaye aliijua siri hii hakutaka kuharakisha kumweleza Zinji kuihusu. Katika hali ya kungojea, ndipo Zinji anaposema: "hakikuwa kipindi kirefu lakini kwangu kilikuwa kama dahari nzima ya wakati"(uk.10).

Mwandishi anatumia tashbihi hii kuonyesha hamu kuu aliyokuwa nayo Zinji kutaka kujua asili yake iliyokuwa huko Tikitimaji ambapo Ami yake mdogo na aliyemnyang'anya mali yake alikuwa anaishi.Katika kufanya hivi, msanii anamtia msomaji hamu ya kutaka kujua siri hii ilikuwa ipi na kwa nini Zinji ana hamu kubwa kiasi hiki ya kuisikia siri hii.Baada ya Mama Rehema kumweleza Zinji kuwa Tikitimaji kuna siri aliyotaka kuijua tangu zamani, hasemi kwa muda mrefu na badala yake anatoa bahasha kubwa ya kaki.Baadaye anaingiza mkono wake ndani ya bahasha na kutoa kibahasha kidogo.Zinji anaeleza:

> Alininyooshea kibahasha hicho kidogo ajabu.Nilikichukua bila ya kusema jambo.Nilikuwa bado nasubiri maagizo mengine Kama tarishi aliyekabidhiwa risala (uk. 10).

Maneno haya ya kiulinganishi yamekusudiwa kuonyesha jinsi Zinji alivyokuwa na hamu kuu ya kutaka kuijua asili yake.Hamu ya kutaka kujua siri iliyomngoja Tikitimaji.Msomaji naye anatiwa katika hali ya taharuki ya kutaka kusoma zaidi ili naye aweze kufahamu asili ya zinji.

Mwandishi ametumia tashbihi katika sehemu hii ili kutuonyesha uhusiano wa karibu baina ya

Zinji na Mama Rehema ambaye alikuwa mlezi wake. Zinji anaeleza:

> Mama Rehema aliniangalia. Akavuta tabasamu.Vidu vya kutamanisha vilijiunda mashavuni. Nilimkaribia na kumkumbatia kwa nguvu zote nilizokuwa nazo. Mpumuo wake ukaungana na wangu. Mili yetu ikawa inachezacheza kama mtu aliyeko kwenye bembea. Mawazo yangu yaliruka kama purutangi hadi walipokuwa wenzangu (uk.11).

Maneno haya yanatumiwa wakati Zinji na wenzake walifika Gwadalupe kumtembelea Mama Rehema.Maneno haya yanadhihirisha mapenzi aliyokuwa nayo Zinji kwa mama aliyemlea na kumsomesha ingawa huyu mama hakuwa mamake mzazi.Kauli hii pia inachangia kuendeleza maudhui kuhusu makao ya watoto, nafasi ya mwanamke katika jamii na kutelekezwa kwa watoto.

Tashbihi nyingine iliyotumiwa ni: “shauku ya safari yenyewe ilitunasa na kutuvuta mbele kama ng’ombe wa shemere kwa matamanio (uk.15)”.Haya ni maneno ya mhusika msimulizi akijirejelea pamoja na wenzake ambao wanasafiri naye kuelekea Tikitimaji.Vijana hawa, Zinji, Sapna, Maya na Kombo wanafunga safari kwenda

Tikitimaji ili kujisaka na kudadisi ili kujua matatizo yanayoikumba Tikitimaji.Wana shauku ya kupata uvumbuzi wa jinsi mambo yalivyo Tikitimaji.Zinji ana hamu zaidi ya kukutana na Ami mdogo aliyemdhulumu.

Mwandishi pia ametumia tashbihi kudhihirisha jinsi Tikitimaji ilivyokuwa imenyongwa na mmomonyoko wa udongo.Msimulizi anasema: "mizizi ya miti na mimea ilitokeza kama matanzu ya mgunga mweupe" (uk.23). Kauli hii inasisitiza jinsi utawala ulioshikilia hatamu za uongozi wakati huo ulikuwa na ujuhali mwingi wa kuachilia udongo kumomonyoka na mizizi ya miti kuachwa wazi hata kandokando ya barabara. Hii inamaanisha kwamba, juhudi hazikufanywa na wizara ya mazingira kulinda na kutunza mazingira inavyopasa.Tena miti hii ilikuwa kando kando ya barabara na ilitishia kuwaangukia watu au hata magari yaliyopitia kwenye barabara hiyo.Maisha ya watu yalihatarishwa.

Tashbihi zingine zilizotumiwa ni: "sote tulitamani kuufikia mto huo kama mtu mwenye kiu anayetamani kuyapata maji ya kuikonga kiu yake" (uk.23).Tashbihi hii inatumika kuonyesha jinsi vijana hawa walivyokuwa na hamu kuu ya kuuona mto huu na kuutumia kutathmini athari za uharibifu wa mazingira.Tashbihi nyingine ni: "Tulitembea kimyakimya, pole pole kama mtu anayepita kwenye jabali lenye kinamasi.Mwishowe tukatokeza sehemu ya chini kabisa.Tukapumua kama mtu aliyekuwa kwenye njia ya chini kwa chini iliyojaa giza" (uk.24).

Mwandishi anatumia mbinu hii ya ulinganishi kuonyesha ilivyokuwa kazi ngumu kupitia kwenye barabara iliyokuwa na miti iliyoinamiana kuelekea barabarani kutoka pande zote mbili za barabara.Ilibidi watu waliotembea kwenye barabara hii kupinda huku na kule

kuepuka kuzongwazongwa na mimea hiyo.Msimulizi anazidi kueleza kuwa ilikuwa vigumu sana kuamini kuwa hii ilikuwa barabara.Maneno haya yanazidi kuendeleza maudhui ya miundo msingi mibovu, jambo ambalo linadhihirika wazi Tikitimaji.

Msimulizi anaeleza hali ya Mzee Jududi alipokuwa akijiandaa kuwasimulia hadithi kwa kutumia tashbihi ifuatayo: "mzee Jududi naye akapumua kama hamali aliyejiandaa kulibwata gunia lililomlemea mabegani". Maneno haya yanatuelekeza kwenye usimulizi wa mzee Jududi kuhusu yaliyowapata watu wake nchini Tikitimaji.Maneno haya ya kulinganisha mpumuo wake na hamali yanadhamiriwa kueleza jinsi mzigo wa mawazo akilini mwake ulivyokuwa mzito.Yaliyompata mzee Jududi yalikuwa makubwa na ndiyo haya aliyotaka kusimulia ili angaa yampungukie akilini na moyoni.

Mzee Jududi anasimulia jinsi walivyofurushwa katika msitu wa mlima Tirimacho na kiongozi wao ambaye ni Jitikiti na mlima ukauziwa Durago. Matumizi ya tashbihi hii, kwa hivyo, yanadhamiriwa kuendeleza ujumbe wa dhuluma na unyanyasaji unaoendelezwa na viongozi wa Tikitimaji.

Mzee Jududi anapoeleza jinsi zamani Tikitimaji ilifunikwa na blanketi zito la kijani na jinsi hewa ilikuwa safi, analinganisha hali hii ya zamani na sasa ambapo hewa inayoingia mwilini ina joto na vumbivumbi na kwamba, mtu anatamani kuitoa nje kwa kasi kama tapishi (uk.44).

Ulinganishaji huu wa hewa chafu yenye joto na vumbi vumbi, na tapishi, unadhirisha jinsi mazingira yalivyoharibiwa na kuchafuliwa hadi inawawia vigumu wakaazi wa Tikitimaji kuivuta hewa yenyewe.

Kama tulivyosema awali, mwanafasihi sharti atumie lugha mwafaka ili kuwasilisha ujumbe wake kwa njia inayomwezesha kugusa hisia na kuwaathiri wasomaji ipasavyo.Kwa kutumia tashbihi hii, msomaji anajenga taswira ya uoni ambapo anaona hali ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira ilivyokuwa imekithiri Tikitimaji.Kwa njia hii, mwandishi anaendeleza ufafanuzi wa dhamira yake kuu ambayo ni uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Maya, Kombo, Sapna, na Zinji wanapomwambia Mzee Jududi kuwa hawakuwa wanamjua Jitikiti na kuwa hawakuwa wamemsikia, alinyamaza, akapumua kwa nguvu kama mwele wa pumu (uk.55).Mzee Jududi anashangazwa na kauli ya vijana hawa kwani Jitikiti alijulikana hata na watoto wa shule nchini Tikitimaji.Anasisitiza kuwa kila mtu anapaswa kuwa anamjua Jitikiti kwa kusema kuwa, Tikitimaji inayotawaliwa na Jitikiti iko kila mahali (uk 54).Hii inamaanisha kuwa, utawala dhalimu unapatikana katika mataifa mengi ulimwenguni na si tatizo la nchi moja pekee.Mzee Jududi anawahimiza vijana hawa kupambana na udhalimu wa viongozi kama hawa kwa ujasiri mwingi.

Mwandishi ametumia mbinu hii ya ulinganishi mara kadha katika hadithi inayosimuliwa na mamake Shamsi.Msimulizi wa hadithi anaeleza kuwa jitikiti lililokuwa shambani lilikuwa linazungumza na kijana aliyekuwa anawinga ndege aliposikia jitikiti likizungumza, alifyatuka kama mshale kuelekea nyumbani.Kijana alipowaeleza wanakijiji aliyoyashuhudia, wote walienda shambani na mmoja wao akalirushia jitikiti lile upanga uliolipasua.Msimulizi anasema: "ule upanga ulilipasua lile jitikiti kubwa ajabu.Ghafla kama umweso kumweka pakaibuka rumbi la jitu.Watu walianza kutoroka lakini hakuna aliyenusurika.Jitu hilo liliwameza kama jinamizi.Liliwafuta wote na kubakia likiiramba midomo yake kwa tamaa kama majuju wa majuju (uk.75).

Matumizi ya tashbihi hii hapa inasisitiza maudhui ya dhuluma ambapo jitikiti linawaogofya na hatimaye kuwameza wanakijiji wote.Hii ina maana kwamba, wenye navyo wanawanyanyasa wasio navyo na walala hoi wanapojaribu kujitetea na kujikomboa, wanakandamizwa hata zaidi hata kwa kutumia vyombo vya dola kama vile polisi na hatimaye wanaangamizwa.

Mama Shamsi anapomaliza kusimulia hadithi yake anawaangalia Zinji, Maya, Sapna na Kombo. Mwishowe, kwa sauti ya chini mfano wa mtu anayeshuku anasikilizwa, anasema, "kuna fununu kuwa hadithi hii haipendwi na Ami mdogo" (uk.76).

Ujumbe anaoupata msomaji ni kwamba, wakazi wa Tikitimaji walikuwa wametiwa woga, kiasi kwamba, hawangezungumza kwa uwazi kuhusu kiongozi wao, kumaanisha kwamba, hawakuwa na uhuru wa kujieleza.Hali hii ya hofu ilikuwa imeenea Tikitimaji kwani hata bawabu alipoulizwa kuhusu Ami mdogo, anazungumza kwa sauti ya chini na kwa tahadhari kubwa.

Mwandishi analenga kuonyesha jinsi wanajamii walivyonyimwa uhuru wa kujieleza jambo linalokwamiza juhudi za jamii nyingi kujikomboa kutokana na utawala dhalimu.Wanaharakati kama vile Mzee Jududi, Mzee Dhamiri na mwalimu Insafu wanapojaribu kuzungumza kuhusu maovu ya viongozi wanafurushwa na wengine kupoteza kazi zao.

Baada ya Zinji, Maya, Sapna na Kombo kupata malazi kwa mamake Shamsi, hawakupata usingizi. Tunaelezwa kuwa, walipoamka asubuhi, "macho ya Maya yalisharabu wekundu mithili ya pilipili iliyoiva na yale ya Zinji nayo yalikuwa mekundu kama ngeu" (uk.77). Kwa kuwa vijana hawa walikuwa katika safari ya kujisaka na kujifahamu, safari

iliyokuwa na matatizo mengi, hawakupata lepe la usingizi kwa kuwazia hali waliyosimuliwa na mamake Shamsi.Yaani hadithi ya jitikiti lililowameza wanakijiji wote.Huenda walikuwa wanawaza jinsi ya kupambana na jitikiti hilo, yaani udhalimu uliokithiri Tikitimaji.Baada ya Shamsi kuwasindikiza wageni wao na kuwaaga, Zinji anasema: "Tulisimama kwa muda kama msafiri anayetaka kukadiria umbali uliobakia wa safari yake" (Uk.79).

Vijana hawa wamegundua mengi yakiwemo uchafuzi na uharibifu wa mazingira, udhalimu, utelekezwaji wa watoto lakini safari yao ya ugunduzi haijafika mwisho.Zinji bado hajampata Ami Mdogo aliyemnyang'anya urithi wake. Anaona kuwa safari hii haiwezi kukamilika kabla ya kukutana na Ami mdogo, akikumbuka kuwa, lengo hasa la safari hii ya kuelekea Tikitimaji lilikuwa kumtafuta Ami Mdogo ambaye hapo awali alikuwa amemnyanyasa.

Zinji, Maya, Sapna na Kombo wanapoendelea na safari yao kuelekea Tikitimaji wanakutana na vijana wanaowaeleza kuwa wazazi wao wanafanya kazi huko Tirimacho kwenye machimbo ya shaba nyekundu.Wanasema kuwa huko kuna kazi nyingi lakini kijijini hakuna kazi. Wanasema: "Huku kijijini kazi hazipatikani! Zimeadimika kama barafu ya kukaanga!" (uk.83).

Mwandishi ametumia ulinganisho huu wa kuadimika kwa kazi na barafu ya kukaanga kuonyesha jinsi uhaba wa kazi ulivyokuwa ukekithiri katika jimbo la Tikitimaji.Dhamira ya uhaba wa kazi inafafanulika zaidi mwandishi anapotumia mbinu hii ya lugha kwani msomaji anaweza kutumia picha ya akilini kuona hali ilivyokuwa.Kwa njia hii, ujumbe

wa mwandishi unawafikia wasomaji kwa ubayana zaidi kuliko ilivyo kama mtunzi angetumia lugha ya kawaida, kwa kusema kuwa Tikitimaji kulikuwa na ukosefu wa kazi.

Mwandishi anapoeleza kuhusu harufu mbaya inayohisika kwa mbali kutoka mji wa Tikitimaji, anasema kuwa Sapna ndiye wa kwanza kuhisi harufu hiyo.Wenzake wanamfanyia mzaha kwa kumwambia kuwa pua yake ilikuwa na ukali wa wembe. Kadiri vijana hawa wanavyosonga mbele kuelekea Tikitimaji ndivyo harufu inavyoongezeka.Msimulizi anaeleza: "Wimbi kubwa la harufu ya uozo likawa nusura kutuzoea na kutupeperusha juu kama usufi uliosombwa na chamchela" (Uk.88).

Katika hatua hii, Sapna anawaambia wenzake: "mazingira yetu yamechafuliwa na kuwa ya kukera kwa sababu pua za wengi zilishafaliji na kukosa uwezo wake wa kimsingi" (uk.88).Lugha hii inayotumiwa na mwandishi inadhamiriwa kutilia nguvu wazo kuwa mazingira yalikuwa yamechafuliwa na uvundo ukaenea kwingi lakini watu walikuwa wamezoea uvundo huo na ukawa kama jambo la kawaida kwa wanatikitimaji.Sapna alianzisha vuguvugu la WAZALIMA ili kuizoa takataka na kuwaonyesha Wanatikitimaji kuwa uchafu na harufu yake havizoeleki. Baada ya muda mfupi kundi la WAZALIMA linakuwa na wanachama wengi sana. Tunaelezwa: "Kundi lenyewe lilikuwa kama chavua iliyowavuta nyuki na wadudu wengine" (uk.128).Hii ina maana kuwa kundi analolianzisha Sapna linapata wanachama wengi ajabu wanaoendeleza Juhudi za utunzaji na usafishaji wa mazingira. Shamsi na mamake pia wanajiunga na kikundi hiki.

Mwandishi anatumia mbinu hii ya lugha kuonyesha kuwa, jambo ndogo linaloanzishwa na mtu mmoja mwenye nia nzuri ili kuweza kurekebisha hali fulani iliyoharibika laweza kukua na kusambaa haraka sana. Kwa hivyo, binadamu asinyamazie hali isiyopendeza

katika jamii bali achukue hatua ya kwanza na huenda hatua hiyo ikazua mambo makubwa ya kunufaisha jamii. Msimulizi anatuchorea picha ya mji wa Turuturu nyakati za usiku na mchana kwa kusema yafuatayo:

> Mchana mji wenyewe ulifufumaa mfano wa bundi aliyejificha mapangoni halafu akatokeza usiku na kuanza kurukaruka huku na kule.Usiku tumba hiyo ya siri ilipapatuka na kutoa picha isiyokuwa ya kawaida.Barabara za mjini ambazo mchana hazikuwa na harakati nyingi zilivuvumka ghafla.Yale mandhari ya usiku yalikuwa kama kichocheo kilichowavuta watu waliofuchama mfano wa kumbikumbi walioinusa harufu ya mvua (uk. 139).

Pembe za barabara zilitapakaa wasichana, wanaume na watu wa kila aina. Katika mji huu ndiko alikokuwa amepotelea Sabiya na wasichana wengine wengi wa umri wake. Shughuli zilizoendelezwa katika mji huu majira ya usiku zilisheheni ukahaba mwingi na waliohusika ni wasichana wadogo na wanaume matajiri.Mwandishi anapotumia ulinganisho wa kumbikumbi na watu waliotokeza mjini Turuturu usiku, anatuchorea picha ya jinsi shughuli za usiku zilikuwa na wahusika wengi kuliko zile za mchana. Ni bayana kuwa kuna uozo na uvundo mijini kwingi nyakati za usiku ambapo biashara za danguro huendelezwa na matajiri wanaowatumia watoto wa umri mdogo wanaopaswa kuwa shuleni. Ingawa suala hili la watoto kutumiwa namna hii limeangaziwa na wasanii kadha bado linaendelea kuwaathiri watoto wasichana kwa wavulana katika jamii nyingi za binadamu.

Kwa kuhitimisha sehemu hii, tunatoa kauli kuwa, mwandishi amefanikiwa si haba kutumia mbinu hii kuioanisha dhamira pamoja na maudhui aliyoyateua katika kazi

yake.Tashbihi alizoziteua kuendeleza mawazo yake kuhusu uchafuzi wa mazingira, udhalimu na unyanyasaji, ukiukaji wa haki za watoto na ukahaba, zimemsaidia sana katika kuchora picha halisi ya uozo ulioko Tikitimaji.

### 3.2 Methali

Ngure (2003:133), anaieleza methali kama semi fupi zenye maana fiche zinazokubalika na kutumiwa kufafanua ukweli na hekima ya jamii. Dhana ya methali imefafanuliwa pia na Matei (2011:61), anaposema kuwa methali ni semi fupi fupi za kimapokeo zenye kueleza fikira, maarifa na hekima. Kulingana na M'Ngaruthi (2008), methali ni kifungu cha maneno yanayotumiwa pamoja kisanii, kwa njia ya kufumba au kupigia mfano jambo fulani.Wahakiki hawa wanaafikiana kuwa methali ni semi zinazofumba maana katika kueleza fikra fulani.

Methali huchukua maana ndefu na pana kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa.Maneno yanayotumiwa kuunda methali hutumiwa pamoja kisanii kwa sababu huenda mtumiaji methali akaitumia kwa njia tofauti na ilivyozoeleka na bado maana yake ikabakia ile ile iliyokusudiwa. Kwa mfano tukisema, 'ganga ganga yao ilimlaza mgonjwa na matumaini', maana inabakia kuwa, 'ganga ganga ya mganga humlaza mgonjwa na matumaini'.Kwa hivyo, kisanii si lazima methali itumike kama ilivyozoeleka. Katika *Tikitimaji* mwandishi ametumia methali nyingi zinazomwezesha kuwasilisha ujumbe wake pamoja na kuipamba kazi yake.

Mwandishi ametumia methali, "wavuvi wa pemba hujuana kwa vilemba" ( uk.11). Methali hii inatumiwa na Zinji anapoeleza kuwa alielewa ujumbe wa Mama Rehema anapomwambia kuwa, sasa alikuwa na kifua cha kuujua ukweli.Kwa kuwa Zinji alikuwa

anajua ni ukweli upi Mama Rehema alikuwa anauzungumzia, hakuona haja ya kuuliza huo ulikuwa ukweli gani. Wao wawili waliuelewa ukweli huo uliohusu asili ya Zinji.Zinji alikuwa amemdadisi Mama Rehema kwa muda mrefu ili amweleze ukweli wa asili yake, na sasa Mama Rehema yuko tayari kumuelekeza ili aende akajifumbulie ukweli wenyewe huko Tikitimaji.

Kama tunavyoelezwa baadaye katika hadithi, Zinji alikuwa amefiwa na wazazi wake akiwa mdogo sana na hivyo ami yake akaachiwa mali yake ili akikua amrithishe, lakini haikutokea kuwa hivyo.Badala ya kumrithisha Zinji mali ile, Ami Mdogo huyo alimpokonya Zinji mali yenyewe kwa madai kuwa mwanamke hakupaswa kurithishwa mali.Hii ndiyo siri Zinji anayotaka kuijua kutoka kwa Mama Rehema.

Kombo anatumia methali, “likujialo pambana nalo" (uk.19), anapomhimiza Sapna aliyeonekana kuwa na wasiwasi kuhusu ile njia waliyokuwa wakiifuata kuelekea Tikitimaji. Sapna anasimama kama anayechelea kusogea mbele na kusema, “Hii njia... Hamwoni ilivyokaa ni kama imeachwa kabisa! (uk.19).Naye Kombo anamhimiza kwa kumwambia kuwa hawawezi kuogopa na kuwa ikiwa kungetokea hatari wangeweza kupambana nayo wote.Katika hatua hii ndipo anatumia methali iliyo hapo juu.Vijana hawa wamo safarini ambayo ni ngumu ili waweze kutambua shida zinazoikumba jamii yao kwa matumaini kuwa wangeweza kusaidia kupata suluhisho.Baadhi yao wanapoanza kufa moyo, wenzao wanawahimiza ili wawe na nguvu za pamoja za kuwawezesha kupambana na maovu katika jamii yao na kuweza kushinda.

“Mgeni njoo mwenyeji apone” (uk.34), ni methali nyingine inayotumiwa na Mzee Jududi anapowarejelea Zinji, Sapna, Maya na Kombo, ambao ni wageni wanaofika Tikitimaji na

huenda wakawasaidia wanatikitimaji kutatua matatizo yanayowakumba.Mzee Jududi anawambia: "wanangu huenda mkatusaidia kulifumbua tatizo la watu wangu!" (uk.34).Mzee Jududi na watu wake walikuwa wamefurushwa kutoka msitu wa Tirimacho kisha mlima ukauziwa Durago.Msanii anatumia methali hii kusisitiza kuwa sharti wanajamii wanaonyanyaswa washirikiane ili kusaidiana kuondoa udhalimu.Mzee Jududi ni mzee mwenye hekima ya kutumia methali anapotaka kuwasilisha ujumbe fulani.Anasema: "Mambo ni Kangaja huenda yakaja" (uk.37), anapowasimulia kina Zinji habari kuhusu walivyokuja watu na kuwambia kuwa walikuwa wameununua mlima Tirimacho alikoishi Mzee Jududi na watu wake kwa dahari na dahari.

Maishani mambo hutokea bila kutarajiwa na ndivyo yalivyotokea kwa Mzee Jududi na watu wengine walioishi Tirimacho.Mzee Jududi na wengine walioishi Tirimacho walikuwa na tabia ya kuwakaribisha wageni na hivyo, watu hao walipofika, wakasema kuwa mgeni ni baraka na kuwa hata akiwa mgeni mbaya ataondoka.Mgeni ni maji ya mto, hupita yakaenda kwao (uk. 38). Hii ndiyo iliyokuwa falsafa ya Mzee Jududi na wanatirimacho wenzake.Lakini badala ya mgeni kufika na kuondoka alikaa kitako na kusema kuwa alimiliki mlima.Watu hao waliofika walitoa stakabadhi za kuonyesha kuwa, kwa kweli walikuwa wameuziwa mlima.Mzee Jududi na watu wake wakafurushwa na mlima ukamilikiwa na Durago.

Methali zilizotumiwa katika muktadha huu, zinachangia kusisitiza hali iliyowajia wakaazi wa Tirimacho bila kutarajia huku wakidhani kuwa wageni waliowatembelea walikuwa wageni wa siku tatu.Kumbe walikuwa washaauziwa mlima na tayari ulikuwa milki yao! Mwandishi anatumia methali hizi kuendeleza maudhui ya udhalimu ambapo viongozi wananyakua ardhi ya watu na kuitumia kwa manufaa yao.

Wageni walipowaonyesha Wanatikitimaji karatasi kuthibitisha wao ndio wamiliki wa mlima, Wanatikitimaji walidhani ulikuwa utani.Mzee Jududi anasema:

> Tukasema kuwa utani ni mzuri lakini ikiwa utani wao utafuata mtindo huu basi si mzuri.Mzaha mzaha hutumbuka usaha. Wakaangua kicheko mara hii.Wakasema kile ni cheti cha ardhi.Cheti kile kinaonyesha wamenunua mlima wenyewe.Ule mlima ni wao.Muda mfupi baadaye tukaanza kufurushwa walikoishi jamaa zetu tangu jadi na asili (uk.39).

Mzee Juhudi na watu wake walipuuza mambo haya ya wageni kuuziwa mlima lakini hatimaye waligundua ukweli wa mambo walipofurushwa kutoka ardhi yao ya jadi.Huu ni udhalimu uliokithiri.

"Sahau ni dawa ya waja" (uk.40) ni methali nyingine anayoitumia Mzee Jududi kuonyesha kwamba baada ya dhuluma hii, watu wa Tikitimaji walianza kusahausahau yaliyotokea na jambo hili likawafanya viongozi kusherehekea.Kama asemavyo mhusika Kame katika tamthilia ya *Kifo Kisimani* iliyoandikwa na Kithaka wa Mberia, wananchi ni watu wa kusahausahau haraka dhuluma za viongozi.Wanyonge hunyanyaswa na kudhulumiwa kwa kuporwa mali, watoto wao kunyimwa haki na kukosa kazi huku rasilimali ya taifa ikitumiwa kibadhirifu, lakini baada ya muda fulani kupita wanayasahau madhila yote haya! Viongozi wanapogundua usahaulifu huu, wanazidisha dhuluma na unyanyasaji wao.Wanyonge wanahimizwa kutosahahu maovu ili wazidi kupambana nayo hadi siku watakapofanikiwa.

Mzee Jududi anawahimiza Zinji, Sapna, Maya, na Kombo wasikate tamaa kwa kuwambia, "penye mawimbi na milango i papo" (uk.46). Methali hii ina maana kuwa

chombo kinapokabiliwa na mawimbi makali huwa kinakaribia njia au mlango wa kuingia bandarini.Hivyo haifai kufa moyo au kukata tamaa matatizo yanapozidi kwani mwisho wa matatizo hayo huwa hauko mbali.Vivyo hivyo, baada ya Sapna na Zinji kujishughulisha na mapambano dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa kuandaa maandamano na kuandika habari hizi magazetini, hawafi moyo bali wanaendeleza vita hivi kwa nguvu mpya.Huu ndio ushauri na himizo wanayopata kutoka kwa Mzee Jududi na anaamini kuwa baada ya muda mfupi watafanikiwa.Utabiri wa mafanikio wa Mzee Jududi unatimia wakati Sapna anakubaliwa kuanzisha vuguvugu la WAZALIMA linaloondoa rundo la uchafu uliorundikana kando kando ya barabara za mji wa Tikitimaji.

Zinji anakumbuka methali ya Kiswahili inayosema: "pauliwapo nyoka hapaachi ndombezi" (uk.48).Kwa mujibu wa King'ei na Ndalu (1989:285), Methali hii ina maana kuwa nyoka ni hasimu wa watu na anapouliwa wenzake hutaka kulipiza kisasi kwa kumshambulia mtu.Hii inamaanisha kwamba mahali penye kutokea kisa cha uadui, huwa na dalili za chuki na uhasama kila mara.Zinji anarejelea methali hii kumaanisha kwamba nchini Tikitimaji, watu walikuwa na matatizo mengi yakiwemo yale ya ukosefu wa malisho kwa mifugo wao, mito kutishia kukauka, watu wa kawaida kunyang'anywa ardhi yao na watetezi wa haki kukabilianwa nao vikali na kufurushwa kutoka nchini mwao. Hali hii ndiyo iliyozua uhasama baina ya viongozi na watawaliwa.

Mzee Jududi anapowaaga Zinji, Sapna Maya na kombo wakati wa jioni anawapa ushauri ufuatao:

> Mkiona usiku unaingia kabla ya kufika mwisho wa safari yenu, msione ugumu kutafuta msaada.Licha ya kuwa watu wa huku ni mafukara wa ulimwengu, lakini ni wakarimu sana.Kutoa ni moyo, usambe ni utajiri.Huku, ule mkono mtupu unarambwa (uk.56).

Matumizi ya methali hizi yanatudokezea kuwa, Tikitimaji watu ni wachoyo kiasi kwamba, mtu hawezi kumsaidia mwenzake ikiwa hatarajii kwamba, pia yeye angepata msaada kutoka kwake.Lakini katika sehemu wanakoelekea vijana hawa wanagundua kuwa Tikitimaji mna watu wa aina tofauti tofauti, wakiwemo wachoyo ingawa ni matajiri na wengine wakarimu ingawa ni maskini. Ukweli wa kauli hii unawadhihirikia wanapofika nyumbani kwa mamake Shamsi ambaye anawapokea kwa mikono miwili, akawapa mahali pa kulala na pia chakula.

Mwandishi ametumia methali "majuto ni mjukuu" (uk 62), "dudu liumalo halipewi kidole" (uk.65), na "maji ukiyavulia nguo lazima uyaoge" (uk.68).Methali "majuto ni mjukuu" inatumika kuonyesha kuwa sharti vijana hawa wafuate ushauri wa Mzee Jududi wa kutafuta mahali pa kulala wasije wakajuta. "Dudu liumalo halipewi kidole" inatumika kuonyesha kuwa ingawa Shamsi alielezwa kuwa Kombo (polisi) hakuwa na neno, bado alikuwa hamwamini kwani nchini Tikitimaji polisi walikuwa wanawahangaisha wanyonge.

Zinji, Maya, Sapna na Kombo wanahimizana kwa kutumia methali ifuatavyo: "tulishayavulia nguo maji, basi hatuna budi kuyaoga".Wanajihimiza hivi wakati safari yao imeanza kuwalemea ili wawe na moyo wa kuendelea.Mwandishi pia ametumia

methali “nyani wanachekana ngoko” (uk.94).Mzee Dhamiri anatumia methali hii anapoeleza madhila yanayowakumba watu wa kawaida.anaeleza:

> Nilimwambia Jitikiti na masahibu wake, mkaangapo tu chini ya gae wakadhani hatuoni.Tangu zamani wanadhani hatuna macho. Ni kama huyo mwenzake Sastima ambaye zamani alikuwa anamkashifu, mambo ya nyani na ngoko wake.Mmm...wanadhani kwa kuwa hatuonyeshi uchungu hautuumizi (uk.94).

Mzee Dhamiri anatumia methali hii kuonyesha kuwa Tikitimaji iliongozwa na viongozi wadhalimu na kwamba kiongozi aliyepo sasa anamnyooshea kiongozi aliyemtangulia kidole cha lawama bila yeye kujiona anavyotawala kidhalimu.Kwa kawaida, kiongozi mmoja akifurushwa na mwingine kuchaguliwa, mambo huwa yaya haya ya kulaumu wengine bila mtu kujichunguza na kurekebisha maovu yaliyomo katika uongozi wake.

Nia anatumia methali, “Nyoka anapoingia shimoni huingizi mkono wako kumtafuta” (uk.113). Kauli hii inamrejelea mwalimu Insafu ambaye inadaiwa kuwa watu walipomkataa kijijini alikimbilia upande walipokuwa wamefika Nia, Maya, Sapna na Zinji.Mwalimu Insafu alikuwa amefurushwa na Jitikiti kwa madai kuwa alikuwa anawachochea watu.Ni mmoja wa wanaharakati wa ukombozi waliofurushwa Tikitimaji.Nia anapoeleza kuwa hakuna aliyemfuatilia mwalimu Insafu huko alikotorokea ndipo anapotumia methali, “nyoka anapoingia shimoni huingizi mkono wako kumtafuta”( uk.113).

Mwandishi ametumia methali hii kuendeleza maudhui ya ukombozi na matatizo yanayowakumba wanaharakati wake, katika Juhudi za kujinasua kutokana na minyororo ya ukandamizaji.Mwalimu Insafu anapoteza kazi yake na pia kufurushwa kutoka makao yake na kuhamia kwingineko hali inayomfanya kutofurahia uhuru wake.

Ndugu Kikwiro ambaye ni afisa wa usafi anapoambiwa na Sapna kuwa vuguvugu alilotaka kulianzisha Sapna lilikuwa linaazimiwa kutunza mazingira, Kikwiro anamwambia Sapna:

> Tikitimaji ni kielelezo cha utunzaji wa mazingira.mazingira hayana neno.Isitoshe, nyie ni wageni.Hamjasikia kuwa kilio huanza kwa wafiwa ndipo wa mbali wakaingia? (uk.124).

Maneno haya ya Kikwiro yanadhibitisha ujuhali wa wafanyakazi waliotwikwa majukumu mbalimbali ili kuisongeza mbele Tikitimaji. Ndugu Kikwiro hana habari kwamba mji wa Tikitimaji una uvundo wa ajabu ilhali yeye ndiye anayepaswa kuwa ametambua hali ilivyo na kuanzisha Juhudi za kuusafisha mji. Sapna anapomweleza Kikwiro kuwa kulikuwa na rundo la taka kando ya barabara anasema kuwa yeye ana miaka mingi hajafika eneo hilo na kuwa, ikiwa pana uchafu basi litakuwa tatizo la wazembe waishio eneo hilo.Anasema, "wapo usioweza kuwasaidia kwa lolote.Msiba wa kujitakia hauna kilio na mwiba wa kjichoma hauna uchungu" (uk.125).

Ndugu Kikwiro anawalaumu wakazi wa eneo husika huku akisahau kuwa takataka yenyewe ilikuwa kwenye lango kuu la kuingilia jijini Tikitimaji na kuwa hali hiyo ingewafanya wawekezaji kususia kuwekeza nchini Tikitimaji.Katika hali halisi ya

maisha, mabaraza ya miji ndiyo huwa na jukumu la kuzoa taka mijini na kuitupa mahali inapopaswa kuwa, lakini mara nyingine wakaazi wa miji hii huachiwa uvundo wa taka hiyo hadi inakuwa kero la kawaida.

Haba na haba hujaza kibaba (uk.128), ni usemi mwingine uliotumika katika *Tikitimaji*. Sapna anapofanikiwa kuanzisha kundi la WAZALIMA, linapata wanachama wengi ajabu baada ya muda mfupi tu.Shamsi anawasaidia kuwashawishi vijana wengi ili wajiunge na kundi hili.Hata mama Shamsi anaishia kujiunga nao.Haba na haba ikajaza kibaba.

Juhudi za Sapna zilizaa matunda kwa kasi ya ajabu, kwani kundi hili lilichukua jukumu la kuhakikisha kuwa uhifadhi na utunzaji wa mazingira unazingatiwa.Kundi la WAZALIMA lilienda kuubomoa mlima wa taka ambapo Mzee Jarisa na vijana wengi walichakura kutafuta chochote cha kujiendeshea maisha yao. Mzee Jarisa alilifahamu jaa la Kumbo vizuri sana.Yeye ndiye ile "kata inayoijua siri ya mtungi" (uk.131).Mzee Jarisa alikuwa na umri wa zaidi ya miaka sitini na bado alikuwa anatafuta riziki yake katika hili jaa la Kumbo.Methali hii imetumiwa na mwandishi kutilia nguvu suala la umaskini uliowaelekeza wakazi wa Tikitimaji kwenye jaa la taka.

Sapna na wenzake walipokuwa katika harakati za kumsaidia Shamsi kumtafuta dadake mjini Langulo (Turuturu), walijaribu kufanya urafiki na mwanamke aliyekuwa anauza matunda. Wakawa wanaenda kwake kula matunda na ikatokea kuwa mwanamke huyo alivutiwa na mavazi ya Sapna. Ikawa "maji ya nazi yamepata mvugulio" (uk.140), yaani walikuwa wamejenga urafiki naye na hatimaye akawasimulia visa na vituko vya Turuturu hasa usiku.Anaeleza kuwa kila jioni wasichana wengi ajabu walifurika kwenye barabara ya Bepa-wa-soko iliyopita karibu na alipouzia matunda. Anaendelea kueleza, "huku ile

falsafa ya kitu kilivunja nguu na milima ikalala inatawala (uk.141).Methali hii ina maana kuwa mtu akiwa na pesa (kitu), anaweza kutekeleza mambo mengi hasa yanayokidhi tamaa za kimwili.

Katika hoteli ya Rose Apple, watalii na matajiri walistareheka.Sapna na wenzake waliamua kwenda kwenye hoteli hiyo majira ya jioni ili kumtafuta Sabiya na hatimaye jioni moja walifanikiwa kumpata. Sabiya na wasichana wengine walikuwa wamenasika mjini Turuturu wakifanya biashara ya ukahaba ili kuweza kujikimu.Hivi ndivyo mambo yalivyokuwa Tikitimaji.Watoto wanaopaswa kuwa shuleni wakisoma ndio wanaofanyizwa kazi ya ukahaba na matajiri wenye mali pamoja na watalii wanaouzuru mji wa Turuturu.

Mwandishi ametumia methali kwa ufundi wa hali ya juu ili iweze kuoana vilivyo na ujumbe anaotaka kuuwasilisha hatua kwa hatua katika kazi yake nzima.Ameitumia methali kuiwasilisha dhamira yake kuu pamoja na masuala mengine yanayotokea katika harakati za kuielezea dhamira yake kuu.Methali zilizotumiwa zimemsaidia msanii kuwasilisha mawazo yake kuhusu ujuhali na kutowajibika kwa viongozi, umaskini unaowafanya watu kuchakura kwenye jaa la takataka na udhalimu.

### 3.3 Misemo

Misemo ni vifungu vya maneno ambavyo hutumiwa kwa maana fulani ambayo huenda isiafikiane na maana halisi ya maneno yanayohusishwa kwenye vifungu vyenyewe.Kwa kawaida vifungu hivi huwa na muundo fulani na aghalabu usiobadilika japo maana zenyewe huweza kubadilika au kupanuliwa, (Wamitila 2003:167).

Kwa ufupi, msemo ni fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalumu ili kutoa maana fulani. Maneno haya yanapotumika huipa lugha uzito na mnato zaidi kuliko vile lugha ya moja kwa moja hufanya. Misemo aghalabu huwa ni mafungu mafupi kuliko methali. Misemo inapotumika katika maandishi au masimulizi ya aina yoyote ile huyapa upekee na sura kamili ya kifani.Hadithi iliyotiwa misemo bila shaka itaivutia hadhira zaidi.Misemo pia hutumika kitasfida. Tasfida ni mbinu ya lugha inayotumika kwa lengo la kupunguza makali ya lugha. Makali haya iwapo hayatapunguzwa huweza kusababisha aibu, huzuni au mshtuko ambao ungepunguzwa kwa matumizi ya tasfida.

Mwandishi wa *Tikitimaji* ametumia misemo mingi sana katika hadithi yake.Hebu tuichunguze misemo iliyotumika na ilivyotumiwa.Zinji anasema kuwa aliwaeleza wenzake yote ambayo Mama Rehema alimwambia kuanzia utandu mpaka ukoko.Hii ina maana kuwa, wenzake waliyajua yote yaliyosemwa na Mama Rehema kupitia maelezo ya Zinji. Vijana hawa wote walilelewa katika makao ya Gwadalupe na walikuwa wamefundishwa kupendana na mama yao mlezi.Baadhi ya mambo aliyomwambia Zinji na ambayo amewaeleza wenzake ni kuwa wazidi kupendana kama walivyofundishwa na Mama Rehema.

Maya alikuwa anawasimulia wenzake visa vya kuchekesha na "kuwavunja mbavu" walipokuwa Gwadalupe. Msemo huu unatumika wakati tunakumbushwa enzi za vijana hawa kwenye makao ya Gwadalupe walikolelewa na kusomeshwa na Mama Rehema.Gwadalupe inapotajwa msomaji anajiwa na fikra ya jinsi watoto wanavyotelekezwa katika jamii.Kwa hivyo, msemo huu unatumika katika ile hali ya kuendeleza maudhui ya utelekezaji wa watoto nchini Tikitimaji.

Tunaelezwa kuwa Maya alikuwa anawasimulia wenzake hadithi walipokuwa safarini kuelekea Tiitimaji na hivyo walimtaka aondoke nyuma ili atangulie kwani akiwa nyuma huenda *akawatia ubwete* wenzake na kuwachelewesha katika safari hiyo muhimu. Msimulizi anasema,"Akiwa mbele tutalazimika kuchafuka kuufuatilia uhondo wa utambaji wake.Kwa njia hiyo, kitalifa cha safari hakitakuwa kirefu"(uk.23).

Maya anapotua kabla ya kuendeleza usimulizi wake Sapna anamhimiza aendelee na usimulizi.Maya anapumua kabla ya "kuushika uzi" wake wa utambaji (uk.23). Hii ina maana kuwa Maya aliiendeleza hadithi yake kutoka pale alipoiachia.Kombo anawahimiza wenzake waendelee na safari anapowambia, "Tuichape miguu" (uk.10). Naye Maya anaendelea na hadithi kuhusu jinamizi kubwa ambalo watu waliamini kuwa kila kitu kilitokana nalo.

Kombo anawahimiza wenzake watembee haraka ili waweze kufikia hatima ya safari yao mapema ilivyowezekana.Wenzake wanapoanza kuwa na wasiwasi kutokana na maneno ya Mzee Jududi, anapowauliza nani aliyewashauri kuelekea Tikitimaji, Kombo haonyeshi hofu yoyote ile.Yaelekea tajriba yake kama polisi "ilishaikomaza ngozi yake" (uk.10). "Aliyakodoa macho" yake bila ya kuyakapua (uk.10).Ujasiri huu wa Kombo katika safari ya kudadisi na kugundua matatizo ya Wanatikitimaji uliwatia wenzake tamaa ya kuendelea na safari yenyewe.

Watu wa Durago "wanaangua kicheko" (uk.39), baada ya kuwaelezea watu wa Mzee Jududi kuwa, walikuwa washaununua mlima na tayari mlima ulikuwa wao.Kicheko hiki ni cha dharau kwani kiongozi wa Tikitimaji anauza mlima walimoishi watu kwa miaka mingi bila hata wao kujua.Wanapodhani kuwa wale watu wa Durago wanafanya mzaha,

wanafahamishwa ukweli unaowadhihirikia kwa bumbuazi kuu.Ardhi yao ilikuwa imenyakuliwa na kuuzwa na kiongozi wao, na waliouziwa wanawacheka kwa dharau.

Mazingira ya Tikitimaji yaliharibiwa kiasi kwamba hata nyuki walihama na hatimaye wanatikitimaji "wakakata tama" (uk.45), na kuipasua mizinga yao na kuitumia kama kuni za kuwashia moto.Msemo huu unadhihirisha uharibifu wa mazingira ulivyokuwa na athari kubwa kwa wakazi wa Tikitimaji.

Mama Shamsi anawambia kina Zinji kuwa mambo ya Tikitimaji "watayaweka kiporo" (uk.45), wanapomtaka awasimulie kuhusu kwa nini Tikitimaji huitwa hivyo. Anamaanisha kwamba, angewasimulia habari ya Tikitimaji baadaye.Mama Shamsi anasema kuwa haoni ugeni wowote kwa kina Zinji ambao walikuwa wageni wake.Zinji anasema, Kila mamake Shamsi anapotuchunguza haoni chochote kinachomfanya aamini kuwa sisi ni wageni.Sisi na wenyeji ni "riale kwa ya pili" (uk.69). Maneno haya yanatuelekeza kufahamu kuwa, hawa wote walikuwa wanatikimaji waliopaswa kusafiri pamoja katika safari ya kujisaka ili waweze kujijua na hatimaye kusuluhisha matatizo yaliyoikumba nchi yao.

Zinji anamweleza Mamake Shamsi kuwa Mama Rehema ndiye "aliyewashika mikono" (uk.70), kwenye njia ya maisha.Mama Rehema ndiye aliyewalea, kuwasomesha na kuwafundisha mengi yaliyohusu maisha. Mama Rehema pia ndiye aliyewaelekeza katika safari ya Tikitimaji ambapo wanaelekea ili kujisaka na kujijua, na hasa kuyaelewa matatizo ya nchi yao ili waweze kuchangia katika utatuzi wake.

Zinji alimwonea gere Sapna aliyelala usingizi wa pono usiku ule walipolala kwa mama Shamsi (uk.76).Yeye hakupata lepe la usingizi na alibakia "kukodoa macho" kwenye

giza tupu na kusikiliza kereng'ende na sauti nyingine za usiku (uk.76).Huenda Zinji alikosa usingizi kutokana na hamu ya kutaka kumwona Ami mdogo aliyempokonya urithi wake.Safari hii ilikuwa muhimu kwake zaidi ya ilivyokuwa kwa wenzake.Vijana hawa wanapokaribia mji wa Tikitimaji, Sapna anahisi harufu mbaya kabla ya wengine.Kwa kuwa Maya hakuhisi harufu hiyo, Sapna anakumbuka jinsi walivyozoea kumkejeli Maya walipokuwa Gwadalupe kuwa pua yake ilikuwa "imekufa ganzi" (uk.87), na kuwa haikufanya kazi.Harufu inayotokea upande wa mji ni sawa na ya mnyama aliyekufa.Uchafuzi wa mazingira umekithiri mno.

Mwandishi ametumia msemo, "kutia kitumbua mchanga" ( uk.123).Sapna anapomweleza Kikwiro kuwa anataka kuanzisha vuguvugu la kulinda mazingira, anashtuka na kuuliza kama hicho kilikuwa chama cha kisiasa na hatimaye anamuuliza Sapna, "unataka kunitilia kitumbua changu mchanga wewe?" Neno vuguvugu linapotamkwa linamtia wasiwasi mwingi Ndugu Kikwiro kwa sababu wanaharakati wengi walikuwa wamejitokeza kupambana na uongozi mbaya Tikitimaji.Kwa hivyo, utawala ulikuwa macho sana kuhusu vuguvugu lolote nchini Tikitimaji. Maneno ya Kikwiro yanadhihirisha kuwa utawala wa Tikitimaji haukukubali vuguvugu lolote la kisiasa lililojitokeza kukabiliana na maovu yaliyosambaa nchini humo.

Msemo "kula mwande" umetumika wakati Sapna na Shamsi wanamtafuta Sabiya mjini Turuturu alikopotelea.Msimulizi anasema, "siku ya kwanza hatukufaulu, ikawa mjango".Ya pili "tukala mwande".Siku ya tatu ndipo "tulipofaulu" (uk.141).Msemo huu umetumika kuonyesha juhudi zilizofanywa na vijana hawa kumtafuta mwenzao hadi wanapofaulu kumpata.Wanafanya hivi ili kuweza kumwokoa kutoka danguroni alikopotelea Sabiya pamoja na wenzake wengine.

Shamsi anapomtambua dadake kati ya wasichana waliokuwa wanaletwa kwa gari na mwanamume fulani wakielekezwa hotelini Rose Apple, naye Zinji anapotaka kuchukua picha ya vituko hivyo, mwanamume yule anatambua mwangaza wa kamera na kutoroka akiwaacha wasichana aliokuwa nao wakijikunyata kwenye baridi ya usiku.Msimulizi anasema, "wasichana wawili watatu ambao walishtuliwa na kitendo chake cha ghafla bin vuu, wakawa wanajitahidi kumkimbilia lakini gari lake likayoyomea nyuma ya majengo yaliyokuwa upande huo.

Haya ndiyo matatizo wanayokumbana nayo wasichana waendao kutafuta kazi ili waweze kukidhi mahitaji yao na ndiyo baadhi ya matukio waliyoyagundua Sapna, Maya, Zinji na Kombo.Sapna na wenzake wanawachukua watoto hawa na kuwapeleka kwenye makao ya Gwadalupe.

Misemo yote iliyotumiwa na mwandishi katika kazi yake inafaa katika kila muktadha wa matumizi na inawiana barabara na ujumbe unaowasilishwa.Uwiano huu unachangia kuitia mnato na mvuto kazi yenyewe kwa hadhira ya mwandishi.

### 3.4 Tashihisi

Kwa mujibu wa Mohammed (1995:127), tashihisi ni mbinu ya uhusisho na ulinganisho inayotokana na haja ya mwanadamu ya kuvihuisha vitu visivyo na uhai.Hiki kitu kisicho na uhai au kisicho na sifa za kibinadamu, hupewa sifa, tabia au matendo ya kiuhai na kibinadamu.Maelezo haya ya Mohammed yanashabihiana na ya Wamitila (2003:223) kuwa tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai huwasilishwa au kusawiriwa kwa namna iliyo sawa na binadamu na kuweza kufikiri na kuhisi.

Mbinu hii ina umuhimu wa kuvitia nguvu na harakati vitu ambavyo kwa kawaida ni vitulivu na kwa kuvitia uhai vitu hivyo, mwanadamu anavifanya vionekane katika mwendo na vitendo mbalimbali, na katika hali hiyo, tashihisi inaweka wazi zaidi maana na kuimarisha usanii unaotakikana katika kazi ya kifasihi (Mohammed: 1995:27).Tamathali hii, kwa hivyo, ina uwezo mkubwa wa kuigusa hisia ya msikilizaji au msomaji wa kazi ya kifasihi. Mwandishi wa *Tikitimaji* ametumia tashihisi mara kadha katika kazi yake ili kumwezesha msomaji kuathirika ipasavyo kihisia kutokana na ujumbe unaowasilishwa.Mwandishi anatumia tashihisi ifuatayo kueleza hali ya hewa ya Gwadalupe:

> Tulikaribishwa Gwadalupe na ule ubaridi unaosababishwa na miti mingi iliyopazunguka.Ile miti mirefu iliyokuwa ikicheza huku na huku kutokana na upepo mwanana ilitupiga pambaja kubwa (uk.5).

Mwandishi ametumia maneno haya kuhuisha baridi, miti na upepo ili kuweza kuisawiri picha ya uzuri wa mahali ambapo miti haikuwa imefyekwa ishara ya mahali palipo na mazingira yaliyohifadhiwa.Msomaji yeyote anayesoma sehemu hii ya kazi yake anafurahia mazingira kama haya na kuyatamani.Kwa hivyo, mtunzi anadhamiria kumshawishi msomaji awe na juhudi za kuhifadhi mazingira ili aweze kuyafurahia.

Mwandishi ametumia tashihisi tena kuonyesha athari za uharibifu wa mazingira ambayo ndio hasa dhamira yake.Zinji, Sapna, Maya na Kombo wanapofika Ganjoni wakielekea Tikitimaji, msimulizi anaeleza hali ya hewa ilivyokuwa mahali hapa kwa kusema:

> Hewa hapa ilikuwa tofauti sana na hewa tuliyoizoea.Ilikuwa na joto fulani. Unyevunyevu wa eneo hili ulikuwa wa juu. Hapa na pale upepo ulijaribu kuyazoa majani ambayo yalikatalia chini kuisusia safari hiyo ya lazima (uk.17).

Maneno haya yanaisawiri picha ya hali ya hewa ilivyokuwa Ganjoni ambapo upepo ulikuwa mwingi kutokana na ukosefu wa miti ya kuukinga upepo wenyewe.Bila ya shaka, hali hii inatokana na uharibifu wa mazingira.Ili kuweza kudhihirisha athari zaidi za uharibifu wa mazingira mwandishi anasema maneno yafuatayo kupitia kinywa cha msimulizi wake:

> Tulitembea na hatimaye tukatokeza sehemu ya chini kabisa. Palikuwa na mto.Kutokana na maneno ya Mama Rehema lazima huu ndio Mto Unasi.Mto huo haukuwa na maji mengi. Palikuwa na maji kidogo kwenye sehemu ya katikati ya mto.Majabali makubwa yaliyolala kwenye sakafu ya mto wenyewe yalidhihirika waziwazi. Mawili matatu yana mabakamabaka hapa na pale athari za miaka zilizoachwa na maji (uk.24).

Mbinu hii inatumika katika sehemu hii ya hadithi ili kuweza kuonyesha jinsi mto Unasi ulivyoathirika na uharibifu wa mazingira. Maji siku hizi ni machache mno mtoni na hayawezi tena kuyafunika majabali yanayorejelewa na ambayo zamani yalifunikwa na maji ya mto Unasi. Ukubwa wa majabali yenyewe unadhihirisha kimo cha maji kilivyokuwa juu zamani ambapo maji hayo yaliweza kuyafunika majabali hayo makubwa.Maji hayo yanaisha na mto Unasi unakaribia kukauka.Jambo hili ndilo Msanii anasisitiza kwa kutumia tamathali hii ya usemi anapouisha majabali yaliyo katika Mto Unasi kwa kusema kuwa yalikuwa yamelala.

Msimulizi anazidi kusimulia jinsi miti ilivyopungua kadri walivyoendelea na safari yao. "Jua ambalo lilikuwa linainama Magharibi lilitokeza jicho lake kubwa" (uk.43).Miali yake ilikuwa na joto ambalo halikuwa la kawaida.Hali ya joto Tikitimaji inawaumiza wakazi wake hata majira ya jioni ambapo kunapaswa kuwa na baridi baridi.Matatizo haya yanatokana na Wanatikitimaji wenyewe kwa sababu ya kuharibu mazingira. Mwandishi anasisitiza suala hili kwa kutumia tashihisi ili kudhihirisha hatari zinazomkabili binadamu anayezidi kuyaharibu na kuyachafua mazingira yanayomhifadhi.

Mzee Jududi anaeleza kuwa hali ya uharibifu wa mazingira ilipozidi hata nyuki walianza kuyaepuka mazingira haya."Mizinga yao iliyokuwa imeangikwa mitini ikabakia kwenda miayo kwa kuwakosa nyuki wenyewe" (uk.45).Anaeleza kuwa nyuki ni wadogo lakini hata wao wana akili zao za kuyaona matendo yao.Mizinga kwenda miayo ni tamathali inayotumika kusisitiza jinsi nyuki walivyohama na kuwaacha Warinaji asali bila tegemeo kwani walikosa asali na hatimaye wakaipasua mizinga yenyewe na kuitumia kama kuni. Uharibifu wa mazingira unawaathiri hata wadudu wanaotumiwa kama kitega uchumi na binadamu mwenyewe. Mwandishi anataka binadamu apate funzo kutokana na matendo yake yanayochangia uharibifu wa mazingira na kutafakari jinsi anavyoweza kuzuia hali hii.

Kwa kuhitimisha sehemu hii ya matumizi ya tashihisi, tumeweza kuona kwamba msanii ameteua tamathali hii na kuitumia kwa njia mwafaka, ili kumwezesha kuwasilisha suala la uharibifu wa mazingira kwa njia ambayo inaziathiri hisia za msomaji.Msomaji anabaki kuyatafakari mambo aliyoyasoma, hali inayomfanya kuchukia uharibifu wa mazingira na kuhisi kwamba yeye pia anapaswa kuwa miongoni mwa wale wanaojitokeza kuyahifadhi mazingira badala ya kuyaharibu.

### 3.5 Nidaa

Kulingana na Wamitila (2008:406), nidaa ni matumizi ya siyahi au maneno ya hisia.Hii ni mbinu ambayo kimsingi inachangia katika kujenga kazi za kifasihi, kwa kuweka wazi hisia kama vile za huzuni, masikitiko, mshangao na nyinginezo katika uwasilishaji wa mawazo ya mwanfasihi, kutegemea kile anachotaka kuwasilisha katika hatua fulani ya kazi yake.Mwandishi wa *Tikitimaji* ametumia mbinu hii katika sehemu mbalimbali kila anapokusudia kuwasilisha hisia fulani kupitia kwa wahusika wake.Kwa mfano, Mama Rehema anamwambia Zinji, "Tikitimaji kuna siri uliyoitaka tangu zamani!" (uk.10). Baadaye Mama Rehema anampa Zinji kibahasha kidogo na kumwambia:

> Usikifungue! Utakifungua tu patakapokuwa na dharura ya kufanya hivyo! Huhitaji kuambiwa ni lini, utajua tu! ... Sasa una kifua cha kuujua ukweli! (uk.10).

Mama Rehema anayasema maneno haya kwa utaratibu unaomtia Zinji mshawasha wa kutaka kujua upesi siri iliyofichama Tikitimaji kumhusu yeye.

Katika hali ya kuwaaga Zinji, Sapna, Maya na Kombo wanapoelekea Tikitimaji, Mama Rehema anawambia, "Msiwe na hofu ya kuliogopa chaka kwa kuona limeshikamana mno! Kumbuka kituo kinaitwa Ganjoni! Msipite hapo msije mkaishia Langulo! (uk.10). Mama Rehema anawahimiza kuwa wasije wakapotoka kama walivyo watu wengi Tikitimaji.Ila wakazane katika kugundua maovu yaliyopo na kung'ang'ana kuyarekebisha.Mama Rehema anahisi kwamba safari yenyewe ni ngumu lakini inawezekana. Matatizo mengi yanaikumba Tikitimaji ukiwemo udhalimu, uchafuzi wa

mazingira, umaskini na mengine mengi ambayo yanapaswa kusuluhishwa kwa juhudi za wanatikitimaji wote, wazee kwa vijana.

Mzee Jududi anadhihirisha hisia za mshangao anapoeleza jinsi wageni walifika Tikitimaji wakauziwa ardhi yao bila wao kujua. Anasema:

> Basi siku moja wakafika watu... Basi tukaimba, kongoni mgeni! Kongoni mgeni! Lakini baadaye wakasema, hii ni karatasi inayoonyesha kuwa wao walikuwa wanaumiliki mlima! Wao ndio wanaoumiliki mlima wa Tirimacho! ...sikumbuki vizuri kama walisema kama kuna mtu au kundi la watu lililowauzia mlima wenyewe.Muhimu ni kwamba, wameununua tayari! Kwa hiyo sisi na mizinga yetu tumeuzwa! (uk.38).

Maneno haya ya Jududi yanasikitisha sana.Ni udhalimu ulioje huu.Ni maneno yanayoibusha hisia za huruma kwa msomaji na pia chuki kwa viongozi walioutekeleza udhalimu huu.Kwa njia hii, mwandishi ametimiza lengo lake la kumwathiri msomaji kihisia, jambo linalomfanya kuelewa na kuhisi hali ilivyokuwa kwa Wanatikitimaji.

Mzee Jududi anapowaelezea kina Zinji habari kuhusu uharibifu wa mazingira anawambia kuwa miti ilikatwa kwa madai kuwa mingine ingepandwa lakini haikupandwa.Anapoulizwa kama miti ilipandwa anasema:

> Ipandwe na nani huku? Wale waliipukuta miti yote na kuliacha eneo hili kama unavyoliona!...umekuwa upara mkubwa wa maumbile.Mvua, labda kwa kuchukia matendo tule kama haya ikawa hainyeshi! (uk.45).

Mbinu hii imetumiwa sana ili kunasa hisia za msomaji kwa kumfanya achukie jinsi mambo yalivyoendeshwa Tikitimaji na pia ahisi kutoa mchango wake kuzuia hali kama hii isitokee katika mazingira yake.

Vijana wanaoelekea Tikitimaji wanaelezwa na Mzee Jududi kuwa Tikitimaji ilikuwa kila mahali.Anasema,"Tikitimaji iko kila mahali kwa kweli! Kote labda hata huko mtokako!"(uk.54).

Maneno haya yanawashtua vijana hawa wanaoachwa katika bumbuwazi kuu.Hata hivyo, Mzee Jududi anahisi kwamba kila mahali kuna uozo unaohitajika kuondolewa katika jamii nyingi ulimwenguni.

Mzee Jududi anawaonya kina Zinji dhidi ya tamaa inayowaingia wengi pindi waingiapo mamlakani.Anawambia: "kumbukeni msitekwe na hila na hadaa mkasahau kilichowaleta huku... muhimu zaidi kumbukeni muwe wajanja msikumbwe na maradhi ya Tikitimaji! Kauli hii ya Mzee Jududi ina maana kuwa, wanaharakati wengi wa ukombozi wanapofaulu kuung'oa uongozi mbaya, wao pia huchukua hatamu za uongozi na kuingiwa na tamaa ile ile ya watangulizi wao. Mzee Jududi ana hofu kuwa, vijana hawa huenda wakaingiwa na tamaa hii baada ya kufanikiwa katika safari yao ya Tikitimaji.

Shamsi anapokuwa na hisia za woga na kumtoroka Kombo, Sapna anasema, "Kombo, kijana amekuona akajua kiyama kimefika! Shamsi, usimwogope Kombo! Hana neno! Huyu ni rafiki tu!" (uk.64).Sapna anashangazwa na jinsi Shamsi alivyotimua mbio baada ya kushuku kuwa Kombo alikuwa askari.Woga wa Shamsi unadhihirisha jinsi askari walivyokuwa watu wa kuogofya badala ya kuwa ishara ya utulivu na amani nchini Tikitimaji.Hawakuwa wanawatumikia watu wa kawaida bali watu waliokuwa na

mali.Haya ni matumizi mabaya ya vyombo vya dola yanayotekelezwa na viongozi madhalimu katika jamii nyingi ulimwenguni. Viongozi walio na tabia hii hawana budi kung'atuliwa mamlakani.

Katika jimbo la Tikitimaji, hata masomo yaliyofundishwa kuhusu visa vya udhalimu vilivyowahi kutokea Tikitimaji yalipigwa marafuku.Kisa kuhusu jitikiti lililogeuka jitu na kuwameza watu wote kijijini hakisimuliwi tena Tikitimaji tangu Master Sticker alipochukua uongozi wa jimbo.Alikataza kisa hicho kisifundishwe shuleni! (uk.70).

Maneno haya yanazidi kuelezea dhuluma ilivyoendelezwa ambapo masomo kama vile historia yalipigwa marufuku na walimu walioyafundisha wakapoteza kazi.Vile vile watu waliozungumza dhidi ya udhalimu walifurushwa kutoka Tikitimaji.

Katika hali halisi ya maisha, hasa katika bara la Afrika na kwingineko ulimwenguni, watu wanaoikosoa serikali au hata waandishi wa fasihi inayoikosoa serikali wanateswa na wengine kutorokea Ughaibuni kwa kutishiwa maisha yao.Utawala wowote wa kidhalimu haupendi kukosolewa na hujitahidi kwa hali na mali ili kubakia mamlakani milele.

Wanatikitimaji walimdhihaki kijana aliyeliona tikitimaji lililojigeuza na kuwa jitu kubwa wakimwambia: "Tikitimaji tu! Unaogopa tikitimaji tu! Mbona wewe ni mwoga kiasi hiki!" (uk.74).

Wanakijiji walifanya mzaha bila kujua hatari iliyowasubiri.Maneno yao yanadhihirisha jinsi walivyofanyia mzaha hata mambo yaliyohatarisha maisha yao.Wanatikitimaji waliyapuuza mambo muhimu yaliyohusiana na uhai wao na hatimaye wakaja kudhurika kutokana na mapuuza yao kwani jitu lililotokea liliwameza wote na kuwaangamiza.

Hisia za mshangao zinawakumba Maya, Kombo na Zinji wanaposimuliwa kisa kuhusu muuzaji njugu karanga aliyezirashia njugu hizo madini ya risasi ili ziwavutie wanunuzi.Sapna na Saki wanapozipeleka njugu zenyewe katika maabara ya serikali zifanyiwe uchunguzi wanashangazwa na matokeo. Zilikuwa na chembechembe za risasi! (uk.90).Matokeo haya pia yanamwacha msomaji amepigwa na bumbuwazi. Haiyumkiniki kwamba, mtu anaweza kufanya mambo kama haya ilhali anafahamu fika madhara ya risasi mwilini mwa binadamu.Hii ni tamaa na ubinafsi uliokithiri.Ingawa wanyonge wanailaumu serikali mara nyingi, ni jukumu lao pia kugundua kuwa tamaa yao, hasa katika biashara inawadhuru wenzao na umma kwa jumla na hivyo wanapaswa kujirekebisha.

Mzee Dhamiri ambaye ni kipofu, anawaambia kina Zinji ifuatavyo wanapomkaribia wakidhani kuwa hakuwa anawaona: "Nawaona tu! Msidhani mtafanya alivyonifanyia Jitikiti! (uk.94).Maneno haya ya mzee Dhamiri yamejaa chuki ya kumbukumbu kuhusu kufurushwa kwake na kiongozi wa Tikitimaji.Hata Zinji, Maya, Sapna na Kombo wanashangaa baadaye, wanapomuuliza kama anamfahamu Ami mdogo ambaye ni kiongozi wa Tikitimaji. Mzee Dhamiri anacheka kicheko cha dhihaka anapotambua kuwa vijana hawa wanamfahamu Jikitiki kama Ndugu Stika Bepa-wa-soko, au Ami Mdogo. "Ahh! Ahh! Ahh!" Anacheka kwa sauti ya juu. Anatulia kabla ya kuendelea,"Ahh! Ahh! Ahh! Ndugu Stikilali....Tulimwita hivyo zamani wakati alipoongozwa na falsafa ya udugu".Kicheko hiki kinamdhihaki Jitikiti ambaye tayari amebadilika na kuwa kiongozi dhalimu.

Mwishomwishoni mwa riwaya, Zinji anafanikiwa kufika kwa Ami Mdogo lakini hauoni uso wa Ami yake huyo, ila anaisikia sauti yake tu.Zinji anamwambia bila kumuona,

"ulininyima nafasi ya kukulia iliko jamaa yangu! Umewanyang'anya watu ardhi yao umuuzie Durago!" Ami mdogo naye anamjibu kuwa hakujua kuwa mwanamke alipaswa kurithi mali. Anasema,"mwanangu, niliamini kuwa mwanamke hawezi kurithi.Nimetambua kosa langu! Siku hizi naugua!". "ugonjwa wako una tiba lakini!" Zinji anamwambia."Hamna! Hamna!". "Ipo! Kaoge mtoni Unasi. Yavue maguo yako Ami Mdogo kisha kaoge mtoni!"Zinji anamwambia. "siwezi! siwezi kuoga mtoni.Huko ni kujifedhehesha mwanangu! siwezi! siwezi!"(uk.153).

Matumizi ya nidaa katika sehemu hii yanamfanya msomaji aone hisia za majuto za Jitikiti anapogundua makosa yake.Zinji anang'ang'ana kumwona Ami mdogo lakini anatoweka baada ya kukataa kuuzingatia ushauri wa Zinji ili kuweza kuboresha uongozi wake. Anaona kwamba kubadilisha mienendo yake mibaya ni kujifedhehesha mbele ya umma.Kutobadilika kwa Jitikiti kunasababisha kuendelezwa kwa udhalimu na maovu mengine yanayodhihirika Tikitimaji. Ni wajibu wa wanatikitimaji kumwondoa hata kwa nguvu ikibidi kwani madhila anayowasababishia hayawezi kuzoeleka kamwe.

Mwandishi ametumia mbinu ya nidaa kwa ustadi mkubwa ili kuitia kazi yake mvuto na mnato katika harakati zake za kuwasilisha malengo yake kwa hadhira lengwa. Kwa kutumia mbinu hii na nyinginezo, mwandishi wa *Tikitimaji* amefaulu kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira yake na kuiathiri kwa njia mwafaka kabisa.

### 3.6 Kuchanganya Ndimi

Hii ni hali ya kutumia zaidi ya lugha moja katika mazungumzo au maandishi ambapo mzungumzaji au mwandishi anatumia maneno kutoka lugha tofauti katika sentensi moja.

Wandishi hutumia mbinu hii kufidia uhaba wa msamiati kutoka lugha inayotumika kuandikia au kusisitiza jambo fulani.

Mwandishi wa Tikitimaji amechanganya ndimi anapotumia maneno katika lugha ya Kihindi na Kingereza.Mwandishi ametumia neno la Kihindi Satyagraha (uk.46) likimaanisha maandamano.Neno hili limetumika ili kusisitiza juhudi nyingi zilizofanywa ili kuyalinda mazingira katika Tikitimaji na vilevile kuangazia maudhui ya ukombozi kwani masuala yanayoangaziwa Tikitimaji ndiyo yaliyoikumba India katika enzi ya Mahatma Gandhi.Sapna ambaye ni mwanamazingira aliongoza *satyagraha* nyingi katika Tikitimaji akiwataka wanaohusika na utunzaji na usafi wa mazingira wakome kukata miti na kuchafua mito.

Inadhihirika kwamba viongozi wanachangiauchafuzi wa mito kwani Ndugu Kikwiro anapendekeza uchafu ukatupwe mtoni.Mwandishi anaeleza kupitia kwa Maya kuwa maandamano mengi yalifanywa kuupinga uharibifu wa mazingira Tikitimaji.

Mwandishi anatumia maneno katika lugha ya Kingereza anapotaka kusisitiza kuwa enzi ya utumwa ilikuwa ya zamani sana lakini matendo ya kiutumwa bado yamo miongoni mwa Wanatikitimaji.Maya anauliza, "Hivi, cha zamani ni enzi yenyewe au matendo yenyewe?" (UK.59).Anauliza swali hili baada ya Kombo kusema kuwa enzi ya utumwa ilikuwa ya zamani sana.Vijana hawa wanazungumzia biashara ya watumwa wanapopiti kwenye njia iliyotumiwa na wafanyabiashara waliohusika na uuzaji wa watumwa. Njia hii inawakumbusha maneno ya Mama Rehema zamani ambapo alisema kuwa jambo moja huweza kuwa mambo mengi kutegemea mtazamo.Maya anasema kuwa, alidhani

kuwa ndicho walichomaanisha wazungu waliposema kuwa. “Beauty lies in the eyes of the beholder” (UK.59).

Katika hali halisi ya maisha watu huyaona mambo kwa mitazamo tofauti.Kuna wale ambao wataiona njia iliyotumiwa na watumwa kama iliyotumika kutenda mambo ya zamani sana lakini kuna wengine wataona kwamba matendo haya ya zamani bado yanadhihirika miongoni mwa wanajamii.

Dhulama bado ipo Tikitimaji ambapo viongozi wanawadhulumu wakazi wake.Mzee Jududi na watu wake walipokonywa ardhi yao na Jitikiti na akaiuza. Kuna watu watakaochukulia dhuluma kama jambo la kawaida ilhali wengine wataliangalia kwa jicho la udadisi na kuchukua hatua ya kuizungumzia na hatimaye kutafuta suluhisho.

Anaposisitiza umuhimu wa kufanya mazoezi, mwandishi anatumia maneno couch potato (uk.63).Sapna humshauri Maya kila wakati kuwa, asikae akisoma tu bali ajizoeze kufanya mazoezi.Anamwambia: “Maya, wajua wewe unakaa sana ukisomasoma.Mwili unatakiwa kufanyishwa mazoezi.Usiwe wanachokiita watu couch potato” (uk.63).

Sapna anamwambia Maya maneno haya kwa kuwa Maya hakuwa anaziweza mbio.Anamshauri kuwa akiendelea kusoma tu bila kufanya mazoezi atazembea hata zaidi.Mwandishi anaangazia umuhimu wa mazoezi kwa wanajamii wote.Yaani watu wayape mazoezi nafasi yake katika mipango ya kazi zao za kila siku.

Safari ya Tikitimaji ilikuwa ngumu kwani kulikuwa na matatizo mengi yaliyotokana na viongozi kuwanyanyasa wananchi wa kawaida.Baada ya kushauriwa na mamake Shamsi kuwa wawe waangalifu katika safari yao, Zinji, Sapna, Maya na Kombo wanaingiwa na hofu fulani kuhusu Tikitimaji.Anapoongeza kuwa Shamsi angewafuata huko kumtafuta

dadake aliyepotelea huko, wanajawa na hofu zaidi.Wanawaza: "Tikitimaji hapakuwa tu pahali pa kutisha bali pia mahali pa kupotelea" ( uk.78). Sapna anaposema kuwa ana shaka na safari ya Tikitimaji, Maya anaongeza na kusema, "hata mimi nina hisia fulani…*some gut feeling*…Lakini inanitia mshawasha zaidi (uk78).Maneno haya ya Kingereza yanatumika kusisitiza kuwa safari yenyewe haikuwa rahisi. Iliwatia vijana hawa hofu kwani kupigana na uongozi mbaya si kazi rahisi.Tunaelezwa kuwa viongozi walipokosolewa waling'ata vikali.Mzee Jududi na wengine waling'atwa kwa kufurushwa Tikitimaji baada ya kumkosoa Jitikiti.

Maneno amusement park (uk.83) yametumiwa kuonyesha sehemu za burudani zilizokuwa zimejengwa huko Langulo, walikopotelea watu wengi waliopenda kuponda raha wakiwemo watalii.Langulo ndiko walikopotelea wasichana wengi kama vile Sabiya na wengine aliokuwa nao wakishiriki ukahaba.Mwandishi anatumia maneno amusement park kuashiria kuwa, sehemu za burudani zimejengwa Tikitimaji na jinsi zinavyotumika katika ukiukaji wa haki za watoto. watoto wengi wa kike na wa kiume wanapatikana wakiwa wamefungiwa katika majumba.Hata hivyo, watoto hawa wanaokolewa na kina Sapna na kupelekwa katika makao ya watoto ya Gwadalupe.

Neno anti-oxidant (uk.140), limetumika kumaanisha hali ya kuondoa uchafu mwilini.Sapna anasema kuwa juisi ya tikitimaji ikichanganywa na tufaha na matunda mengine ambayo hakuyakumbuka, huwa ni mchanganyiko mzuri sana wa kuondoa uchafu mwilini yaani ni *anti-oxidant* nzuri sana.

Msanii ametumia maneno haya ya Kingereza kusisitiza umuhimu wa tunda la tikitimaji na pia kufidia msamiati wa kisayansi ambao lugha ya Kiswahili ina uhaba kwayo.Zaidi

ya haya, anataka kuonyesha kuwa wanatikitimaji waliacha kupanda matikitimaji kwa kuwa yalihusishwa na Jitikiti ambaye ni kiongozi dhalimu.

Zinji na wenzake wanapozungumzia umuhimu wa tikitimaji na kushangaa kama Wanatikitimaji wanalielewa jambo hilo, Sapna anaongeza na kusema kuwa alipochakura katika mtandao alipata kuwa tikitimaji lina faida nyingi kama vile kupambana na kensa ya ziwa. Mwandishi anapotumia maneno ya Kingereza, anasisitiza umuhimu wa matunda mbalimbali na kwa nini miti ya matunda inapaswa kutunzwa badala ya kususiwa kupandwa katika Tikitimaji.

## 3.7 Sitiari

Kulingana na Kuvuna na Wengine (1992:27), sitiari ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu viwili ambavyo kwa asili ni tofauti kitabia kwa kufuatisha sifa fulani iliyo katika vyote viwili bila kuitaja sifa yenyewe.Maelezo haya yanalingana na yale ya Wamitila (2008:421), anayesema kuwa sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi usiotumia, vilinganishi 'kama', 'mithili ya', 'mfano wa' n.k.

Katika *Tikitimaji*, mwandishi ametumia tamathali hii ya lugha kutoa ulinganisho wa aina mbalimbali, ili kuweza kusisitiza ujumbe katika kazi yake.Mwandishi ametumia sitiari ya *kurunzi* (uk.1). Msimulizi anaeleza kuwa sauti ya Mama Rehema ilikuwa kurunzi iliyoiangaza njia yao kwenye safari ya kuelekea Tikitimaji. Kurunzi inalinganishwa na maneno ya busara na ushauri ya Mama Rehema kwa vijana wanne waonafunga safari kuelekea Tikitimaji.Mama Rehema anawashauri kuwa wasije wakatengana wala kusongwa na tamaa ya kujitakia makuu.Ushauri huu unalinganishwa na kurunzi inayotoa

mwangaza ili mtu aweze kuona anakokwenda.Vivi hivi, utangamano na ushirikiano wa vijana hawa ungewaongoza katika safari hii ngumu na muhimu.

Mapenzi waliyoyapata vijana hawa kutokana na mafunzo ya Mama Rehema katika makao ya Gwadalupe yanalinganishwa na gundi inavyounganisha vitu pamoja.Msimulizi anasema, "gundi ya mapenzi hayo ilitugandamanisha pamoja.Hakuna kitu chochote kilichoweza kutubagua wala kutumamanua" (uk.1).Ni vigumu sana kuwatenganisha Zinji, Sapna, Maya na Kombo kwa kupanda mbegu ya chuki baina yao.Mapenzi yalikuwa kama gundi iliyowashikamanisha pamoja.

Maneno ya Mama Rehema kwa Zinji yanalinganishwa na sumaku kwa kuwa yalimvuta Zinji upande wa Mama Rehema kama sumaku ivutavyo vitu vya chuma upande wake. Mama Rehema anapomwambia Zinji kuwa aende Gwadalupe ili amweleze jambo fulani, Zinji anasema kuwa maneno hayo ya Mama Rehema *yalikuwa na uwezo wa sumaku* (uk.3).Zinji alikuwa na hamu ya kujua Mama Rehema alikuwa na ujumbe upi kwake.

Msimulizi anaeleza jinsi jini la wakati lilivyokuwa limeifyonza mikono ya Mama Rehema utomvu wa siha aliyokuwa nayo zamani (uk.6).Wakati unalinganishwa na jini ambalo huhusishwa na mambo maovu.Zinji anakumbuka jinsi Mama Rehema alivyowabeba juu zamani lakini siku hizi hawezi kufanya hivyo kwa sababu ya uzee.

Akili ya Mama Rehema inalinganishwa na ukali wa wembe. Ingawa Mama Rehema alikuwa amezeeka, bado alikuwa na uwezo wa kukumbuka mambo yaliyotendeka zamani.Alikuwa anakumbuka maswali mengi ambayo Zinji alikuwa anamuuliza kuhusu asili yake, yaani asili ya Zinji.Wembe ulivyo na ukali wa kukata, ndivyo pia akili ya

Mama Rehema ilivyokuwa na ukali wa kukumbuka mambo ingawa alikuwa mama aliyezeeka.

Mzee Jududi anapozungumzia uharibifu wa mazingira anasema kuwa watu wenyewe waligeuka mchwa (uk.44) na kuivamia miti.Anazidi kusema kuwa hata mchwa ni afadhali kwani hawali miti na kuimaliza.Watu ambao ni waharibifu wa miti hata zaidi ya mchwa wanalinganishwa na huo mchwa ingawa Jududi anatambua kuwa watu ndio huharibu mazingira hata zaidi ya mchwa. Anaichora taswira hii ili kuonyesha kiwango cha uharibifu wa mazingira kilivyokuwa kimezidi.Mzee Jududi akizidi kuelezea kukithiri kwa uharibifu wa mazingira anasema kuwa miti yote ya asili ilikuwa imemalizwa na eneo kubwa la Tikitimaji lilibaki kuwa *upara mkubwa wa maumbile* (uk.44) Eneo lililoachwa bila miti linalinganishwa na kichwa ambacho hakina unywele hata mmoja.

Kwa kutumia tamathali hii ya lugha, mwandishi amefaulu kuitia kazi yake mvuto na mnato huku akipania kuendeleza maudhui kwa njia inayomnasa msomaji kutaka kuendelea kusoma kazi yake na kuyapata zaidi yaliyomo pamoja na kuyatafakari kwa kina.

### 3.8 Takriri

Takriri ni urudiaji wa sauti, neno au sentensi katika matini au kazi fulani. Takriri hutumiwa katika fasihi ili kusisitiza jambo fulani.

Katika *Tikitimaji*, mwandishi ametumia takriri kusisitiza maudhui fulani fulani inapobidi ili kuyaweka wazi zaidi kwa wasomaji wake.Anapotaka kusisitiza umoja na mapenzi yaliyokuzwa miongoni mwa watoto waliokulia makaoni Gwadalupe, mtunzi anasema

maneno haya kupitia kwa mhusika Zinji: "tulikuwa *watoto* wa Gwadalupe.*Watoto* wa Mama Rehema.Isitoshe tulikuwa marafiki wa kufa kuzikana (uk.4).

Kutokana na maneno haya, inadhihirika kwamba watoto waliolelewa katika makao ya watoto ya Gwadalupe walifunzwa kupendana na kuwa marafiki wa kuaminiana ingawa mfumo wa kisiasa wa Tikitimaji ulikuwa na uozo mwingi.Urafiki na uaminifu waliokuwa nao Zinji, Sapna, Maya na Kombo, na ambao walijifunza kuwa nao kupitia kwa Mama Rehema, ndio unaowawezesha kutimiza mipango yao katika safari ya Tikitimaji.

Umoja huu uliwawezesha kuunda kikundi cha WAZALIMA ambacho kiliwezesha uhifadhi na usafi wa mazingira Tikitimaji. Waliweza pia kuwaokoa watoto wengi walionyimwa haki zao na vilevile kuwafunza wananchi kuwa polisi hawapaswi kuogopwa bali wao ni marafiki wa umma.

Ili kusisitiza uharibifu wa mazingira mwandishi anaendelea kutumia urudiaji anapoeleza kuwa Tikitimaji hapakuwa na miti mingi katika sehemu nyingi.Msimulizi anasema, '"palikuwa na dalili za kukatwakatwa kwa miti. Hapa na pale palikuwa na magogo ya miti. Hapa na pale palikuwa na alama za magurudumu ya magari labda malori (uk.18).Maneno hapa na pale yamerudiwa ili kusisitiza jinsi miti ilivyokatwa na kusafirishwa kwa malori kumaanisha kwamba malori haya yalikuwa yameidhinishwa kubeba malighafi za ujenzi zinazotokana na miti hiyo. Viongozi wenyewe ndio waliohusika katika ukataji wa miti badala ya kuwa walinzi wa miti ili isikatwe.

Maneno Afande! Afande! Afande! yamerudiwa ili kusisitiza athari za ukoloni katika vikosi vya polisi. Kombo alikuwa askari na anapoulizwa na Maya kama amewahi kusikia kisa cha Jinamizi anajibu kuwa hajawahi kukisikia kwani jeshini hamna fursa ya visa.

Baada ya jibu la Kombo ndipo Maya anamkejeli kwa kusema kuwa kilicho jeshini ni Afande!Afande! Afande! (uk.20). Kauli ya Maya inadhihirisha jinsi askari wa vyeo vya chini wanapaswa kutii amri ya wale walio na vyeo vya juu kwa kunyenyekea na kusujudu hali iliyorithiwa kutoka kwa wakoloni.

Mzee Jududi anayakariri maneno, hamjapotea njia mara mbili anapozungumza na Maya, Zinji, Sapna na Kombo, baada ya vijana hawa kumwuliza kama walikuwa wamepotea njia katika safari yao ya kuelekea Tikitimaji.Vijana hawa wanapomweleza mzee Jududi kuwa walikuwa wanaenda Tikitimaji anashangaa sana, jambo linalowaelekeza kudhani kuwa walikuwa wamepotea njia. Sapna anamwuliza Mzee Jududi,Je, 'tumepotea njia?' Mzee Jududi anamwangalia Sapna kisha anatikisa kichwa polepole kabla ya kuongeza, "La! Wanangu, humjapotea njia...Anapumua kwa nguvu kabla ya kukariri tena, Hamjapotea njia kamwe! Kinachonishangaza ni kuwa mmeamua kuja huku.Njia hii wanayoitumia ni watokao Tikitimaji.Wanaoelekea huko ni wachache mno.Ukufi wa watu tu hata labda unaweza kuwahesabu kwa vyanda vya mkononi" (uk.30).

Mzee Jududi anashangaa kwa kuwa vijana hawa wanne wamejitokeza kujisaka na kujidadisi ili waweze kuyaelewa matatizo ya nchi yao na kutambua ikiwa matatizo haya yanasababishwa na wao (Wanatikitimaji) wenyewe au yanasababishwa na mataifa mengine.Wanaochangia kuharibika kwa mambo mengi ni wengi ilhali wanaojaribu kuyasuluhisha kwa uwazi ni wachache mno.Hii ndio maana Mzee Jududi anawambia kwamba hawakupotea njia ila walikuwa wamechukua hatua ya kijasiri ya kuelekea kule ambako watu wengi wanajaribu kutoka.Yaani Wanatikitimaji wengi hawajali hata ingawa mambo mengi Tikitimaji yanaenda mrama.

Mzee Jududi anapowasimulia Zinji, Sapna, Maya na Kombo jinsi wageni walivyofika Tikitimaji kisha wakakaribishwa na hatimaye ikatokea kuwa watu hao walikuwa wamenunua ardhi yao bila wao kujua, anakariri maneno yafuatayo: "walifika watu! Hata huo mto mliovuka ambao siku hizi hauna maji, chanzo chake ni Tirimacho!" Akapumua na kuendelea, "lakini siku moja, walifika watu.Zinji naye akauliza, "walifika watu?" Mzee Jududi akaendelea,``Ndiyo walifika watu!"Akashusha pumzi na kuongeza, "Nyinyi mmesoma, nadhani mnajua mambo ni kangaja huenda yakaja ina maana gani...Basi siku moja wakafika watu.Sisi tangu zamani tuna jadi ya kuwakaribisha wegeni..." (uk.38-9).

Maneno *wakafika watu* yamekaririwa mara kadha ili kusisitiza jinsi wageni wale walivyofika Tikitimaji, wakakaribishwa na wenyeji na hatimaye wenyeji wakapigwa na bumbuwazi kusikia kuwa wageni wale waliuziwa mlima wa Tirimacho, walikokuwa wameishi wenyenji hawa kwa miaka na dahari.Mlima ulikuwa umeuziwa wageni na kiongozi wa Tikitimaji.

Neno *mlima* limekaririwa kusisitiza kuwa kweli mlima ulikuwa umeuzwa na wageni walikuwa tayari wamepewa cheti cha umiliki wake.Hali hii inadhihirisha udhalimu na unyanyasaji unaotekelezwa na viongozi miongoni mwa jamii ya binadamu. Kwa kutumia mbinu hii ya uradidi wa maneno, mwandishi amefanikiwa kusisitiza dhuluma na unyanyasaji unavyowakumba wanyonge katika jamii ya Tikitimaji.

### 3.9 Hitimisho

Kwa kuhitimisha, tumegundua kwamba mwandishi ametumia tamathali za usemi kwa ustadi na ubunifu wa hali ya juu.Ameoanisha lugha na maudhui kwa njia inayomwathiri msomaji kuwa na hisia tofauti tofauti kama vile chuki kwa wahusika madhalimu,

huruma, kwa wanaonyanyaswa na hata pongezi kwa mashujaa na wanaharakati wa ukombozi ambao wamejitolea kwa hali na mali ili kuona kwamba Tikitimaji imerejea katika hali yake ya awali wakati uongozi ulikuwa bora na wa haki.

Mbinu mbalimbali za uandishi zimetumika katika kazi hii, zikiwemo majazi, taharuki, tashihisi, tashbihi na nyinginezo.Ingawa mwandishi ametumia mbinu hizi, ni dhahiri kuwa mtindo unaomtambulisha ni matumizi ya sitiari ambayo ni mbinu inayoitawala kazi hii.Wamitila amejenga kazi yake katika msingi wa sitiari ya safari ya nchi ya Tikitimaji ambapo wahusika wote wako katika safari na kila mmoja anachangia hatima ya safari hiyo.Safari hii ni ya watu kujisaka ili wajielewe na kuelewa mazingira yao.

Katika kujisaka huku, wanang'amua makosa yao ambayo, kama tuelezwavyo, yanamhusu kila mtawala katili ambaye daima huwa na umma uliomruhusu ama kumpa uwezo wa kutekeleza ukatili wake na kwamba wao wenyewe wamechangia kusababisha matatizo yanayowakabili. Kupitia mbinu hii na nyingine alizozitumia mwandishi kuwasilisha ujumbe wake, tumechorewa hali halisi ya wanyonge wanyongwao, tena katika ardhi yao wenyewe.Hata hivyo, hawa ni wanyonge ambao hatimaye wanaamua liwalo na liwe lakini kwa kuchukua tahadhari kuhusu hatari ya hasira na visasi vinavyoweza kuwadhuru katika harakati za ukombozi wa nchi yao. Kwa hakika mwandishi ametumia sitiari na mbinu nyinginezo za sanaa kwa ufundi mkubwa ambao unaifanya kazi hii iwe na uketo wa kimaudhui na mvuto wa kisanaa.

## SURA YA NNE

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 4.0 Utangulizi

Tumechanganua maudhui na mtindo katika *Tikitimaji* tukiongozwa na nadharia za uhalisia na umitindo.Tumeangazia yaliyomo katika *Tikitimaji* pamoja na mbinu alizotumia mwandishi tukijikita katika lugha ya kitamathali na tumegundua ya kwamba mwandishi, amezioanisha tamathali za usemi alizoziteua na maudhui kwa ufundi mkubwa na kuweza kuwasilisha dhamira yake kwa njia mwafaka kabisa.

Tumeweza kutimiza malengo yetu kwa sababu tulisoma *Tikitimaji* kwa undani na matini nyingine ambazo zilituwezesha kupata mwanga zaidi kuhusu masuala ya kimaudhui na kimtindo.Ilitubidi pia tutafute ushauri kutoka kwa wataalamu wa fasihi jambo lililotuwezesha kuandika kazi bora na ya kiwango cha juu inayoweza kukubalika na kuaminika na wataalamu wengine wa fasihi.

### 4.1 Hitimisho

Mwandishi wa *Tikitimaji* ameyaangazia masuala yanayomkabili binadamu kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kisaikolojia. Migogoro ya kisiasa inatokea wakati viongozi wanaamua kutawala kiimla nao watawaliwa wanafanya uamuzi wa kujikomboa, jambo linalozua upinzani dhidi ya uongozi huo mbaya.

Kuna migogoro ya kijamii ambapo baadhi ya wanajamii wanaamua kuwanyanyasa wanyonge miongoni mwao hususan mayatima ambao wananyang'anywa urithi

wanaoachiwa na wazazi wao.Hatimaye, mayatima hawa hujipata wakirandaranda mitaani na wanaobahatika wanajipata katika makao ya watoto wanakopokelewa na kulelewa.

Wanyonge pia wanadhalilishwa kiuchumi kwa kupokonywa ardhi yao ambayo imekuwa tumaini lao kwa miaka na dahari na kubaki wakiumia moyoni kwa sababu ya mateso mengi wanayoyapitia.Udhalimu huu unatokana na viongozi wanaopaswa kuwa walinzi wa umma.

Wanatikitimaji wanapojaribu kupambana na maovu wanayotendewa na viongozi wao wanakutana na upinzani mkali unaosababisha wapinzani kufurushwa na kuondolewa kwenye makazi yao.Wazalendo wengine wa Tikitimaji wanapoandamana ili kupinga uchafuzi na uharibifu wa mazingira pia wanakutana na upinzani mkali lakini wanajibidiisha hadi wanapofaulu kuunda vuguvugu la WAZALIMA ambalo linajitwika jukumu la kuhifadhi na kutunza mazingira.

Mwandishi anawatetea wanyonge na wanaharakati wa ukombozi kwa kuwa ingawa wanaharakati wa ukombozi hawajafaulu kabisa, wazee wanawausia vijana kuendeleza juhudi za ukombozi hadi watakapofanikiwa nao vijana wanaonekana kuukubali mwito wa wazee wa kuendeleza juhudi hizi.Sapna anapoanzisha vuguvugu la WAZALIMA linakua haraka sana na kuwa kundi kubwa ajabu linalojumuisha hata wazee.Kundi hili linapoandamana ili kuzuia utawala kuendelea kuharibu mazingira linafanikiwa na kuanza shughuli za kuzoa taka jijini Tikitimaji ili kuhakikisha kuwa mazingira yanatunzwa na kuhifadhiwa.Mwandishi wa *Tikitimaji* amelipatia ushindi vuguvugu la WAZALIMA na kwa njia hii amefanikiwa kuukashifu uongozi wa Tikitimaji uliojawa na ujuhali mwingi.

Wakati mwandishi wa kazi ya sanaa anapowazia kuandika sharti awe na malengo fulani katika uandishi wake.Waandishi huenda wakaandika ili kuwakosoa binadamu, kuwaadilisha, kuwaonya, kuwatahadharisha, kuwasifu au hata kuwakashifu.Wamitila ameandika kazi yake kwa kutumia lugha inayomwathiri msomaji kiasi cha kumfanya awaonee huruma wanaonyanyaswa na kudhulumiwa na wakati huo huo awachukie madhalimu.Hisia hizi zinampa msomaji funzo kuwa wanajamii wanapaswa wawe waadilifu nao waovu wanapaswa kujikosoa na kujirekebisha kitabia.Hadhira ya mwandishi huenda ikapania kutenda haki hasa ikiwa inahusishwa na uongozi nao wanaodhulumiwa huenda wakapania kujikomboa kwa kila njia.

Kazi hii vile vile inawafundisha wanajamii kuwa mambo fulani yanapoenda kombo katika jamii zao, watu binafsi wanapaswa kujitolea na kutafuta suluhisho kwani mambo haya huwaathiri wanajamii wote. Katika utafiti wetu tumegundua kuwa masuala anayoyaangazia msanii katika *Tikitimaji* yanashabihiana sana na matukio yanayotendeka miongoni mwa wanajamii ulimwenguni.

Masuala kama vile uyatima, makao ya watoto, uharibifu wa mazingira na uchafuzi wake, unyakuzi wa ardhi ya wanyonge, kufurushwa kwa viongozi wa upinzani, watoto kuhusishwa na ukahaba na wengine kupata riziki zao kwenye majalala ya taka yanadhihirika wazi nchini Tikitimaji. Haya ni mambo tunayoyashuhudia katika jamii zetu hasa katika mataifa yanayoendelea.

Ugunduzi huu ndio uliotufanya kuchagua nadharia ya Uhalisia kuwa dira ya kutuongoza katika uchanganuzi wa maudhui ambapo tumegundua kuwa mwandishi wa *Tikitimaji* amefanikiwa kuangazia maswala yanayoakisi hali halisi ya maisha ya binadamu na

kwamba, msomaji yeyote wa kazi hii anaweza kukiri kwamba, mambo yaliyoangaziwa ni ya kuaminika na kwamba, mambo haya hushuhudiwa katika takribani kila jamii ulimwenguni.

Kuhusiana na upimaji wa nadharia tete ambazo tuliziwasilisha kama maswali ya utafiti, tumegundua kwamba nadharia tete zote zimesadifu kuwa za kweli kwani lugha ya kitamathali ambayo mwandishi ameteua kuitumia katika uwasilishaji wa maudhui imeafikiana kabisa na maudhui yenyewe.Kauli hii ni ya kweli kwa sababu kila wakati ambapo mwandishi alitaka kusisitiza maudhui fulani alitumia tamathali mwafaka ya usemi ili kutimiza lengo fulani katika muktadha uliohusika, kama tulivyoeleza katika Sura ya Tatu.Maelezo haya yanathibitisha ukweli wa nadharia tete yetu iliyodai kuwa, mwandishi ameteua mbinu za kimtindo zinazoafikiana na maudhui anayoyaangazia katika *Tikitimaji.*

Nadharia tete yetu ya pili ilidai kuwa, mwandishi wa *Tikitimaji* ameangazia maswala ambayo yanaakisi hali halisi ya maisha ya binadamu.Kauli hii imetokea kuwa ya kweli kwa sababu maswala yote tuliyoangazia katika Sura ya Pili ni matukio ambayo yanadhihirika wazi katika jamii nyingi ulimwenguni.Baadhi ya maswala haya ni pamoja na ukiukaji wa haki za watoto ambapo watoto huzaliwa kisha wakatupwa na wazazi wao badala ya kutunzwa na kulelewa wanavyostahili na vilivile watoto wadogo kutumika danguroni.

Mwisho, tulikisia kwamba mwandishi wa Tikitimaji amefanikiwa katika uwasilishaji wa kazi yake, jambo linalotokea kuwa la kweli kwa sababu nadharia alizotumia kuwa msingi wa kazi yake hazina utata.Yaani, nadharia ya Uhalisia inadhihirika wazi katika kazi hii

kwa kuwa matukio yanayoangaziwa, mandhari na wahusika walioteuliwa kuyaangazia ni vya kihalisia kabisa.Matumizi ya lugha pia yameitia kazi hii mvuto na mnato wa kiujumi kwani lugha iliyotumika imechangia kuyatia maudhui uzito na kuwachangamsha wasomaji au hadhira kwa jumla.

## 4.2 Mapendekezo

Kama tulivyotangulia kusema katika sura ya kwanza, kazi ya mwandishi mmoja inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti tofauti na wahakiki mbalimbali.Kwa mantiki hii, napendekeza kwamba kazi hii inaweza kuchunguzwa na wahakiki wa baadaye kwa sababu hatujashughulikia masuala yote yanayopaswa kuchunguzwa.Sisi tumeangazia maudhui na mtindo na hasa tumejikita katika matumizi ya lugha.Wahakiki wa baadaye wanaweza kuchunguza masuala mengine kama vile:

(i) Mbinu nyinginezo za fasihi kama vile majazi, taswira, taharuki na kisengere nyuma zinavyotumika katika uwasilishaji wa ujumbe.

(ii) Usawiri wa wahusika na jinsi uteuzi wao unavyochangia kuendeleza dhamira na kujenga maudhui.

## MAREJELEO


Arege, T. (2009) *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd.

Caleb, C.W (2013) *Taswira ya Mwanake Katika Tamthilia za Nguzo Mama na Mama Ee.* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Hegel, G.W.F (1979) *Introduction to Aesthetics*. Oxford: Clarendon.

Holman, C.H (1936) *A Handbook to Literature*. New York: Odyssey.

Kamunde, M.E (1983) *Kilio cha Wanyonge katika Riwaya za Said Ahmed Mohammed*. Tasnifu ya shahada ya uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi.

King'ei, K. na Kemoli, A. (2001) *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Limited.

King'ei, K. na Ndalu, A. (1989) *Kamusi ya Methali*.Toleo Jipya.Nairobi: East African Educational Publishers.

Kuvuna S.M na Wengine (1992) *Nuru ya Ushairi: Mwongozo na Uchambuzi*. Nairobi: KLB.

Lukacs, G. (1963) *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Press.

Matei, A.K (2011) *Fani ya Fasihi Simulizi Kwa Shule za Upili.* Nairobi University Press.

Mbatiah, M. (2002) *Kamusi ya Fasihi*.Nairobi: Standard Textbooks.

Mberia, K. W (2001) *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mdee, J. (1986) *Kiswahili: Muundo na Matumizi yake*.Nairobi: International Publishers Ltd.

Mgullu, R.S (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi:Longhorn Publishers.

M'Ngaruthi, T.K (2008) *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohammed, S.A (1995*) Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*.Nairobi: East African Educational Publishers.

___________ (1980) *Utengano*.Nairobi: Long horn Publishers.

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*.Nairobi: East African Educational Publishers.

Ngure, A. (2003) *Fasihi Simulizi Kwa Shule za Sekondari*.Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Senkoro, F.E.M.K (1982*) Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Wafula, R.M na Njogu, K. (2007*) Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

,Wamitila, K.W (2002*) Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

___________ (2003*) Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*.Nairobi: Focus Publications Ltd.

___________ (2003*) Kichocheo Cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

____________ (2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

____________ (2013*) Tikitimaji*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.